ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 2 Juni, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika nakushukuru, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naomba kuwasilisha hati mezani. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 16

Tatizo la Uingiaji wa Maji ya Bahari katika Maeneo ya Kilimo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya ardhi za kilimo. Na kwa kuwa katika Wilaya ya Mkoani, kambi ya Chuo cha Mafunzo Kengeja, Skuli ya Mwambwe, Jombwe na Sipwese ni baadhi ya maeneo yaliyoathirika na kadhia hii ya uingiaji wa maji chumvi, ikisaidiwa na lile tuta lenye urefu wa mita 100 linalounganisha Jombwe na Sipwese ambalo kwa sasa limevunjika.

(a) Je, ni kweli kwamba uingiaji wa maji haya umesababishwa na kubomoka kwa tuta hilo.

(b) Kama ni kweli, serikali imesaidia nini katika kujenga tena tuta hilo *(re-construction*).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 16, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Kama inavyofahamika kuwa baina ya kijiji cha Jombwe na Sipwese, Mkoa wa Kusini Pemba kuna tuta ambalo lilijengwa mwaka 2004, hii ilitokana na kuanza kuingia kwa maji ya chumvi mwaka 2002 katika eneo katika eneo hilo ambalo lilikuwa ni kiunganishi kati ya sehemu hizo mbili. Tuta hilo lenye urefu wa zaidi ya mita 100 mbali ya kuwa ni kizuizi cha maji ya chumvi yanayoingia katika maeneo hayo, lakini pia tuta hilo limetumika zaidi kama kivuko kati ya maeneo hayo mawili.

Wananchi walitumia tuta hili kama ni njia ya kwenda Mwambe na wanafunzi walilitumia kama ni njia yao ya kwendea Skuli ya Mwambe. Mwaka 2010 tuta hilo lilianza kubomoka na hatimae ikawa rahisi kwa maji ya chumvi kuweza kupita na kuelekea maeneo ya Sipwese na Chuo cha Mafunzo Kengeja. Kubomoka kwa tuta hilo kumetokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na baadhi ya wananchi walivunja mawe yaliyokuweko kwenye tuta hilo hasa wavuvi wa samaki aina ya "bombwe" ambao walivunja tuta hilo ili kuruhusu samaki hao wapite na waweze kuwanasa katika mitego yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa ruhusa yako tena naomba kuleta majibu muwafaka kwa swali la Mhe. Mwakilishi, namba 16 kama ifuatavyo:-

a) Uingiaji wa maji ya chumvi katika maeneo hayo haukusababishwa na ubomokaji wa tuta hilo, bali kwa kiasi kikubwa umetokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababishwa na shughuli mbali mbali zinazofanywa na binaadamu na hivyo kupelekea kina cha baharí kuongezeka. Uingiaji wa maji ulianza mwaka 2002 wakati tuta lilijengwa mwaka 2004. Hata hivyo, kwa kuwa tuta hilo limeshaanza kubomoka, ni wazi basi kwamba maji ya chumvi yataendelea kuingia katika eneo hilo.

b) Serikali kwa sasa haijasaidia katika kujenga tena tuta hilo. Kama sote tunavyofahamu na ambavyo nimekuwa nikieleza ndani ya Baraza hili, serikali imezindua Mkakati wa Zanzibar wa Mabadiliko ya Tabianchi, kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa mkakati huo, serikali inaanda mpango kazi wa utekelezaji mkakati huo ambapo utayarishaji mpango huo unategemewa kumalizika mwezi Januari, 2016 kwa hatua za uhamasishaji wa nyenzo za utekelezaji. Mpango huo ndio utakaotoa dira ya kuweza kuyashughulikia maeneo yaliyoingia maji ya chumvi ambayo yapo 145 Unguja na Pemba. Utekelezaji wa maeneo yanayoingia maji ya chumvi

ikiwa ni pamoja na maeneo ya Sipwese na Jombwe utafanywa hatua kwa hatua kutegemea na upatikanaji wa fedha za Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi ambao unatayarishwa.

Hata hivyo, ni juhudi za kupunguza kasi ya maji ya chumvi kuelekea maeneo ya Sipwese na Chuo cha Mafunzo Kengeja. Serikali ikishirikiana na wananchi wa Jombwe kupitia ushirika wa *(Green Peace and Environmental Conservation – GPEC)* na wananchi wa Sipwese kupitia ushirika wao wa kuhifadhi mazingira imeweza kupanda miti ya mikoko/mikandaa katika maeneo hayo. Jumla ya hekta 3 za miti hiyo zimepandwa katika eneo hilo na imeendelea kustawi vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, kuwa marefu naomba kumuuliza maswali mawili tu madogo ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabianchi ni tatizo linaloikabili dunia hivi sasa mwaka huu wa fedha wa serikali anayeongoza yeye wizara hiyo imetenga kiasi gani cha kutatua tatizo hilo na ukizingatia hali ya Mwambe, Jombwe, Sipwese wananchi wake hali zao ni za chini. Kuna hatua gani za dharura za kuokoa tatizo hilo kwa wananchi wake wanyonge hasa ukizingatia kazi yao kubwa ni kugonga gonga mawe kule Mwambe. Hilo la kwanza.

La pili, tatizo la mabadiliko ya tabianchi mbali ya kuathiri sekta ya kilimo na wananchi wanaoishi katika ukanda wa pwani kama vile Jambiani, Paje, Bwejuu na kwengineko, nyumba zao nyingi zimeanza kumong'onyoka. Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao ukizingatia, serikali ni wananchi na serikali hii isingekuwa madarakani bila ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, serikali kwa mwaka huu wa fedha kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atakumbuka vizuri katika fedha za maendeleo zimetengwa jumla ya shilingi 450 milioni kwa kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Lakini vile vile ofisi kupitia Idara ya Mazingira itapata fedha za ziada za kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi kutokana na Mfumo wa Mabadiliko ya Tabianchi ambao nao utapata fedha zake kutokana na Mfuko wa Miundombinu ambao umeanzishwa na bajeti hii.

Kuhusu suala la maeneo ambayo yameathirika hasa kwa wakaazi wa nyumba, ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira tumekuwa tunafanya ziara mbali mbali ili kukagua sehemu hizo na tumekuwa tunashirikiana na Halmashauri zinazohusika na sehemu hizo ili kuona kwamba wananchi hawatoathiriwa na kuweza kuleta majanga katika visiwa vyetu. Ushauri uliotoka ndani ya serikali ni kwamba, kama kuna wananchi ambao tayari nyumba zao zimo katika fukwe na zinaathiriwa na

uingiaji wa maji basi serikali ifanye jitihada ya kuwatafutia viwanja ambavyo viko eneo la juu ili waweze kutengeneza makazi yao ili kuepusha majanga.

Mhe. Spika, tumelifanya hilo katika maeneo ya Kisiwa cha Pemba katika eneo linaloitwa Mjini Kiuyu, tumefanya hivyo na tumeweza kuhamisha familia kama 16 kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na kuweza kuwapatia maeneo. Nyumba hizo 16 zilikuwa tayari wakati wa maji makubwa hawawezi kulala kwa sababu maji yalikuwa yanaingia ndani ya nyumba zao. Kwa hivyo, nawashauri Waheshimiwa Wawakilishi wote kama katika maeneo yao ipo hali hiyo washirikiane na ofisi yetu kupitia Idara ya Mazingira ili tuone tunashirikiana vipi na Halmashauri za Wilaya ili kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, katika suala la mtandao mzima huu wa mto wa Jombwe hadi Sipwese na kufikia pale katika Chuo cha Mafunzo Kengeja, lakini mtandao wa mto ule umetambaa hadi katika maeneo ya nje ya Maumbwini hadi kuelekea Mto Mkuu, ambako kunaelekea kuathirika hadi katika maeneo hayo.

Je, kuna mpango gani kuhakikisha kwamba athari hii haitaingia katika maeneo hayo ya Mto Mkuu pamoja na Maumbwini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba maeneo zaidi ya 145 kwa sasa katika visiwa vya Unguja na Pemba yameathiriwa na uingiaji wa maji ya chumvi. Maeneo aliyoyataja ni miongoni mwa maeneo hayo. Sasa katika hatua za awali tunawashauri sana wananchi wa maeneo hayo kuweza kuchukua hatua za kupanda miti ya mikoko ili kuzuia uingiaji wa maji ya chumvi hayo wakati serikali inaendelea na juhudi zake za kuandaa utekelezaji wa mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, mwaka 2013 Mhe. Waziri na timu yake alifuatana na Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani kushiriki zoezi la upandaji miti Shehia ya Mwambe kwenye kikundi cha *Green Peace and Environmental Conservation* ambayo miti ile imestawi vizuri sana.

(a) Mhe. Waziri, atakuwa tayari wiki hii kabla ya mwezi wa Ramadhani kupanga ziara na Mhe. Mwakilishi ili wakaone matunda ya miti hiyo waliyoipanda na ilivyostawi.

(b) Upandaji wa miti hii inasaidia sana kuhifadhi na kufanya hewa ukaa ambapo Mashirika ya Kimataifa *UNESCO* na wengine wamekuwa wakitoa misaada kwa wale wanaopanda miti kuhifadhi hewa ukaa. Ni kwa nini wananchi wa Shehia ya Mwambe ambao yeye alishiriki kupanda miti na imestawi hawajapatapo kupata msaada wowote kutoka wizara yake wala Idara ya misitu hata kwenye fungu la hewa ukaa ambalo linatolewa na *UNESCO*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tulikwenda kufanya shughuli ya upandaji miti katika maeneo hayo katika jitihada za kuzuia maji ya chumvi yasiendelee kutuathiri katika maeneo yetu. Niko tayari kufuatana naye pale muda utakapokuwa muwafaka ili kwenda kufanya ziara ya kukagua kazi ile ambayo tumeifanya lakini pia kuhamasisha katika maeneo mengine wananchi waweze kuendelea kupanda miti hiyo.

Jibu lake la pili ni kwamba, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira bado haijafaidika na fedha ambazo yeye amezitaja za hewa ukaa kutoka *UNESCO*. Sisi tunafahamu kwamba suala hilo bado lipo kwenye mazungumzo na nchi zinazoendelea bado hazijafaidika katika suala hilo.

TAARIFA

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nimekubaliana na majibu ya Mhe. Waziri, lakini mimi Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ambayo inashughulikia Wizara ya Kilimo na Maliasili, Idara ya Misitu imekuwa ikikusanya hii fedha kutoka *UNESCO* ambayo inawasaidia wananchi wanaopanda miti Zanzibar. Sasa Idara yake ya Mazingira ndio inayo-*coordínate* mambo haya ya mazingira. Nimshauri Mhe. Waziri na nimuombe aende Idara ya Misitu wakafanye mawasiliano ili waone fedha inavyoingia Zanzibar na kwa nini idara yake haifaidiki na hilo. Naomba kumuelekeza hivyo tu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, ametoa taarifa hiyo sijui kama una maneno yoyote Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba kupokea hiyo taarifa, lakini ni vile tunavyoeleza kwamba suala la mazingira ni *cross-cutting*. Sasa katika suala la upandaji miti *per say* kwa maana ya kupanda miti liko kilimo, sisi suala letu kubwa ni kuhakikisha kwamba mabadiliko ya tabianchi hayatuathiri. Lakini kwa kufanya hivyo tunashiriki katika jitihada za pamoja za kupanda miti pamoja na kilimo, nachukua ushauri wake na kuona jinsi gani wananchi wa maeneo hayo wataweza kufaidika na fedha hiyo ambayo imepokelewa kilimo.

Nam. 63

Msongamano Katika Barabara ya Soko la Mwanakwerekwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kabla ya kuuliza swali langu Nambari 63, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri, ukizingatia leo ni siku yake ya kuzaliwa. Lakini nataka nimkumbushe tu sisi Waislamu tunatakiwa tutafakari na kuzingatia. Je, umri unakwenda mauti yanakaribia, huko biashara gani aliyofanya na Mwenyezi Mungu. Baada ya maelezo hayo nimtakie *birthday* njema na naomba swali Namba 63 ambalo linamuhusu yeye na yeye ni muathirika mkubwa wa suala hili lipate jawabu.

Kumekuwepo na msongamano mkubwa wa gari katika eneo la barabara ya sokoni Mwanakwerekwe, msongamano huo kwa utafiti wangu unasababishwa na gari zinazogeuza katika sehemu finyu ya barabara hiyo ambayo imeachwa bila kuzibwa kama zilivyozibwa sehemu nyengine za mpindo wa barabara hiyo.

(a) Kwa kuwa eneo hilo limekuwa na shughuli nyingi kwa hivi sasa, kwa nini sehemu za kugeuzia gari za barabara hiyo zisizibwe zote na badala yake gari zote zinazotaka kugeuza zitumie barabara ya Mwanakwerekwe Makaburini.

(b) Kuendelea kuziacha gari zigeuze hapo hapo sokoni si kunaendelea kuongeza msongamano usiokuwa wa lazima.

(c) Serikali ina njia mbadala ya kuondoa msongamano wa gari katika barabara ya sokoni Mwanakwerekwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 63 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, eneo analolisoma Mhe. Mjumbe ni eneo ambalo katika kipindi cha miaka saba takriban hivi sasa limekuwa na harakati nyingi sana za kimaisha na kibiashara. Aidha, serikali kwa kuliona hilo imeingiza baadhi ya huduma ili kukabiliana na changamoto kama hizo. Imeweza kuongeza ujenzi wa barabara

mpya kutoka ile barabara moja iliyokuwepo kabla, lakini pia tumeongeza barabara ya dharura kwa matumizi ya kawaida au kwa kuzingatia hali maalum kwa kujenga barabara ya Mombasa hadi Nyumba mbili.

Hata hivyo, tunakiri kuwepo kwa changamoto kubwa hasa panapotokea athari yoyote ya kupelekea barabara ya Fuoni hadi Tunguu kuonekana kama kisiwa. Wizara yangu tunaangalia jitihada maalumu za kuimairisha barabara za ndani kama vile barabara ya ndani Amani, Magogoni hadi Nyarugusu, barabara kutukoa Mombasa hadi Meli tano Fuoni. Lakini pia ile barabara ya Fuoni hado kutokea Maungani.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba ipi haja na hoja ya wizara yangu kwa kupitia Idara husika ya ukitunzaji na ujenzi wa barabara pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni kuendelea kukutana na kujadiliana na wenzetu wa Jeshi la Polisi kitengo cha Usalama barabarani ili tuendelee kuona namna gani kwa kujadiliana na mapana kuweza kukubaliana hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

Aidha, tunapenda kusisitiza matumizi ya usimamizi wa sheria husika kunaweza kutupunguzia kwa kiwango kikubwa sana tatizo liliopo hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa ujumla matumaini yetu kwamba barabara hiyo itaweza kutumika vizuri bila ya bughuza yoyote pale tu tutakaposimamia vyema husika. Tunaomba Jeshi la Polisi kusimamia kwa dhati kabisa taratibu husika kwa kudhibiti maeneo yote yaliyopo hapo ili madereva wasiyatumie kinyume kwa wakati ambao utapelekea usumbufu na msongamano kwa watumiaji wa barabara husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba kuwa kumsaidia kidogo kwa kumbukusha maswali mawili madogo.

(a) Kwa kuwa barabara za Mchina zimejengwa na tatizo bado lipo Mhe. Naibu Waziri, kwa kutumia Baraza hili ni hatua gani unaweza kutueleza ulizozichukuwa hasa dawa ya kidonda ni kutibu kidonda na sio kukifuga hilo moja.

(b) Kwa kuwa waathirika wa foleni katika eneo hilo akiwemo yeye mwenyewe Mhe. Naibu Waziri, hasa kwa sababu anakosishi katika maeneo hayo njia hiyo ya barabara haioni ni mfano unakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo mashimo mengi pale na bado tatizo hilo lipo au vile vile tutamtegemea Mkuu wa Mkoa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama na eneo lile kulifungu kufunga kupunguza foleni kufanya barabara moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, eneo analolizungumzia Mhe. Mwakilishi ni eneo ambalo liko mbele ya Soko la

Mwanakwerekwe. Jitihada za serikali kwa mara ya kwanza tuliongeza laini ya pili ya barabara kukawa na barabara mbili moja inayoelekea shamba na moja inayokuja mjini. Lakini bado kumeonekana kuna tatizo na tatizo hili linatokana kwamba barabara ile ina maeneo maalum ya kuweza kupinda kwa gari ama kurudi mjini au kurudi shamba.

Mategemeo yetu ni kwamba tumekaa na wenzetu Jeshi la Polisi tumeona kwamba kama watasimamia vizuri hasa kwa nyakati za asubuhi kunaweza kukapelekea sehemu kubwa ya kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo hili la foleni.

Lakini jambo jengine kwamba barabara hii ya kupita Mombasa kutokea nyumba mbili ipo na madhumuni yake ni kusaidia inapotekea dharura na nina hakika mwenyewe Mhe. Mwakilishi anathibitisha hilo. Kipindi kilichopita hapa baada ya kunyesha mvua barabara ile ilikuwa ndio manusura ambayo ilikuwa inasaidia wananchi kuweza kutoka mjini kwenda katika barabara ya Fuoni.

Tunakiri kwamba bado tuna tatizo kubwa la ufinyu wa barabara na ndio maana tukaeleza katika majibu ya msingi kwamba tumeona kwamba ipo haja ya kuendelea kuimairisha barabara inayotoka Amani, Magogoni mpaka Nyarugusu, barabara inayotoka Mombasa mpaka Meli tano ili kuweza kuongeza *traffic* iwe rahisi kwa watu wanaotoka mjini, ama wanaotoka maeneo ya Fuoni kuja maeneo ya Mjini.

Tunatambua kwamba ongezeko la magari, mahitaji ya huduma katika eneo lile hatutokuwa na nafasi ya kuwazuia watu wasiende eneo la Sokoni, lazima tujipange vizuri kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wale wanaokuja Sokoni kwa kufuata huduma za Sokoni waweze kupata utaratibu mzuri na hayo ndiyo malengo ya serikali.

Jambo la pili, amezungumzia suala la mashimo. Barabara hii ni kama kiumbe kadiri inavyotumika ndivyo inaathirika na kama tutapata matatizo yoyote wajibu wetu ni kujenga, ni kweli barabara zetu zimeathirika hasa maeneo ya Fuoni kwa kutokana na mvua kubwa. Lakini sisi kama serikali yale maeneo ambayo yameharibika tunahikikisha tunafanya haraka kuweza kuyarejebisha.

Lakini jambo la ziada kwamba tayari serikali tumeshatangaza Zabuni barabara ya Fuoni eneo la Mwanakwerekwe mpaka Fuoni Polisi tayari barabara hii imeshatangaziwa Zabuni mkandarasi amesapatikana na tunaamini kwamba itaanza kujengwa muda mfupi kuanza hivi sasa.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ndogo.

Mhe. Spika, mimi nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri hii barabara ya Mwanakwerekwe matatizo yake ni kama tunavyoona ya gari nyingi zinazopita, pana Makalbi mengi sana barabara ile na watu wanaathirika wengine wanajigonga, hivi nasikia mtoto pale kajigonga na kakatika mguu na kaumia. Yale makalbi ni lini yataondolewa?

Pili, anasema kuwa barabara kweli zinaharika kwa ajili ya mvua nyingi, ni sababu zipi za kuwa hamuwezi kufanya barabara za ndani za dharura kutokea barabara inayotokea hapa Mwanakwereke kuingia ndani kutokea Amani ambayo kuwa ikaweza watu kuwasaidia katika ile misongomano itakapokuwa kunatokea dharura naomba majibu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Alijibu:-

Mhe. Spika, makalbi tunayoyasema hapa ni tofauti na yale ambayo anayasema Mhe. Jaku Hashim Ayoub ya kule Bandarini na makalbi yaliyowekwa hapa ni kwa hayo malengo ambayo tulikuwa tunayataka sote yawe hivyo. Makalbi haya yamewekwa katika maeneo yale ambayo yanamapengo ya barabara kwa ajili ya kuweza kupinda ama ukarudi huku ama ukenda upande wa pili.

Kwa uwekwaji wa makalbi haya ni kwa ajili ya kuzuia magari yasifanye ile *return* kwa ajili ya kukimbia huo msongamano ambao upo. Kwa hiyo, makalbi hayo akisema tutayaondosha lini, hatuyaondoshi ila tumeyaweka makusudi kwa ajili ya kudhibiti watu wanaofanya *return* kwa ajili ya kupata matumizi mazuri ya barabara.

Mhe. Spika, sababu za barabara za dharura, tumeeleza kwa mara nyingi tu kwamba jukumu letu la msingi ni kujenga barabara kuu. Lakini kwa kutambua uwezo mdogo wa Halmashauri zetu, sisi tuko tayari kutoa kila aina ya msaada kuweza kuona huduma hizi za usafiri hasa za barabara zinaimarika.

Kwa hiyo, barabara za ndani ziliopo ziko ambazo serikali kuu tumeanza kujenga na tuaendelea kujenga na tumeleza katika jibu la msingi kwamba tumeona kwamba kuna tatizo na ndio maana tumesema tutaimarisha barabara ya kutoka Amani-Magogoni Nyarugusu inaungana na barabara ya Fuoni, tutaimairisha barabara ya Mombasa mpaka Meli tano inaungana na barabara ya Fuoni. Lakini pia tutaimarisha barabara ya kutoka Fuoni mpaka Nyamazi ili kuweza kuona kwamba usumbufu huu unaondoka. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, alichouliza Mhe. Raya Suleiman, kuna alama yoyote itawekwa kwenye makalbi kutokana na watu kijigonga na wengine kukata miguu, ni vizuri suala alilosema Mhe. Naibu Waziri, lakini wangeweka alama yoyote kunusu maisha ya wananchi, ni hilo tu.

Mhe. Spika: Hilo litakuwa ni swali jengine la Nyongeza ambayo tayari ulikwisha pata nafasi kwa hiyo nafasi sasa iende kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad, swali la mwisho la nyongeza kama ni taarifa basi nishaichukuwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, Mhe. Waziri, katika kutoa majibu yake alizunguza barabara ya Nyumba mbili kuwa imesaidia na kutumika vizuri hasa ule wakati palipokuwa na mafuruko na hivyo barabara kuu kufungwa.

Kwa sababu barabara hii wakati huo ilikuwa ikitumika kulilazimisha kuwe na mpango mpya kwa gari zote zinazotoka mjini kupitia hiyo barabara ya nyumba mbili. Lakini gari zinazotoka Fuoni na kadhalika kueleka Mjini kuna krosi ya mwanzo pale ambayo kulikuwa na barabara ya kifusi yenye mashimo gari zote ilikuwa zipite na ilikuwa ikisaidia sana ili usafiri uwe mzuri. Kwa sababu hivi sasa hali ilivyo Mwanakwerekwe ni kama ilivyoekezwa. Mhe. Waziri, haoni kuwa upo umuhimu wa kufanya haja ya dharura kuona kuwa kile kipande ambacho kina mawe na mashimo makubwa pia kitengenezwe ili usafiri wetu uweze kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeona ipo haja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, amekimbia bila ya kumwambia sasa akushukuru. Hata hivyo, namshukuru sana, tunaendelea.

Nam. 76

Mgao wa Gari za Misaada

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: - Aliuliza:-

Mnamo tarehe 27 Septemba, 2014 Shirika linaloshughulikia idadi ya watu ulimwengini *UNFPA* ilitoa msaada wa magari manne (4) kwa Wizara ya Afya ili kupunguza idadi ya vifo vya mama wajawazito na watoto.

(a) Mhe. Waziri, anaweza kunieleza mgao wa magari hayo ulikwendaje.

(b) Mara nyingi wanaotupa hiyo misaada wanahimiza sana utunzaji wa misaada wanayotoa. Je, Mhe. Waziri, anaweza kunieleza ni mara ngapi amezifanyia ukaguzi gari hizo ili kuona kwamba kweli gari hizo zinatunzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kumpongeza sana ndugu yetu Naibu Waziri mwenzangu ndugu Issa Ussi Gavu kwa kutimiza miaka 28.

Naomba niungane na Mhe. Jaku Hashim Ayoup, katika pongezi hizo na kumtakia kheri na neema maana pale nilipokuwa nimekaa nae Mhe. Jaku Hashim, alitoa wazo la neema zake zimetumika vipi, yaani atafakari kila baada ya muda amshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema alizomjaalia. Sasa na yeye kanithibitishia kwamba ikifanywa hesabu mpaka sasa hivi *Alhamdulillah* katumia neema hizo vizuri sana, naomba nimpongeze. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 76 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika ni kweli kwamba mwezi wa Septemba 2014 Shirika linaloshughulikia idadi ya watu ulimwenguni yaani *UNFPA* lilitoa msaada ya magari manne kwa Wizara ya Afya ili kupunguza kampeni maalum ya kupunguza idadi ya vifo vya mama na watoto.

(a) Mhe. Spika, magari hayo hayo yamegaiwa kwa upande wa Unguja gari 2 na kwa Pemba gari 2, haki imekuwa sawa kwa wote; kwa upande wa Unguja Hospitali zilizopatiwa gari hizo ni Hospitali ya Kivunge na Muwembeladu na kwa upande wa Pemba ni Hospitali ya Micheweni na Chake Chake. Safari hii Mnazi Mmoja haikupata kitu.

(b) Mhe. Spika, napenda kukuhakikishia kuwa magari hayo yanatunzwa na yamepatiwa bima aina ya *fully comprehensive,* pia yanakaguliwa na Mkuu wa usafiri wa Wizara ambaye ndiye dhamana Mkuu wa ukaguzi wa magari hayo yote na kufanyiwa *services* kila pale inapostahiki. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, ni mara nyingi madereva wengi wanaoendesha gari za serikali huwa hawana uchungu na magari hayo ya SMZ, wanaendesha magari bila ya uangalifu.

Je, wizara yako imeshawahi kuwachukulia hatua madereva walioharibu magari hospitali kwa uzembe?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Wizara ya Afya imeshawi kuwachukulia hatua madereva ambao wamekuwa wazembe na magari hayo na inaendelea kuhakikisha kwamba magari hayo kwa sababu ni ya kuokoa maisha ya mama na watoto madereva wanaochukuliwa hapo ni *experienced* ili isiwe upande mmoja tunaokoa maisha na upande wa pili tunaondosha maisha kwa ajali.

Kwa hivyo, tunachukuwa madereva ambao *experienced* na wale wamekuwa wazembe washawahi kuchukuliwa hatua. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kusemakama wanaagalia madereva wanaondesha gari vizuri ili kuokoa maisha ya watu ni vizuri sana. Lakini napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa madereva wanafanya kazi za gari hizi za Hospitali mchana usiku bila ya kupumzika, wanakuwa hawana mapumziko kwa ajili ya kuchukuwa wagonjwa na kwa kuwa wanaendesha gari hizi kwa uangalifu, lakini Mhe. Naibu Waziri, wizara yake haina kuwapa maposho ya ziada madereva wanaofanya kazi usiku mchana kuokoa maisha ya watu.

Je, ni lini wizara yake itaona kama hawa madereva na wao wanastahiki kupewa maposho ya zaida na kuongezwa mishahara yao ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Ahsante sana, kwa kweli madereva wanaingia kwa *shift* kwa sababu huwezi kumuweka dereva mmoja masaa 24 hasa ukizingatia kazi za gari hizi ni kazi maalum za kubebea wagonjwa na wakati mwengine huhitajika kidogo kwenda mwendo wa kasi kwa ajili ya kuwahisha wale wagonjwa, ndio maana kunahitajika *experience* kubwa.

Kwa hiyo, wanaingia kwa *shift* mbili hivi sasa na tunaendelea kufanya utaratibu wa kupunguza masaa yao au saa zao wanazofanya kazi. Kwa upande wa maposho jana tu tulikuwa tumebahatika tumekaa na Mhe. Waziri kwenye kikao tukawa tunazungumzia kuhusu zile *allowances* za **On call Allowance** na mambo mengine, yaani *benefits* zao nyengine. Hatua hizi tunaendelea kuzizungumza mpaka pale tutakapopata pase wale wote wanaodai, basi tutahakikisha wanapatia pesa zao sio wao tu wako wengi wako kada ya madaktari na kada ya wauguzi ambao wao wanakuja *overtime* wanaoitwa usiku kukiwa na *emergence*. Kwa hayo, yote tumo katika mchakato wa kuyashughulikia ili walipwe. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwanza naomba nimpongeze sana Mjukuu wangu hapa Mhe. Issa Haji Gavu, kwa kutumiza miaka 28 na hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anamzaa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuwa watu wa visiwa vidogo vidogo wanapenda sana kula *marine food* kama vile pweza, ngisi pamoja na chaza, jambo ambalo linapelekea sana wao kupata uzazi kwa wingi, yaani watu wanakuwa wanazaa sana katika visiwa vidogo vidogo kama vile Tumbatu, Fundo, Kisiwa Panza, Uvinje na kwa kuwa gari hazifiki katika visiwa ili kunusu vifo vya mama na watoto, yaani kwa kuwa gari hazifiki katika visiwa vidogo vidogo. Je, ni lini serikali itatufuta *speed boat* ili kupunguza vifo vya mama na watoto katika maeneo haya ya Tumbatu, Kisiwa Panza, Fundo na Uvinje pamoja na Makoongwe. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Kabla sijamruhusu Mhe. Naibu Waziri, kujibu hilo swali kwa utamaduni wetu Mhe. Issa Haji Ussi, kwa utamaduni wetu kwa umri huu wa kula, yeye itakuwa ni wa mwisho kunawa katika Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi/Kicheko)*

Mhe. Naibu Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza naomba nimshukuru kwa swali zuri sana. Mheshimiwa, huwa mara nyingi anauliza swali ambalo linatoa fursa pana ya jamii pia kuelimika, kwa sababu tunasikilizwa na wananchi hapa. Kwa hivyo, mara nyingi huwa anauliza swali ambalo linakuwa pana na wananchi wanaweza kuelimika.

Mimi naomba nikubaliane naye kwamba wale wanaotoka katika visiwa hivi na vile vyakula alivyotaja wanavyokula hasa hawa samaki aina, maana yake wanaitwa samaki, jamii ya samaki kama pweza, ngisi, chaza. Hawa ndiyo wenye *protein* zaidi ile *protein* maalum ya *almovement* ya kusababisha uzazi kuwa mkubwa zaidi kuliko samaki wengine wowote. (*Makofi*)

Mara nyingi watu huwa wanadharau samaki hawa na kuona aah! hichi ni chakula cha maskini au yule anayebakia mwisho ndiyo anakula, samaki wakubwa wote wanauzwa kwenye hoteli za kitalii na kadhalika. Lakini ukenda nchi nyengine samaki hawa ndiyo wanakuwa ghali zaidi kuliko samaki tuliozoewa kula kama changu na *king fish* ama nguru. Hilo naomba nikubaliane.
Lakini pili imekuwa imesadifiwa vizuri kwamba jana tu tulikuwa tunajadiliana suala la Visiwa vya Tumbatu, Fundo, Kisiwapanda kwa sababu tunataka kufanya ziara pamoja na wenzetu hawa wa *WHO* pamoja na *UNFPA*, kwa sababu

tumemaliza maeneo yote mengine bado hatukwenda huku visiwani na tunaelewa pia kama kuna matatizo mbali mbali, hivi karibuni tuliangalia *TV,* ule upepo na hali ya hewa ilivyokuja, tunaelewa.

Kwa hivyo, ninaomba nimuhakikishie kwamba huduma zinazokuwepo sasa hivi zinaendelea kutolewa katika visiwa hivyo na vipo kama Tumbatu, ninadhani vipo vituo zaidi ya viwili. Hivyo, huduma zinaendelea kutolewa ila sisi tunakwenda kuifanya huduma iwe bora zaidi na kutanua ule wito, kwa sababu tumeshaona kitakwimu pale pana nyongeza ya uzazi kuliko sehemu nyengine yoyote.

Tumbatu inachangia sana takwimu za Mkoa wa Kaskazini Unguja katika uzazi, kwa sababu wao ndiyo wanaoongoza. Kwa hivyo, Mheshimiwa, ninakushukuru sana kwa swali hilo na tunaendelea na harakati hizo ulizotoa mawazo hayo na hivi karibuni tu Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaweza kuweka sawa mambo.

Mhe. Spika, ahsante.(*Makofi*)

Nam. 67

Upimaji wa Mipaka ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba swali Nam. 67 ambalo nina hakika jawabu lake limekuwa kizungumkuti lakini wacha lipate jawabu.

a) Serikali haioni ipo haja ya kukaa upya na kuangalia utaratibu wa kugawa mipaka katika Mji Mkongwe ikiwa kuanzia barabara ya Bwawani kuelekea Hospitali ya Mnazi Mmoja eneo hilo likawa la Mji Mkongwe ili kupitisha ujenzi wa Bwawani usiwe na vipingamizi ili iwe kazi rahisi.

b) Je, Serikali iko tayari kulifanyia kazi wazo hili na inatoa kauli gani ukizingatia ujenzi wa pale unahitaji ghorofa 15 na kuendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Nam. 67 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe imewekwa kisheria tangu 1994 katika *Act No. 3* na kuthibitishwa tena katika marekebisho ya sheria hiyo katika mwaka 2010 kwa *Act No. 4.* Mji Mkongwe wa Zanzibar umeingizwa katika orodha ya urithi wa

Kimataifa kwa kufuata sheria hiyo pamoja na mpango mkuu wa uhifadhi *(Conservation plan).* Haja ya kukaa upya na kuangalia utaratibu wa kugawa mipaka upya katika Mji Mkongwe kuanzia barabara ya Bwawani kuelekea Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kupitisha ujenzi wa Bwawani usiwe na pingamizi. Hili ni suala ambalo lipo kinyume na sheria na mpango mkuu wa Mji Mkongwe. Inabidi ombi hilo liwasilishwe upya *UNESCO* kama sheria na taratibu za *UNESCO* zinavyosema.

Mhe. Spika, Serikali haijakuwa tayari kulifanyia kazi wazo hilo kwa sababu zilizokwishaelezwa hapo juu, lakini pia ikiwezekana kugawa mipaka kwa kubadilisha sheria, kazi ambayo ni ngumu sana kukubalika na eneo hilo litakuwa ni *buffer zone* ambapo kwa sheria ya *UNESCO* hairuhusiwi kujenga majengo marefu yatakayozidi ghorofa tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu ya kusikitisha sana ya kutokuwa na afya na hasa masuala yanayohusu Mji Mkongwe, unakuwa ukweli haupatikani.

Mimi ninataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kuwa mimi sikupinga kuwa Mji Mkongwe haikuwekwa sheria, ninajua imewekwa kisheia, lakini mamlaka hii ambayo haifuati Sheria ya Mamlaka ya Mji Mkongwe, imekuwa ikifanya kazi zake kwa ubaguzi, hilo suala halitaki tochi wala upendeleo.

Na kugawa mipaka ninafikri siyo Wizara yake ni Wizara ya Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ndiyo inayogawa mipaka, hivi nyengine zinashuhudia tu. Lakini pamoja na hayo katika jibu lako Mhe. Naibu Waziri, umesema kuna majengo hairuhusiwi zaidi ya ghorofa tatu katika maeneo yale, kwa maana hiyo isizidi ghorofa nne.

Kuna sababu gani wengine wamekwenda kuomba kujenga ghorofa tatu mpaka hivi leo hawajapewa na maelekezo yameshatoka, kuna uzito gani na barua zimeshapelekwa kutoka kwa Katibu Mkuu lakini Mkurugenzi amepewa muda mrefu barua zile akazikalia, hakuna jawabu inayopatikana.

1) Huu siyo ubaguzi, ndiyo utendaji bora au ndiyo utawala bora. Ni lini Mkurugenzi ataanza kujibu angalau zile barua.

2) Kwa eneo lile la Bwawani Serikali imekuwa ikipiga kelele kwa muda mrefu sana shimo liliopo mbele na kutafuta mwekezaji, kuna taarifa kuwa mwekezaji kapatikana kuwekeza katika eneo lile ambalo limekuwa ni uchafu na mazalio ya mbu na majambazi kujificha ndani katika msitu ule. Kwa kweli mwekezaji shimo lile atakuja kujenga

ghorofa tatu. Huu u-*seriousness* upo wapi. Haya majawabu unapotoa Mhe. Naibu Waziri uyafanyie utafiti kwanza, wananchi wanatusikiliza na hichi chombo ni cha wananchi, tumekuja hapa kutetea masuala ya wananchi. Kwa ghorofa tatu pale haji mwekezaji kuja kuwekeza katika eneo lile.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nataka nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara yangu haifanyi kazi kiubaguzi, inafanya kazi kwa mujibu wa sheria na inamfanyia haki kila mwananchi ambaye anayestahiki kufanyiwa haki. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kama kuna suala la mtu ambaye kajenga nyumba ya ghorofa tatu kinyume na utaratibu basi Mhe. Jaku, aje atufahamishe zaidi ikisha na sisi tutalifualia ili tujue ukweli halisi upo wapi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri, suala la ujenzi wa Mji Mkongwe kwa zaidi ya ghorofa tatu limezungumzwa kwa zaidi ya miaka kumi sasa, na kila ambapo Mhe. Waziri, anaomba Wawakilishi wakumuoneshe hizo nyumba.

Leo yupo tayari baada ya majibu tukamuoneshe hizo nyumba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Nipo tayari kwenda katika hayo maeneo pamoja na Maafisa wangu, siyo mimi peke yangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na majadiliano na leo tuna wageni, vijana wetu. Wageni hao leo wamekuja kwa ajili ya mafunzo kuona namna gani tunafanya shughuli zetu.

Wageni waliopo wanatoka Skuli ya Machui, jumla yao wapo 36 na wamefuatana na walimu wao watatu. Walimu waliofuatana nao ni:

1. Mwalimu Sadik John
2. Mwalimu Berita Trasias
3. Mwalimu Pandu Mkombe

Wanafunzi hao pamoja na walimu wao naomba sasa wote wasimame ili kuwatambua Waheshimiwa Wawakilishi, wale pale. (*Makofi*)

Walimu na wanafunzi karibuni sana katika ukumbi wetu ili muone na mujifunze shughuli zetu hizi. Ahsante.

La pili, Waheshimiwa Wajumbe, nimepokea dharura mbali mbali kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe, ambao wana mambo ya msingi kuhitaji kufanya safari. Sasa kama tunavyoelewa shughuli zetu hizi tunakabiliwa na tatizo la mahudhurio. Pale ambapo *quorum* inakuwa ipo *Alhamdulillahi* kama ilivyo sasa, ni vizuri tukazingatia kuitumia *quorum* hiyo.Vyenginevyo, shughuli zetu zitakuwa zinakwama na hazitoweza kuendelea.

Mumeona huko nyuma tulivyokuwa tangu tuanze shughuli zetu hizi. Mara nyingi tunakuwa na upungufu mkubwa sana wa Akidi katika Baraza hili. Sasa ili kukidhi baadhi ya maombi ambayo yana umuhimu na pia ili kukidhi hata mimi pia nina tatizo moja kubwa leo. Basi inafaa shughuli hii kwa idadi hii tuimalize hivi kipindi cha asubuhi na ili tupate wasaa kidogo, zile dharura muhimu ambazo wameniambia lakini pia na kupitisha hoja hii iliyopo mbele yetu pia ina umhimu yaweze yote kutekelezeka kwa siku ya leo na pengine kesho.

Basi niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao tumeleta maombi ya kuchangia, waliobaki kama nilivyowatamka jana ni Wajumbe wanane na tisa kaongezeka leo asubuhi. Ni dhahiri hatatoweza kuwasikiliza wote, hata

tukipunguza muda kwa kiasi gani, mwishowe itakuwa haina maana hata kumwita Mjumbe ukamwambia changia kwa dakika tano.

Sasa niwaombe basi kwanza tutumie dakika kumi kumi na Mjumbe ambaye atakuwa na maelezo kidogo tukiamini kwamba mengine mengi yameshazungumzwa na wengine, basi atumie ufundi labda kusema tu anaunga mkono yaliyosemwa na fulani au hata akiacha, ili tuhakikishe kwamba inapofika kiasi cha saa tano, nimuombe Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho ili kumaliza hoja hii. (*Makofi*)

Kwa utaratibu inawezesha yale maombi mbali mbali tukaweza kuyatekeleza lakini na jambo hili muhimu pia likaweza kutekelezeka kwa ufanisi. Naomba sana tufanye hivyo na baada ya hayo basi naomba twende kwa utaratibu huo.

Waheshimiwa Wajumbe, ninawashukuru sana kwa usikivu wenu. Majadiliano sasa yanaendelea na kwa maana hiyo nimuomba Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, afuate Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali, kama hayupo hiyo nafasi ndiyo imekwenda na baadae Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Mwanaidi, karibu kwa dakika kumi.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa dakika kumi, mimi kwangu zinanitosha.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikawa na afya njema na asubuhi hii nikawa ya mwanzo katika kuchangia hotuba hii. Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kutuwasilishia hotuba ya Makadirio na Mapato kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, hotuba hii imewasilishwa vizuri sana na ninamwambia Mhe. Waziri hongera sana, tena sana. Mhe. Spika, pia, niwapongeze kwa dhati kwa watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya na kumpa mashirikiano mazuri Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niendelee na mchango wangu niende katika Idara, Mamlaka za Serikali za Mikoa. Kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yote ya Zanzibar kwa kazi nzuri wanazofanya. Kusema kweli wanajitahidi hasa katika masuala haya ya ulinzi na usalama.

Kusema kweli kila mtu mwenye macho haambiwi tizama. Wakuu hawa wa Mikoa wanafanya kazi zao vizuri, ninawapongeza sana. Pia, baada ya kuwapongeza

Wakuu wa Mikoa niwapongeze na Wakuu wa Wilaya, kusema kweli Wakuu wa Wilaya nao wanafanya kazi vizuri, wanawapa mashirikiano Wakuu wao wa Mikoa na kazi zinaonekana zinafanyika vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea niende katika Halmashauri. Niwapongeze Makatibu wa Halmashauri zote za Zanzibar; Unguja na Pemba. Mhe. Spika, kusema kweli watendaji wote katika Halmashauri wakishirikiana na Makatibu wao wamefanya kazi vizuri hasa hii ya ukusanyaji wa mapato. Kusema kweli mapato mpaka kufikia asilimia 77 kwa Halmashauri zote, kusema kweli wanastahiki pongezi lakini wajitahidi waongeze jitihada ili ipatikane ile asilimia waliokuwa wamejipangia.

Mhe. Spika, Halmashauri zetu kusema kweli zinafanya kazi vizuri, zinatekeza majukumu waliokuwa wamejipangia. Kwa hivyo, naomba jitihada zao ziongezeka kuona yale yote wamejipangia katika mwaka wanayafanikisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea niende Idara Maalum ya SMZ. Mhe. Spika, kwanza nivipongeze Vikosi vyote vya SMZ kwa kazi nzuri wanazozifanya, hasa zile za ulinzi, kilimo na nyingi nyenginezo. Mhe. Spika, pamoja na kazi nzuri basi tuwaangalie tena askari hawa kuhusu maslahi yao.

Pia, Mhe. Spika, tuangalie kama wenzangu walivyokuwa wameanza kutangulia kusema kuhusu upandaji wa vyeo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, basi pale inapofika wakati wa kupandisha vyeo, wafuate taratibu kama walivyokuwa wamejipangia ili tuone malalamiko yanaondoka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo katika Vikosi na kutoa pongezi zangu nyingi sana; Vikosi vyote vya SMZ kwa kazi nzuri wanazozifanya ninawaambia hongera sana. Mhe. Spika, niende katika Kikosi cha KMKM. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kusema kweli Kikosi hichi kinajitahidi kwa kazi nzuri ya ulinzi wa doria, uokozi na udhibiti wa magendo. Kama hotuba ya Mhe. Waziri alivyotuwasilishia ni kweli wanafanya kazi zao vizuri, kazi za doria wanafanya vizuri, kazi za uokozi na kudhibiti magendo. Hivi sasa tukizingatia tulikuwa tuna utaratibu wa kusikia asubuhi kwenye taarifa zetu kwamba kumekamatwa boti, lakini sasa hivi *Alhamdulillah* kikosi hiki kwa kazi yake nzuri kimejitahidi kudhibiti magendo.

Pamoja na kazi hiyo nzuri ya ulinzi pamoja na doria, pia, Kikosi hiki cha KMKM niwape pongezi nyingi sana kwa kutoa huduma za matibabu mbali mbali kwa mama wajawazito na watoto katika Hospitali yao ya KMKM. Kusema kweli kama Mhe. Waziri, hotuba yake inavyojieleza kwamba Kikosi hiki cha KMKM kinafanyakazi ya mama wajawazito na watoto na kutoa chanjo mbali mbali, ni

kweli kwa sababu hata wananchi wetu wanakisifu sana kituo hiki, wananchi wetu wanatoka katika maeneo mbali mbali kwenda kupata tiba katika kituo hiki, pia nawapa hongera sana.

Vile vile, Mhe. Spika, niwape hongera kwa kufuatilia ahadi, ambazo aliahidi Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kusimamia Hospitali ya KMKM, kwa programu ya mafunzo ya miaka mitatu. Nawaambia hongera sana na wazidi kufuatilia ahadi nyengine zilizotolewa na viongozi wengine.

Mhe. Spika, nikitoka katika Kikosi hiki cha KMKM, niende katika Kituo cha Mafunzo. Mhe. Spika, pia na wao niwape hongera nyingi sana Kikosi hiki cha Mafunzo. Kama tutakumbuka nyuma tulikuwa tunapiga kelele hapa kuhusu chakula cha wafungwa, lakini sasa hivi *Alhamdulillah* chakula kinapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Unazo dakika tatu.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Namuomba Mhe. Waziri. ili azidi kulisimamia vizuri na kuona wafungwa wetu wanapata chakula vizuri.

Pia. nije katika Magereza Wete. Mhe. Spika, pale tulikwenda kusema kweli ofisi ya kituo kile hairidhishi wala haipendezi kusema kweli ofisi ni ndogo haina nafasi. Lakini katika maeneo wanaowekwa wafungwa wanawake. Mhe. Spika, inasikitisha sana kusema kweli japo kuwa wanawake sio wakorofi sana, lakini lile eneo lililokuwa limetengwa kwa wao sio zuri wala halistahiki kuwekwa mwanamke. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa vile umeniambia bado dakika tatu, nataka niende katika Ofisi ya Msajili na Kadi za Vitambulisho. Kwanza Mhe. Spika, ofisi hii naipongeza sana kwa kazi zao nzuri wanazozifanya. Pamoja na wajumbe wamesema kuna sheria Nam. 7 ya mwaka 2005. Kusema kweli Mhe. Spika, sheria hii tumeipitisha sote humu Barazani, sasa mimi nashangaa kuona kwamba wengine hii sheria ndio kwanza wanaishangaa kama vile ndio kwanza mpya. Lakini hii sheria tumeipitisha sote humu Barazani na wewe ukatuuliza, tukakubali na tukaipitisha. Sasa leo nashangaa watu kuhoji sheria hii, wakati sheria hii tumeipitisha humu humu Barazani.

Mhe. Spika, tumezowea masuala haya. Tulivyoanza kuingia Barazani humu kulikuwa kuna malalamiko, ooh! Vikosi vya KMKM, sijui SMZ, kisha wametulia. Tumekuja tena ooh! Tume ya Uchaguzi imetulia. Tumekuja tena ooh! Mashaha, Masheha kisha imetulia. Sasa tumekuja tena tunaanza kuwagusa majeshi. Lakini Mhe. Spika, hayo tumeyazowea.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na muda ni mdogo, tunataka tuchangie wajumbe wote tuliokuwa hapa. Basi Mhe. Spika, kwa niaba ya Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwanaidi Kassim, tunakushukuru na tunakushukuru pia kwa kuokoa muda. Nimkaribishe basi Mhe. Mohammedraza Hassanali hayupo, nafasi hiyo ndio imekwenda. Mhe. Subeit Khamis Faki, baadae Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Nassor Salim Ali, anajitayarisha. Mhe. Subeit Khamis.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa na mimi kuchangia kidogo hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, muda kidogo ni mdogo, lakini nitatumia hivyo hivyo pamoja na udogo wake ninaoupata. Mhe. Spika, kwa sababu ya muda sitaki nisifu sana kwanza nataka niende moja kwa moja kwenye *point*, kwa sababu nikisifu sana muda wangu nitakuwa naupoteza. Isipokuwa na mimi nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kusoma hotuba yake kwa umahiri mkubwa kabisa, nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza napenda nianze katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Micheweni. Mhe. Spika, nawapongeza sana Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, kwa kujenga jengo zuri kubwa la kisasa la ukumbi wa mikutano. Lakini Mhe. Spika, jengo hili limekwenda kwa kasi kubwa, lakini naona sasa hivi limesita. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri, aniambie tu ni kikwazo gani ambacho kimefanya jengo lile lisite kidogo.

Pia, namuomba Mhe. Waziri, anifafanulie, lilikadiriwa lile jengo kutumia kiasi gani cha fedha, na limeshatumia kiasi gani hivi sasa na mpaka kumalizika kwake sasa hivi linakadiriwa litatumia kiasi gani cha fedha. Kwa sababu tunataka na sisi tujuwe kwamba je, fedha za walipa kodi zimetumika kiasi gani.

Mhe. Spika, baada ya Halamashauri yangu ya Wilaya ya Micheweni kuwapongeza na kuwasifu kwa jengo wanalojenga zuri, naomba kidogo nizungumzie suala la sehemu za Tawala za Mikoa na hasa katika Mkoa wa Kusini Pemba, ukizingatia kama Mji wa Chake Chake na pamoja na Mkoani ni Wilaya maarufu, kwa sababu wafanyabiashara wote wa Pemba karibu wote tunategemea Chake Chake. Lakini masikitiko yangu ni kwamba mpaka sasa hivi Chake Chake hakuna soko ambalo linaweza likawakidhi Wapemba na wakajua kama wanakwenda kwenye soko lao Pemba la kufanyabiashara.

Mhe. Spika, sasa hivi utaona soko la Katari ni soko ambalo lilikuwa linabeba watu katika Wilaya ya Micheweni, Wilaya ya Mkoani, Wilaya ya Chake Chake na Wilaya ya Wete na baadhi ya wilaya nyengine. Lakini ukienda Katari wenyewe ukipaangalia hapafai hata kupita mara moja, maana ni pachafu, barabara mashimo, tope, ni balaa tupu Mhe. Spika.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie suala hili, kama bado hatujapata soko la kudumu, lakini pale Katari basi paangaliwe pafanyiwe angalau matengenezo kidogo iwe panaweza kupitika na watu wanaweza kufanya biashara zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa naomba nizungumzie tena kuhusu suala la *stand* ya magari. Bado hatujaweza kupata *stand* ya magari Chake Chake. Mnatuambia tu mtajenga sehemu ile lakini hatujui lini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, angetueleza hasa wamefikia hatua gani ya kuona kwamba tunapata *stand* ya kutambulikana, kwa sababu Chake Chake ni mji wetu tunaotegemea kwa Pemba nzima.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nimuulize Mhe. Waziri, ni suala la ujenzi wa Makao Makuu ya KVZ kule Micheweni. Mhe. Spika, pale wananchi walikuja kulalamika na mimi nilizungumza naye Mhe. Waziri, kwamba wanalalamika wananchi wamechukuliwa maeneo yao, yaani mashamba yao bila ya kupewa fidia ya aina yoyote ile. Kulikuwa na baadhi ya minazi ilikatwa, lakini wale wenye maeneo hawakupata fidia ya aina yoyote. Sasa namuomba Mhe. Waziri, akija anijibu kama suala hili limefikia uwamuzi ama limefikia hatua gani, kuona kama wale wananchi wameridhishwa na wao kwa kulipwa fidia katika maeneo yao yanayochukuliwa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakuja katika suala la kuboresha Tawala za Mikoa, kuboresha Madaraka Mikoani. Mhe. Spika, kama ilivyozungumzwa kama wadi zote Pemba zilikuwa 141, lakini katika kuangalia kwake na upunguzwaji wake zimepunguzwa wadi 30. Sasa katika wadi zile zilizopunguzwa 30, wadi 25 ni Pemba na wadi 5 ni Unguja. Jana Mhe. Hamza Hassan Juma, alikuwa akitoa ufafanuzi, na hapa nina masikitiko sana Mhe. Spika. Masikitiko yangu ni kwamba sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, tunachangia kumuomba waziri atupe ufafanuzi wa masuala haya.

Lakini sasa tumekuwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ndio mawaziri tunaowajibu wenzetu wakichangia. Hii sio busara nzuri, na wakati huo huo Mhe. Spika, humu Barazani tuliomo sote ni wanasiasa, hakuna asiyekuwa mwanasiasa. Leo ukimwambia waziri kwamba jibu hoja zilizokuwa sio za kisiasa na za siasa uziwache, humu ni nani asiyekuwa mwanasiasa na sote tumekuja kwa kupitia vyama vya siasa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwanza watu wasijifanye wao ndio mawaziri humu wakawajibu wenzao. Sisi tunamuuliza waziri, waziri ana nafasi kubwa ya kukaa kule mbele akatujibu, kwa nini tunajibiana sisi kwa sisi humu, hii sio desturi nzuri. Sasa Mhe. Spika, nikienda kwenye hoja yangu. Nauliza katika hizo wadi zinazokatwa na Mhe. Hamza Hassan, alisema kwa sababu zimekatwa Pemba kuna watu 400,000 na Unguja kuna watu 900,000, ndio sababu ya kukatwa zile wadi 25 Pemba na huku Unguja zikakatwa wadi 5.

Mhe. Spika, sasa namuuliza Mhe. Waziri, huku nyuma wananchi wa Zanzibar walikuwa ni 300,000 tulikuwa na wadi hizi hizi 141. Leo tumeongezeka tumefika watu 1,300,000 inakuwaje badala ya kuongezwa zipunguzwe. Huku Unguja zimepunguzwa kwa nini na kule Pemba kwa nini wakati tumeongezeka? Sasa hiki si kitu cha ajabu kwamba leo watu wameongezeka zinapunguzwa, pale tulipokuwa kidogo zipo nyingi, lakini sasa tumeongezeka zimepunguzwa ni sababu ipi ya msingi mpaka zipunguzwe.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa masikitiko kabisa mara zote tukija humu Barazani tukichangia, basi tunasema Wilaya ya Micheweni inaongoza kwa umaskini. Leo kama Wilaya ya Micheweni inaongoza kwa umaskini, mnataka kila mkija kwenye vitabu mutuongeze kutuandika kwamba Wilaya ya Micheweni inaongoza, kwa umasikini. Nasema hili kwa sababu maalum. Wilaya ya Micheweni ukitoa Shehia ya Mgogoni, ukitoa Shehia ya Kinyasini na ukitoa Shehia ya Finya ndizo eneo ambazo zina karafuu, ndio maeneo ambayo yana mikarafuu na ndio maeneo ambayo tunajidai kama Wilaya ya Micheweni na sisi tunatoa mapato ya serikali ya kitaifa.

Leo ikiwa maeneo yale yametolewa yamepelekwa Wete, tumebakiwa na kijijararo kidogo cha mawe, Mheshimiwa, mnataka kila siku mkija sisi mtutie kwenye vitabu kama Micheweni inaongoza kwa umasikini. Sasa hata huruma hamtuonei. Ukitoa maeneo na ukipeleka kale ndio maeneo ambayo yana uchumi wa nchi. Sasa mnayapeleka kwenye wilaya nyengine mnatutolea sisi Wilaya ya Micheweni mnatuelekeza wapi.

Pili, kwenye sheria Mheshimiwa, alisema kama hazitapungua katika wilaya wadi 10, sisi tumebakishiwa wadi 8, kwa nini tubakishiwe wadi 8 Wilaya ya Micheweni na wakati sheria huku inasema hazitapungua kwenye 10, leo tumebakishiwa wadi 8 tu sisi. Hivi sisi mnatufanya kama kule Micheweni hatuna roho na hatuna jinsi. Halafu wakati huo huo Mhe. Waziri, ulipokuwa ukipanga hizo wadi ulikuwa uangalie, ni lazima muangalie na muwaulize wananchi. Lakini mnakichukua kama kieneo cha kisiwa cha Kojani. Kisiwa cha Kojani ilikuwa ni wadi tena ni kisiwani wameitoa wakaipeleka Wadi ya Mchangamdogo, wawaelekeza wapi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Unadakika tatu Mheshimiwa. Dakika tatu Mheshimiwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Jamani mambo yanakwenda na huruma ni lazima twende na huruma. Tukija kusema humu mnatuambia tunalalamika na tumezowea kulalamika. Tunalalamika kwa sababu mnatufanyia yasiyokuwa na ingekuwa mnatufanyia mazuri tusingelalamika.Tunalalamika kwa sababu mnapofanya mambo yenu hamuangalii, hamna fungu la huruma, mnatufanyia kama sisi hatustahiki, mnatutenga, ni lazima tulalamike. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, tukija kwenye suala hili la vitambulisho mnatuambia tunalalamika. Lazima tulalamike. Leo kuna watu wamepiga vitambulisho vyao tangu mwezi wa 10 uliopita hawajavipata, kuanzia Januari mpaka mwezi wa 6 huu hawajavipata, watu wana vikaratasi, watu wanakwenda kupiga vitambulisho leo na wanapewa leo, wao wamezuiliwa hawapewi, halafu mnatuambia tumezowea kulalamika.Tunalalamika kwa haki yetu, hatulalamiki tu, kwa sababu tunalalamika mnatufanyia mambo siyo, na ndio maana tukalalamika. Ingekuwa mnatufanyia ndio basi tusingelalamika. *(Makofi)*

Leo kuna mtu amekwenda kujiandikisha. Juzi nilimwambia Mhe. Waziri, alikwenda kujiandikisha kitambulisho chake, akaenda hana cheti cha kuzaliwa asipewe, akahangaika amepima damu mpaka kapata cheti za kuzaliwa. Amekwenda kuandikisha tangu mwezi wa Januari, baada ya kuandikisha kapewa risiti ya kuchukulia kitambulisho chake, hata vitambulisho vimeshakuja yeye anakwenda anaambiwa amewekewa pingamizi na nani, ni Mkuu wa Uandikishaji, kwa sababu gani. Tangu mwaka 2000 hajaandikisha kaja kutaka kitambulisho mwaka huu, sina cheti na huku sheria inasema uwe na cheti. Leo nimeshapata cheti nakuja mnaniwekea pingamizi ya aina gani hiyo. Jamaa zangu mambo mnayoyafanya siyoo na ndio maana tukalalamika jamani. Mkifanya vitu mfanye mkiwaangalia na wenzenu.

Leo wanachukuliwa watu, hamjifichi kamwe katika hao watu mnaowachukua wakienda kujiandikisha, kwani mnataka ushahidi unajificha, hamjifichi. Mkija hapa mnasema CCM ina mtaji mwingi, hamna mbinu mnatumia nguvu tu, wala msiseme kama mnambinu nyingi, hamna mbinu. Mnalolitumia nyinyi ni nguvu, kwa sababu mnanguvu. Leo vyombo vya ulinzi mnawaingiza kwenye mambo ya siasa, nyinyi mnasema kwamba hamuwaingizi, mnawaingiza kwenye mambo ya siasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Haya.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Waheshimiwa, nawaomba sana mnapofanya mambo yenu basi mfanye kwa uangalifu msitufanye kama sisi ni watoto wadogo, basi iwe

sisi tunakuja kulalamika huku, mtuite watoto wadogo, au tumekosa akili sisi humu. Tunakuja kusema mambo humu kwa sababu tunayaona, mnatufanyia na tunayaona.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Haya, ahsante sana Mheshimiwa muda umemalizika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mimi siungi mkono mpaka nipate hoja zangu.

Mhe. Spika: Haya. Unajua tatizo la kusema kwa ukali, nimeliona jana kwa Mhe. Abdalla Juma Abdalla, aliomba maji haraka pale. Lakini *Inshaallah* ikitokea hivyo tutapeleka maji. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Marina Joel Thomas. Hayupo, nafasi hiyo ndio imeruka. Mhe. Nassor Salim Ali, hayupo nayo imekwenda. Mhe. Mohammedraza Hassanali sasa itabidi uandike kwa maandishi nafasi yako ilikwisharuka. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said, baadae Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nikazungumza machache asubuhi hii ya leo. Mhe. Spika, pia, nichukuwe fursa hii kumshukuru waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, niseme machache na niende kwenye majukumu muhimu ambayo sisi wawakilishi yanatulazimu kuyafanya. Moja ni kutunga sheria, kuwakilisha wananchi, kupitisha bajeti na kuihoji baadae serikali juu ya matumizi hayo. Baada ya bajeti kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, kuna majukumu mengine ambayo yanafuata kwa taasisi nyengine ambayo ni *CAG*. *CAG* anajukumu la kutoa *grand of credit* na baadae kuyakagua mahesabu hayo.

Mhe. Spika, Ofisi hii ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina majukumu mazito sana. Moja ni kudumisha amani, ulinzi na usalama katika mikoa, wilaya na mashehia, pia, kulinda mali za Taifa na za watu binafsi zisiharibiwe, kuzuwia uingizaji na utoaji nje ya nchi kimagendo, pamoja na kusimamia kazi za uzimaji moto na uokozi. Mhe. Spika, kwa kweli niiombe serikali kwanza fedha zitolewe kwa wakati na kisha fedha zile zielekezwe hasa kule zinakokusudiwa.

Mhe. Spika, mimi naishukuru sana serikali kwamba kuanzisha huu mfumo wa kibajeti ambao unakwenda moja kwa moja kwenye *programme*, naamini mfumo huu utaleta ufanisi.

Mhe. Spika, katika kitabu hichi na katika yale yale majukumu nimeona kuna taasisi ya vitambulisho ambayo wenzangu wengi wameshaisema kwa kweli kama

alivyosema kwamba tumepitisha sheria kama sisi Wawakilishi ndio tumepitisha sheria, lakini jambo la kushangaza kila mtu anapokuja hapa anasema maneno mengi. Mhe. Spika, kwa kweli na mimi nashangazwa sana jambo lolote kwanza dhana ni mbaya, nitoe hadithi moja.

Siku moja kuna mtu na mkewe na mfanyakazi wake, siku moja yule mfanyakazi baada ya kufanya kazi za ndani ya nyumba akaenda chumbani kule kwenda kuweka sawa nako, kaona kitanda kimetandikwa vizuri akakitizama kile kitanda akaona na mimi nikionje hiki kitanda, kitanda kizuri kama hivi kimetandikwa kwa hivyo nilale, si usingizi umemchukua pale, akaja bwana yule alipokuja na yeye akaona huyu bibi leo kalala mapema na yeye akalala kwa dhana ile ile ya kwamba anaona mwenziwe ameshalala kajifinika, kujifinika pale sasa kaja mwanamke mama mwenye nyumba alipofika pale kashangaa ilikuwaje, mbona leo kuna watu wawili wameshalala huyu mwengine katoka wapi.

Sasa hiyo ni dhana yule kafikiria ni mkewe aliyelala na yeye kalala, kumbe yule ni mfanyakazi, kuja kufanya utafiti na utafiti ni jambo zuri zaidi, kumbe anakuta dume, wote kuja kutizamana kila mmoja anamtizama mwenziwe, kwa hivyo, niseme ile kitu dhana, dhana ni jambo baya sana na unaweza kudhania jambo likakufikisha pahala pabaya. Mimi naamini kwamba majeshi wana kazi zao na mara nyingi kazi zao wanafanya kwa kujiamini kabisa, tuwaachie wafanye kazi zao, sasa hivi ni kipindi ambacho kuna ajira, ajira nahisi haifanywi mahala popote lazima wanafanya kwenye makambi yao, kwa hivyo, ningewaambia tu wenzangu tuwe na uhakika wa mambo yale tunayoyasema.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri, ametuletea vitabu vitatu na vyote ni muhimu katika kuchangia na kuvichanganua vitabu hivi, ukurasa wa 49 kwenye kitabu hiki cha utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mitaa, kwa kweli kitabu hichi kila palipogusa kwenye Halmshauri huku ni uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato jambo ambalo ni la msingi kabisa, ningeishauri Serikali mcheza kwao hutunzwa, pale panapokusanywa vizuri basi watizame na hasa madiwani wetu, kwa kweli bado hali zao ni duni wanapata posho tu, basi pale angalau palipokusanywa vizuri basi na wao waweze kuangaliwa.

Mhe. Spika, niseme kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye programu kubwa na programu ndogo, naamini baada ya kupitishwa fedha hizi basi mara nyingi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kunakuwa na matatizo ya ufungaji wa mahesabu, niwaambie watendaji wa Wizara hii ni muhimu kufuata zile Sheria za fedha na Sheria za manunuzi, ni muhimu kuwa na madaftari ya kutunzia mali na pia tuwe na ufanisi mzuri wa kuweka mahesabu yale, kwa sababu mara nyingi hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zinakuja kwenye kufunga mahesabu, mahesabu yanakuwa hayapelekwi kwa wakati na kwa kila mwaka

tarehe 30 ya Mwezi wa Septemba, inatakiwa hesabu zile ziwe zimeshafika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini mara nyingi mtu anaingojea mpaka ile tarehe 30, kumbe hisabu za mwaka tunafunga hapa mwezi wa Juni, Julai tunaanza hesabu mpya kwa kila mwaka wa hesabu.

Lakini mtu anangojea ule mwezi wa mwisho ule ndio anapeleka mahesabu yale na baadae kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakuwa ni tatizo, kwa sababu Serikali ni lazima ifunge mahesabu yake na kujua kwamba ina mali gani na ina uwezo gani.

Kwa hivyo, mkikosesha kuzipeleka hesabu hizi mapema kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inakuwa kwa kweli ule uwajibikaji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kweli inakuwa ni tatizo, kwa hivyo, Mhe. Spika, niwaombe.

Mhe. Spika: Unazo dakika mbili.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, niwaombe baada ya kuzipata fedha hizi basi tuzitumie vizuri pale tunapopalenga hasa.

Mhe. Spika, nikushukuru sana na pia kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani wenye imani na mimi na mimi nina imani na wao, naunga mkono hotuba hii ya Waziri asilimia mia kwa mia. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha siku ya leo nikiwa mzima, lakini vile vile nakushukuru wewe kwa kunipa muda wako wa kuchangia hotuba hii ya Ofisi kubwa sana Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum, kwa kweli hii Wizara ni Wizara muhimu inayohusiana na maisha ya watu wetu. Wizara hii inahusiana na utawala mikoani, wilayani, masheha, kwenye vikosi vyetu , wadi zetu, Halmashauri zetuna Mabara ya Miji yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli usimamizi wa Wizara hii unahitaji umakini mkubwa sana, usimamizi wa Wizara hii Mhe. Spika, hauhitaji kuonyesha ushabiki wa kisiasa, ukiruhusiwa ushabiki wa kisiasa nchi itagawika kwa mwelekeo wa vyama, naomba kumpa indhari Mhe. Waziri wa Ofisi hii kwa maoni yangu mambo hayaendi vizuri, usimamizi wa kazi katika taasisi hii yanaachiwa yaende bila ya kukaguliwa vizuri.

Mhe. Spika, naomba nitoe mfano kwa mujibu wa Sheria tumekubaliana Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni watumishi wa umma, lakini leo hii Mhe. Spika, na hili nishawahi kulisema humu Barazani utawakuta wamevaa gwanda la chama cha siasa au wamekaa maskani ya chama, iweje leo viongozi wa umma wavae sare za

chama na watembee mitaani. Mhe. Spika, hebu Mhe. Waziri, atuambie hii ina maana gani.

Mhe. Spika, mimi kama mimi Mkuu wangu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa hata avae magwanda ya Chama, alale nayo akiamka nayo ikiwa hayamkeri basi mimi hayanikeri na nikiwa na shida yangu ambayo inawahusu wao nitawafuata kwa sababu nawajua tokea hapo mwanzo wanatoka upande gani, lakini hapa lazima itizamwe sheria na kwa kweli Mhe. Waziri, ikiwa atayaachilia mambo haya yaendelee wanachama wa Chama alichovaa sare mtumishi huyu hawawezi kuwa na imani na utumishi wao. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, hili alizingatie kwa sababu tunajua katika Zanzibar kila mmoja ana chama chake na tunajua kwamba viongozi hawa na watumishi hawa wanatoka katika chama fulani, lakini ile kuvaa sare maana yake wakatoa hisia tofauti kwa wale wananchi haipendezi. Naomba sana Mhe. Waziri, hili aliangalie.

Lakini jambo la pili ambalo nitalizungumzia kidogo Mhe. Spika, kwa sababu wajumbe wengi wameshalizungumzia ni kuhusu vitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, hapa kwa kweli pana mtihani mkubwa masheha hawatoi fomu ingawa tunaambiwa tumeshawaacha kwa sababu bado tutaendelea nao kwa sababu bado wananchi hawajapata haki zao.

Na hapa Barazani suala hili liliulizwa na eti Waziri alijibu hakuna mwananchi aliyemfuata Wizarani na akampa mashitaka, hebu tujiulize jana Mhe. Hamad, hapa alisema Micheweni kuna zaidi ya watu 300, Wete kuna watu kibao, Chake Chake vile vile na Mkoani, ivo kweli Mhe. Spika, inawezekana mwananchi aliyeko Micheweni na hali zetu za maisha tunazijua au aliyekuweko Vitongoji Kibokoni pale apande meli aje kwa Mhe. Waziri, kushtaki kama sheha hajampa fomu ya kupata kitambilisho, hivyo kweli wananchi hao nauli hiyo wataitoa wapi na wakifika watakaa wapi na watakuja wangapi. Mhe. Spika, kweli sheria ndivyo inavyosema, lakini je utekelezaji wake inawezekana au hichi kifungu kipo kwa ajili ya kusema kama sheria ndivyo isemavyo. Namuomba sana Mhe. Waziri, wakati anapotoa majibu atizame na hali za wananchi zilivyo.

Mhe. Spika, mimi namshauri sana Mhe. Waziri, mambo haya asiyachukulie kimtazamo wa kisiasa, alenge kutatua matatizo ya wananchi waliokuwa bado hawajapata haki zao na kwa hapa Mhe. Spika, nataka nimpongeze sana Dk. Mwinyihaji wakati alipokuwa Waziri wa Wizara hii alifika katika Wilaya zetu kwa ajili ya kutafuta namna ya kuondoa matatizo yale na kwa kiasi fulani ilisaidia kidogo, japo hayakuondoka kabisa lakini ilisaidia.

Mhe. Spika, lakini vile vile jana Wajumbe hapa walichangia kama kuna vitambulisho wanapewa wageni lakini Wazanzibari wazawa hawapewi, Mhe.

Spika, hili ni kweli na wale waliosema wanahitaji ushahidi mie miezi miwili nyuma iliyopita nilikuwepo *Islamic Bank*, walikuja ndugu zetu kutoka Bara wameajiriwa na walikuja pale kwa ajili ya kufungua *account*, nafikiri wametoka huko wameletwa kwa ajili ya ajira, walipofika pale wakaulizwa kitambulisho, wakasema sisi tumepewa barua hii tumeambiwa tufunguliwe *account* kwa sababu tokea kuja ni wiki moja lakini baada ya wiki moja tutapata vitambulisho. Hivyo kweli Mhe. Spika, sheria inasema kama wiki mbili mtu apewe vitambulisho wakati Mzanzibari aliyezaliwa hapa ananyimwa kitambulisho; mara anaambiwa cheti ni kifupi, mara tisa imekaa upande, mara baba yako hatumjui, kwa kweli hili ni tatizo.

Mfano mwengine ambao nataka niugusie Mhe. Spika, ni katika jambo ambalo limefanyika hivi karibuni ambalo limezua mjadala mkubwa na uendeshaji wake unaonyesha kazi zake Mhe. Spika, ni za kisiasa, ni ugawaji wa Shehia na Wadi zake, hivi nimuulize Mhe. Waziri, japo jana wengine walijibu, ni vigezo gani vilivyotumika na nini lengo lake? Mimi Mhe. Spika, maoni yangu nadhani hii ni sababu ya uchaguzi kuunganisha shehia na wadi na kuhamisha maeneo mengine ili kujihakikishia ushindi wa majimbo. Katika gazeti la Serikali niliona ugawaji ulivyofanyika na Shehia zilivyounganishwa, kwa kweli ni kama vile hawa wahusika waliofanya hivi hawajui jografia ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mfano Shehia ya Chonga iko Wilaya ya Chake Chake, Chambani iko Wilaya ya Mkoani, utachukuaje Shehia ya Dodo iliyoko Chonga uipeleke Chambani, lakini vile vile Mhe. Spika, kuna Shehia ya Limbani ipo Wete pale Mjini itarukaje ipelekwe Wadi ya Piki wakati hapa katikati pana Shehia ya Mzambarauni. Mhe. Spika, shehia nyengine ambayo pia nataka niitolee mfano ni Shehia ya Bopwe itarukaje ipelekwe Mgogoni na hapo katikati kuna Shehia ya Kizimbani, kwa kweli huu ugawaji ni mambo ya ajabu sana, huwezi kuichukua sheria iliyopo hapa ukainganisha na iliyopo kwa Mhe. Salma, ukasema ni wadi fulani wakati pana shehia katikati hapa, mimi nashangaa sana. Mifano ya aina hii ipo mingi Mhe. Waziri, kwa hili inaonekana Wizara yako ilikurupuka.

Mifano ya jambo hili Mhe. Spika, ilifanyika wakati wa ukoloni ambapo maeneo ya uchaguzi yalikuwa yakikatwa kwa mbinu ili kushindikiza ushindi wa majimbo ya chama fulani, lakini Mhe. Spika, wananchi hawakubabaishwa na njama hizo, ninalolishangaa hivi sasa mambo haya kufanyika wakati eti tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini, mimi kwa kweli suala hili limenishtua sana.

Mhe. Spika: Una dakika mbili.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, naomba kabla ya kumaliza nimwambie Waziri akiachia mambo haya yaende hivi, nchi inaweza kuingia kwenye vurugu na ni vyema ajue amani ikipotea ni vigumu kurejesheka.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kuvipongeza vikosi vyetu kwa kazi nzuri wanazofanya ingawa wengi walisema kama wanasiasa wanaviingiza vikosi katika siasa, Mhe. Spika, hili si jambo zuri hawa ni walinzi wetu, wanatusaidia kwa kila mambo, iwapo tutawashirikisha kwenye mambo ya siasa tutaleta ubaguzi, kunaweza kutokea jambo hawa wakashindwa kutusaidia wakasema huyu yuko upande fulani, hebu Mhe. Waziri, tuviachie vikosi vifanye kazi yake.

Lakini jambo jengine naomba Mhe. Spika, nizishukuru Halmashauri zetu na Mabaraza ya Mji kwa namna wanavyochangia na kukusanya mapato, na namuomba Mhe. Waziri, ajue katika watu wanaoshiriki kuchangia kupatikana kwa mapato hayo ni madiwani, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awaone madiwani wetu kimaslahi.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Hamza, kwa jinsi alivyomsaidia Mhe. Waziri, kijibu lakini kuna wengi walimlaumu, mimi simlaumu Mhe. Hamza, kwa sababu alisema Mhe. Waziri, ni mwalimu wake na kawaida mwalimu anaujua uwezo wa mwanafunzi na mwanafunzi vile vile anaujua uwezo wa mwalimu, kwa hivyo, Mhe. Hamza, sisi Barazani humu kujibiwa hoja zetu Mhe. Spika, ni wajibu ikiwa Waziri huyu unamshinda, ajibu Makamu wa Pili wa Rais yumo humu, atujibu, sasa ikiwa yeye kamkataza kujibu bila ya shaka kaona kama hoja za Mhe. Hamad Masoud, hazijibiki.

Mhe. Spika, nakushukuru *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, kwanza sina budi kumshukuru Mhe. Rais kwa ugawaji mzuri wa Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha wadi zetu zimekaa vizuri ili kuhakikisha wananchi wetu wamegawika na kuhakikisha kila wadi inauzito wa watu ambao wamewekwa katika wadi hizo.

Mhe. Spika, ugawaji wa Mkoa na Wilaya imehakikisha kwamba nchi yetu sehemu nyingi zilizokatwa zilikuwa hazina watu wa kutosha, ndio sababu ya kukaa serikali na kuona kwamba iko haja ya mikoa, wilaya pamoja na wadi zihakikishe kwamba zinakaa sambamba kufuatana na watu, ili kuweka sawa sehemu ambazo hazina watu. Hizo ndizo sababu zilizokatwa ili kuhakikisha kwamba mgao unaenda sambamba hata kinapopelekwa kitu kunawezekano vitu visizidi wala visipungue.

Ndio sababu kubwa hasa mgao wa wadi ikaonekana lazima ufanyike kwa wakati huu.

Mhe. Spika, nikiendelea nizungumzie kuhusu vikosi vyetu vya SMZ. Hivi sasa vikosi vyetu vinafanya kazi za doria na ulinzi pamoja na vikosi vya Muungano. Mchanganyiko wa vikosi katika sehemu zinazohitajika ulinzi na usalama kwamba vikosi vyote vinachanganyika katika ulinzi wa nchi yetu na wanaendelea vizuri. Iko haja Mhe. Spika, vikosi vyetu vinapounganishwa na vikosi vya Muungano. Mhe. Waziri, afatilie uwezo wa vikosi vyetu ili viwe vinalinda uzuri na mchanganyiko na doria na vikosi vya ulinzi vya Tanzania.

Kwa hivyo, Vikosi vya SMZ iko haja ya kuvipatia maslahi vikafanana na vikosi vya ulinzi vya Tanzania. Kwa sababu doria zao ni pamoja, ulinzi wao ni mmoja, silaha wanatumia namna moja. Ipo haja vikosi hivi kuhakikisha navyo vinahakikishiwa kwamba maslahi ya ulinzi vinapata nafasi kubwa ya kujihakikisha wanapokuwa ulinzi na vikosi vya Muungano wanabadilishana mawazo ya ulinzi pamoja na maslahi.

Wenzetu vikosi vya Muungano vinapozungumzia kuhusu maslahi vinazungumzia posho. Posho anayopata askari wa Muungano ndio mshahara wa askari wa Vikosi vya SMZ. Inarejesha nyuma vikosi vyetu na inarejesha nyuma ulinzi. Hivyo namshauri Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba anafatilia vikosi vyetu vinaishi vipi ili kuhakikisha kwamba vinapata maslahi ya ulinzi, kwani inahitajika askari aenziwe na atunzwe. Kwa hivyo, vikosi vidogo vidogo vya SMZ vinakuwa na masikitiko sana na kuweza kutuma viongozi kama sisi kuweza kuwasemea kila mara. Mhe. Spika, iko haja ichukuliwe hatua ya ukweli kwamba na wao wanapata maslahi ambayo yanaondoa malalamiko kwa viongozi wao hadi kwa viongozi sisi ambao tunaweza kuwazungumzia katika serikali hii.

Mhe. Spika, hapa mara nyingi tunamatatizo ya kujibizana kwa watu wa *back bencher* na Mawaziri. Lakini utaona wenzetu wanasiasa wa Chama cha Upinzani mara nyingi wanazungumzia siasa ya kusikitika, jambo hata halina uhakika au halina ushahidi. Mtu atakwambia hivi sasa vitambulisho vya Zanzibari sehemu nyingi havitolewi kisheria. Utakuta vipande vya Mzanzibari vinatoka kutokana na sheria. Mtu awepo katika ile shehia yake ndipo aweze kuomba kipande cha Mzanzibari. Ama amefika kwa sheha ahakikishe kwamba sheha ndiye anayemuombea barua kuhakikisha kupata kipande cha Mzanzibari. Lakini utakuta mwananchi yule yupo Chake Chake anaomba kipande cha Mzanzibari katika jimbo la Koani. Sasa utashindwa kumsaidia, asaidiwe vipi, ili apate haki yake.

Mimi naona arudi katika sehemu yake ndiko anapoweza kuomba Kipande kile cha Mzanzibari akaweza kupata haki yake ya msingi. Haiwezekani mtu yupo Wawi

lakini maslahi yake anayataka Unguja Ukuu, hiyo haiwezekani. Maslahi ya Unguja Ukuu ni ya Unguja Ukuu hasa kwa waliopewa kibali cha Mzanzibari. Maslahi ya Wawi ni ya Wawi kwa kipande cha Mzanzibari. Hivyo, nawaomba wanasiasa wenzetu wahakikishe wanapozungumzia kitu kiwe na ushahidi na uhakika, si hivyo itakuwa wanaizonga sana serikali na kulaumu Mawaziri kwamba wanawafanyia sio haki.

Mtu anazungumzia kuhusu Waziri, Waziri ndiye aliyepewa sehemu ile kuiongoza na ujuzi wa kuongoza anao yeye Waziri. Sio *back bencher* anazungumzia kuhusu suala la Waziri kwamba Wazari afanye hivi, afanye hivi. Basi sisi *back bencher* ina haja ya kwamba sote tuwe Mawaziri kwa wakati mmoja, lakini kwa hivi sasa iko haja kwamba tuwaachie Mawaziri ndio waliopewa haki ya kuweza kujibu masuala ambayo wanaulizwa na sisi *back bencher.*

Kutokana na mengine yote na kutokana na hali ya muda mimi naunga mkono ya wenzangu waliyoyajibu maswala haya. Kwa hayo sina zaidi isipokuwa kama ulivyotupa sheria nzuri leo ya kusema kuunga mkono sheria waliyozungumza wenzetu na mimi kutokana na mengi yamebakia naunga mkono yote yaliyochangiwa na wanachama wenzetu pamoja na wanasiasa walivyojibizana mimi naunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti yetu hii ambayo ipo mbele yetu.

Mhe. Spika, nikishakumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, mimi nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake katika wizara. Lakini pongezi kubwa zaidi na za kipekee nazipeleka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwongozi wake makini juu ya namna ambavyo wizara zake hizi anavyozisimamia na kutekeleza yale ambayo yamekwisha kuagizwa kama ambavyo Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi imekuwa ikielekeza.

Mhe. Spika, mimi nianze na *Hansard* ya mwaka 2014, terehe 3 Juni. Katika *Hansard* hii Mhe. Spika, humu kuna mambo mawili makubwa yalikuwa yamezungumzwa; moja ni suala zima la usafi katika Manispaliti ya Mji wa Zanzibar. Katika *Hansard* hii na mchango wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walizungumzia sana juu ya suala zima la usafi.

Mhe. Spika, kwa kweli Baraza la Mji linajitahidi na wanajitahidi sana katika suala zima la kuhakikisha kwamba Mji wa Zanzibar unakuwa safi na salama. Lakini

kuna ambayo wenzetu wa Baraza la Mji wanahitaji msaada kutoka kwetu kama wananchi na wakaazi wa maeneo haya tunayoishi kwa pamoja.

Mhe. Spika, njia za kupitia maji nina maana ya mitaro, mingi sana ina matatizo kama ambavyo tumekwisha kushuhudia hapa kwa michango mbali mbali ambayo Wajumbe wanakuwa wanatoa. Lakini inapotokezea wakati ule wa mvua, mitaro hii tunapambana na kadhia ya taka nyingi ambazo sisi wenyewe wananchi huwa tunazitupa katika mitaro ile.

Ningeliomba sana pamoja na kuipa jukumu serikali katika suala zima la usafi, lakini na sisi kama wananchi tuna nafasi ya kutimiza wajibu wetu kuhakikisha kwamba na sisi tunaenzi usafi na zile njia ya kupitiwa maji zinaenziwa ili mvua inapokuja kutokezea isije ikawa inaendelea kuleta maafa kama ambavyo tunashuhudia kila mvua zinapokuwa zinanyesha katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, mvua ambayo inamalizikia sasa hivi, katika maeneo mbali mbali, imeleta maafa ya namna kwa namna. Lakini pia imeweza kusababisha maradhi haya ya maleria kuweza kurudi na safari hii yamekuja kwa kasi kubwa. Sasa hii mbali ya mvua inasababishwa vile vile na uchafu ambao umo katika maeneo ambayo inakuwa maji yale yanataka kupiga. Ningeliomba kuchukua fursa hii kuwaomba wananchi wenzangu tuwe na utaratibu wa kutunza usafi ili mvua zinaponyesha tuweze kuweza kunusurika na majanga na matatizo ambayo yanakuwa yanajitokeza.

Mhe. Spika, nilipochangia Bajeti Kuu na huko nyuma nilizungumzia suala zima la mradi wa *ZUSP*. Lakini Mhe. Spika, nitamke tu kwamba nimefarijika na hatua za serikali zinazochukuliwa juu ya suala zima la mradi wa *SUSP* na kwa sasa hivi hapa nampongeza sana Waziri ambaye anasimamia Wizara hii kwa kazi nzuri na kwa ziara ambayo nimeishuhudia mimi mwenywe, ndani ya jimbo la Kikwajuni ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi katika kutembelea maeneo na vile vile kufahamu mkakati na matayarisho ambayo serikali imetayarisha juu ya suala zima la haya maeneo ambayo yanapambana na matatizo ambayo siku zote ilikuwa tunayatolea maelezo hapa. Hilo nimefarijika nalo na nawaomba basi wasichukue muda mrefu ili suala hili wazidi kulishughulikia kwa karibu zaidi na mambo haya yaweze kupatikana na salama iweze kuonekanwa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa, nakuja katika kijitabu chetu hichi cha Muhtasari wa hotuba ya Waziri, katika ukurasa wa 13, ningeliomba tu Mhe. Waziri atuwekee sawa pale katika *Hansard* ili isije ikaleta utata. Kwa sababu kwenye maandishi katika kifungu cha 44 katika ugawaji wa asilimia kuna elfu moja na nane. Nafikiria alikuwa amekusudia kuandika mia moja na nane. Kwa hiyo,

naomba ili *Hansard* ikae sawa hapa aparekebishe na tuweze kupata mustakbali ambao tulikuwa tunautegemea.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika kifungu cha 40 katika ukurasa huo huo wa 13. Hapa paliongelewa suala zima la vitambulisho kwa upande wa Zanzibar kwa ujumla wake. Mhe. Spika, hii nchi inaendeshwa katika utaratibu na nchi hii inaendeshwa kwa sheria. Hapa Mhe. Spika, nina *Hansard* tokea mwaka 2005, nimejaribu kuzipitia mpaka nikawa nimemaliza. Wenzetu hawa ilikuwa mwanzo kuna kelele nyingi sana zinazozungumziwa juu ya suala zima la vyeti vya kuzaliwa kwa upande wa Zanzibar kabla ya kwenda kwenye *Zan-ID*. Baada ya mabadiliko haya na mipango mizuri ambayo imepangwa na Wizara hizi zikagaiwa katika utekelezaji na utendaji ambao unaendelea, suala zima la vyeti vya kuzaliwa sasa hivi halizungumzwi. Mimi sababu sijui, isipokuwa kwa sasa panazungumziwa suala la kipande cha Mzanzibari Mkaazi.

Jamani sheria zipo na watu wanakwenda kwa mujibu wa taratibu, mbona sisi wengine hatuji hapa tukawa tunazumza suala hili la vitambulisho. Mimi Mhe. Spika, katika jimbo langu nina watu zaidi ya 300 hawajapata hivi vitambulisho. Wanapokuja katika maeneo yetu tunawafahamisha utaratibu wa kuweza kwenda kupata vipande vile. Mpaka Jumamosi kuna wengine wanakwambia kwamba vyetu vimepotea, basi wanakuja wanatafuta na angalau wapewe shilingi elfu tano waweze kwenda kulipia kule ili walipe vyengine. Nawambia hapana, hicho kitambulisho ni chako mwenyewe, mimi kama una matatizo mengine nitakusaidia lakini kama masuala kama haya, nenda kafuatilie utaratibu wako mwenyewe.

Lakini nashangaa kuona sasa hapa wenzetu imekuwa wao ndiyo wamevaa njuga kwa ajili ya suala la vitambulisho, jamani vitambulisho vina utaratibu wake, watu waende kwenye utaratibu, wafuate taratibu zinahusu, waende wakavichukuwe vitambuisho, vitambulisho vipo bwana Mhe. Spika, vinavyopaswa kuwepo. Juzi hapa katika hoja binafsi ilivyoletwa vililetwa vitambulisho zaidi ya elfu tano hapa, vikamwagwa hapo mbele, sote tulivishuhudia. Sasa leo imekuwaje tunakuja kupata maelekezo kama haya. Tuzungumzeni kitu ambacho kina mashiko, tusizungumze kitu ambacho kina miujiza.

Kwa kujali wakati wako Mhe. Spika, sasa niende katika zoezi hili la ukataji wa wadi pamoja na shehia na mazoezi ambayo yanaendelea katika maeneo fulani fulani. Mhe. Spika, hapa jana palikuja kuzungumziwa hoja juu ya suala la watu wanaochukuliwa kwa makarandinga wakapelekwa jeshini. Mimi nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie, je, katika maeneo ya majeshi kuna vituo vya Tume ya Uchaguzi. Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie.

Lakini kwa upande mwengine mimi napenda kumuachia kazi Bregedia Kamanda kule mambo hayo, ndiyo yamezungumzwa anatakiwa ayathibitishe kwa sababu sekta yake ile. Sasa hii itakuwa ni kazi yake yeye mwenyewe. Lakini nikiachia hapo Mhe. Spika, hapa wamezungumza watu kwa jazba kubwa sana juu ya suala zima la watu kuwa wanaandikishwa kinyume cha taratibu.

Mhe. Spika, katika kazi ambayo imeanza jana katika maeneo ya Micheweni Pemba kuna taarifa za uhakika kabisa waliokwenda kujiandikisha kule baadhi yao ni wananchi ambao wametoka Tanga na wengine wametoka Mombasa. Sasa, je, haya yote mnakuwa hamuyaoni au mnaona yale ambayo kuwa hayana uhakika ambayo yametokea Zanzibar tu. (*Makofi*)

Baada ya maelekezo hayo kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nashukuru Mhe. Mahmoud, kwa mchango huo na kuokoa muda, sasa wakati muwafaka umefika, nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Inafaa awe na msaidizi wa kumsaidia nondo zile zikianguka aokote na kumuwekea sawa. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika kuchangia bajeti yangu, bajeti ya wananchi wa Zanzibar kuhusu makadirio na mapato ya kuendeshea wizara yangu na maendeleo mengine ya wananchi katika kipindi cha mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, Wajumbe ambao wamechangia hotuba hii ni Wajumbe 26. Wajumbe 21 wamechangia kwa kusema wenyewe na Wajumbe watano wamechangia kwa maandishi. Niwashukuru sana wale Wajumbe wote ambao wamechangia hotuba hii na niwashukuru pia wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia lakini walikuwa na hamu ya kuchangia.

Naomba niwatambue Wajumbe ambao wamechangia kwa pamoja, kwa sababu nitakapokwenda kutoa ufafanuzi sitamtaja Mjumbe na hoja yake mimi nitatoa ufafanuzi juu ya mchango ambao umetolewa.

Wa kwanza Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ambaye ametoa mchango kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Spika, tumekuwa tunasisitiza sana habari ya kanuni lakini uzoefu unaonesha kwamba Mhe. Spika, kwa mfano Spika kama ungekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Naibu Spika, anataka

kukuwakilisha kwenye kiti, maana yake wewe ungetakiwa utoke ndani ya Baraza kwa mujibu wa uzoefu ambao nimeupata katika kipindi cha nyuma wakatu tuna Naibu Spika, Mhe. Kamal na Mhe. Ali Mzee Ali akiwa Mwenyekiti. Sasa huu utaratibu nitaomba Mhe. Spika, tuuangalie.

Tuna utaratibu wa kuchagua Wenyeviti wa Kamati, si kawaida kwa Mwenyekiti wa Kamati kuwa yupo akawa anawakilishwa labda awe na dharura ya ugonjwa. Lakini kama hayupo Mwenyekiti anachaguliwa Makamu Mwenyekiti lakini Makamu Mwenyekiti anawakilishwa na Mjumbe akiwa humu ndani.

Sasa napendekeza kipindi kijacho watakaobahatika basi tuangalie upya utaratibu huu maana si utaratibu wa kawaida katika Mabunge mengi, ilivyo ukiwakilishwa maana yake hupo, ukiwa upo huwezi kukaimiwa huo ndio utaratibu wa kidunia ulivyo.

1. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Hamza Hassan Juma
6. Mhe. Hassan Hamad Omar
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad
9. Mhe. Farida Amour Mohammed
10. Mhe. Hussein Ibarahim Makungu
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid
13. Mhe. Abdi Mossi Kombo
14. Mhe. Salim Abdalla Hamad
15. Mhe. Panya Ali Abdalla
16. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
17. Mhe. Subeit Khamis Faki
18. Mhe. Nassor Salim Ali
19. Mhe. Fatma Mbarouk Said
20. Mhe. Salma Mohammed Ali
21. Mhe. Mussa Ali Hassan
22. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, hao walichangia kwa kusema.

Waliochangia kwa maandishi ni :

1. Mhe. Nassor Salim Ali
2. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

3. Mhe. Mgeni Hassan Juma
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, na
5. Mhe. Salma Bilali.

Nataka niwashukuru wote kwa michango ambayo wamechangia kwenye hotuba yangu hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Spika, nataka niwashukuru wote waliochangia kwa kutumia demokrasia yao, kutoa maoni kama walivyoeleza wenyewe yale ambayo wamepewa na wananchi katika kuja kuwawakilisha hapa.

Kwa hivyo, michango yao yote nimeipokea na naomba nitoe ufafanuzi kwa michango ambayo imetolewa, na nitajaribu sana kutoa ufafanuzi wa jumla hasa kwa zile hoja ambazo zimezungumzwa na wachangiaji wengi.

Hoja ambazo zimezungumzwa na wachangiaji wengi ni hoja kama tatu. Hoja ya Ofisi ya Usajili na kadi ya vitambulisho, hoja ya ugawaji wa mipaka na hoja ya ushushwaji wa bendera kule Micheweni ya chama kimoja cha siasa. Sasa nitaomba hiyo niitoe kwa ujumla, kwa sababu wachangiaji walikuwa wanazungumzia hilo na limechangiwa na watu wengi. Zile hoja ambazo zimechangiwa na mchangiaji mmoja mmoja nitajaribu sana nazo kuzieleza ili wajumbe waweze kujua nini hasa Serikali inafanya.

Lakini hoja ambayo nataka niitangulize ile iliyochangiwa na Mhe. Salma Mohammed Ali. Kwa kweli siifahamu kipimo chake kwangu cha kusema kwamba mimi sina uwezo wa kujibu hoja za Mhe. Hamad Masoud. Licha ya hoja ambazo wamezitoa hapa niliweza kujibu hoja yake binafsi aliyoiwasilisha kikao cha mwisho cha Baraza na sio Mhe. Hamad Masoud tu, nina uwezo wa kujibu hoja ya mtu yeyote, uwezo huo ninao si kwa ubabe lakini kwa maarifa ambayo Mwenyezi Mungu amenijaalia. Wala kusimama *back bencher* akatoa ufafanuzi hainifanyi mimi nishindwe kutoa ufafanuzi, kwa sababu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ameniteua mimi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum. *(Makofi)*

Kwa hivyo, najua wajibu wangu Mhe. Salma, kweli kweli, tena ninajua wajibu wangu huu nilionao humu ndani na ninajua wajibu wangu mwengine kabisa. Kwa hivyo usiwe na wasiwasi kwamba nitashindwa kujibu hoja zenu, nitajibu na nitatoa ufafanuzi. Si kujibu tu lakini nitachukua nafasi hii kutoa ufafanuzi, kwa hivyo usiwe na wasiwasi kaa mkao wa kula usikilize ninakujibu nini kuhusu hoja zako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyingi zimejitokeza nianze na hoja Mhe. Salma ambazo amezisema nyengine kama nilivyosema nitazitoa kwa ujumla wake. *No*, nianze na

Mhe. Mahmoud na mkiniona naanzia nyuma kwenda mbele ni kwa sababu tu zile nyengine watendaji nilishakaa nao na kuziratibu lakini hizi sikupata nafasi ya kukaa na watendaji wangu, kwa hivyo, nitajaribu kuzitolea ufafanuzi ili nisije nikazisahau.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, ninamshukuru sana kwa maelezo ambayo ameyatoa yanayohusu kutoa taaluma kwa wananchi wa Zanzibar hasa mji wa Zanzibar kuimarisha suala zima la usafi. Usafi wa mji wetu na kutuasa kwamba tuwe na utamaduni wa kufuata taratibu hasa mvua inaponyesha wa kutokutupa taka katika mitaro yetu na hatimaye mitaro ndipo inaziba inatuletea maafa na inasababisha mambo mengine. Lakini pia utamaduni wa usafi wa kutunza mji wetu na tuache ile tabia ya kusifia miji ya wenzetu wakati sisi wenyewe tunashindwa kufuata taratibu za kuweza kuutunza huo mji. Kwa hivyo, ninamshukuru sana Mhe. Mahmoud, kwa maelezo yake na Waheshimiwa wengine nadhani Mhe. Hamza alizungumzia sana suala la mradi wa *ZUSP* na Mhe. Farida, alizungumzia sana masuala hayo.

Nataka niwahakikishie kwamba maeneo yote yaliyomo katika mradi huu wa *ZUSP* sasa yameshakamilika, yale yanayohusu ujenzi wakandarasi wako *site* na wanafanya kazi, ukiacha huu mradi mmoja wa michirizi mjini Unguja lakini miradi yote iko tayari. *Sea wall* tayari, yaani ule ukuta wa bandarini pale baharini uko tayari, mkandarasi yuko tayari na harakati mmeanza kuziona.

Mradi wa taa za njiani ambao utahusisha baadhi ya maeneo ya Mji Mkongwe na barabara itakayotoka Muembeladu kuzunguka Mikunguni mpaka Mwanakwerekwe kurudi Kariakoo na huo Mkandarasi ameshapewa hiyo kazi karibuni utaanza kazi. Miradi mengine iliyopo katika kisiwa chetu cha pili cha Pemba, naye Mkandarasi yuko *site* na Mhe. Farida, alizungumzia sana suala lile. Nataka nitambue shukurani zako kwangu na watendaji kwa kelele ambazo ulizipiga kwa mtu aliyetaka kufanya ujanja kulivamia eneo la Baraza la Mji Wete, na Serikali ikafanya juhudi ikaweza kuurejesha umiliki ule kwa Baraza la Mji la Wete.

Sasa mradi uliopo pale katika Baraza la Mji la Wete, soko ni eneo moja lakini kuna soko, kuna *parking* kuna na ukarabati wa Ofisi ya Baraza la Mji Wete. Kwa hivyo kama ulivyosema yale mengine ambayo uliyoyasema yale Mhe. Farida naomba tukubaliane tu kwamba ni kweli kama madiwani walivyoniletea barua ya kutaka kujua wanajengewa soko kwa maana ya soko la ghorofa mbili au tatu au namna gani. Kwa hivyo mawazo ya madiwani wa Baraza la Mji wa Wete wakati ule, sio hili Baraza la Mji, linalomaliza muda wake kipindi hiki, lile lililopita walipendekeza hilo. Lakini yale yalikuwa ni maombi kwa *World Bank*, kwamba Madiwani na wananchi wa Baraza la Mji la Wete walitaka kujenga soko la

ghorofa, lakini tulipopeleka ule mradi kwa wafadhili kuna mambo mbali mbali waliyaona kwamba kufanya vile haiwezekani.

Kwanza kutokana na kiwango kile, *amount* ya pesa ambayo alikuwa ameitenga kwa ajili ya soko lakini vile vile wao walikuwa na mawazo mbadala kwamba pale kwa sababu ni soko la zamani kwa hivyo lile soko lifanyiwe ukarabati liimarishwe vizuri zaidi, huko mbele tunakokwenda tutafute eneo jengine la kuweza kujenga soko jengine kwa mahitaji ya wakati huo. Lakini kwa sasa kwa mujibu wa eneo lile isingewezekana kuweza kujenga soko lile pale.

Kwa hivyo, huu mradi wa ujenzi wa soko na miradi mengine kwa Baraza la Mji la Wete inaendelea vizuri. Kilichobakia sasa hivi ni huu mradi wa michirizi ya mji wa Zanzibar ambayo nayo iko katika hatua nzuri ya kuweza kupata *no objection* kutoka *World Bank,* walituahidi kwamba ingekuwa kabla ya tarehe 15 mwezi huu wa sita tungeweza kupata *no objection,* ili mradi wa michirizi nao ukamilike. Kwa hivyo suala hili la Mhe. Mahmoud na Mhe. Hamza, kwa michirizi ya Mjini Unguja nayo hivi karibuni atapatikana mkandarasi itapatikana *no objection* nayo itaanza kazi.

Lakini kwa upande Wete Mhe. Farida nadhani ile miradi ni mitatu iko katika *component* tatu kwa pamoja, ukiacha ile ya kuleta magari, lakini ya ujenzi inahusisha suala la *stand* ya pale, linahusisha suala la soko inahusisha na Ofisi ya wapi. Kwa hivyo Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa mradi wa michirizi mjini pamoja na Mhe. Hamza mradi huu si muda mrefu nao utaanza kazi.

Mhe. Salma Mohammed Ali, nadhani hoja moja nishaitolea ufafanuzi sina haja ya kuirejea.

Mhe. Mussa, nimepokea maoni yako nadhani wewe zaidi ulikuwa ukipongeza na ukisema kwa nini tumefanya hii kazi. Tumefanya kazi kwa sababu ndio tuliopewa majukumu ya kutekeleza hili jambo na yale mengine nadhani mimi sipaswi kuyajibu kwa sababu ulikuwa unatoa elimu ijapokuwa hukutoa barua ya Semina. Na hata jana Mhe. Salim Abdalla Hamad alitoa semina sana hapa ya Katiba ijapokuwa hakutuarifu Wajumbe kwamba anatupa semina.

Alikuwa akizungumza akitupa semina lakini hakutupa barua maskini, kama ile barua tuliyopata jana ya kushiriki kwenye semina ya barabara siku ya Jumamosi. Maana yake kawaida ukitaka kutoa semina lazima utoe barua kwa Wajumbe wenzio wajue ili wajitayarishe kuja kuichangia hiyo semina.

Kwa hivyo wale waliotoa semina basi wajumbe watakuwa wameisikia japokuwa si rasmi, kwa sababu hawakutoa barua naweza nikaishia kusema hivyo.

Mhe. Salma anasema mwananchi kutoka Micheweni atampataje waziri. Katika waziri ambaye rahisi kuweza kupatikana ni mimi. Mtandao wangu wa kiutawala unamuwezesha mwananchi yeyote kufikisha taarifa na akazipata waziri. Ni waziri pekee ambaye nina mtandao mkubwa kutoka kwenye shehia, *local authority,* Halmashauri, Wilaya, Serikali Kuu, Mkoa lakini na Ofisi Kuu Pemba.

Kwa hivyo, mwananchi aliyeko Kisiwani Tumbatu ana uwezo kwenda kwa Sheha, kwenda Wilaya ndogo, kwenda Halmashauri kama taarifa zinanihusu mimi, yeye atayarishe tu taarifa zake azifunge ziandikwe tu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa basi zitakuja tu ofisini kwangu na nitazifanyia kazi. Kwa hivyo, tusiwe na mashakam, mwananchi aliyeko huko atanipataje, nina mtandao mkubwa wa kufanyia kazi. Kwa hivyo kwa hili Mhe. Salma asiwe na wasiwasi sana juu ya mimi namna ninavyoweza kufanya kazi zangu.

Nimezungumza suala la *Islamic Bank* ndio maana nasema dhana hizi saa nyengine sio nzuri, *Islamic Bank* unapofungua *account* sio tu unatakiwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, unaweza ukawa unatakiwa kitambulisho cha Mtanzania, unaweza ukawa unatakiwa kitambulisho, *passport,* unaweza ukawa unatakiwa utoe *license;* vitambulisho ni vingi. Sasa si dhana sahihi kwamba kila anayetaka kwenda benki kutaka kufungua *account* kwamba atatakiwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi si sahihi sana, lakini kama unacho kinaweza kikawa kati ya kielelezo ambacho kitahitajika katika kufungua *account* au katika kufanya mambo mengine ya kijamii na ya kiuchumi, lakini sio sahihi sana na ndivyo duniani wanavyofanya. Bahati sio nzuri sana nchi yetu haijaendelea kiasi hicho, lakini pengine haya mashaka haya yataondoka pale tutapoweza kuunganisha *registry* zote kuwa katika eneo moja.

Wajumbe mshawahi kusema, nchi zilizoendelea kuanzia siku unayozaliwa cheti cha kwenye *birth certificate* namba yake ndio hiyo hiyo itafuata vitambulisho vyako vyote. Sasa na sisi *inshaallah* Mungu akipenda tutafika huko.

Mhe. Omar Yussuf Mzee waziri aliyepewa dhamana ya fedha ameanza kuonesha muelekeo na Rais wetu ameanza kusimamia, Dkt. Ali Mohamed Shein kunyanyua mapato ya nchi ili tufikie huko lakini pia tukiweza kuchimba mafuta yetu na gesi tutafikia huko kuweza kuondosha mashaka haya ya nani anasimamia nini, nani anasimamia nini. Tunakuwa na *registry* moja kuunganisha zile *registry* tutaondokana na haya matatizo ya kudhaniana dhaniana.

Nawaomba Wajumbe muwe na subra huko tutafika, na sisi kwenye *manifesto* yetu ya ilani ya uchaguzi tutaweka hilo angalizo, sifichi, tuwe na *registry* moja tuondokane na haya matatizo ya kudhaniana dhaniana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said yeye zaidi amezungumzia tafsiri ya dhana nadhani sina haja ya kurejea waheshimiwa wamesikia. Majeshi wanafanya kazi zao. Na mimi nataka niseme tuhuma hizi ambazo tumelipa Jeshi la Wananchi wa Tanzania si tuhuma nzuri sana. Ningeomba wajumbe wanapotoa tuhuma kama hizi ni utaratibu tu wa kidemokrasia kwamba Mjumbe anapoamua kuchangia hapa na kwa busara ya Mhe. Spika unaachiwa uchangie. Lakini tunakuja kwenye mizozo yetu sisi tunataka kuhamisha mzozo kuupeleka jeshini, nadhani sio sahihi sana. Tuwaache wanajeshi wafanye kazi zao, na kama kweli kuna tatizo hilo nilimshuhudia Waziri wa Ulinzi alipewa suala hili kule Bungeni na akaomba apelekewe ushahidi ili achukue hatua.

Mhe. Spika, nasikitika kusema hakupelekewa mpaka leo, ukitaka unipe mimi kwa upande mmoja wa shilingi nitashindwa, kwa sababu mamlaka yangu haiko jeshini. Na utaratibu wa wenzetu hawa kama wanajeshi msidhani tu mtu unaweza ukamwambia waziri njoo nataka twende tukashuhudie, huwezi kuingia jeshini tu. *Brigadier General* aliyepo Migombani hapo hana mamlaka ya kuingia kwenye kambi bila ya taarifa maalum ya *CDF*. Huo ndio utaratibu wa kuendesha taasisi hizi za kijeshi, sio kwa sababu mimi waziri nina uhusiano pengine na vikosi hivi vya SMT halafu unichukue tu Mjumbe unipeleke jeshini, mimi nitakataa, kwa sababu nitakuwa najua Kanuni za Kijeshi.

Nasema *Brigadier General* wa Nyuki anapotaka kwenda kwenye kambi ya Bavuai pale, si jirani yao, lazima atoe taarifa kwa *CDF*, *CDF* amuarifu mkuu wa kikosi wewe ndio uweze kuingia jeshini, huo ndio utaratibu.

Kwa hiyo, ningeomba sana mambo haya tunavyoyazungumza sisi kama wanasiasa na mimi nakubali wengi mmesema askari tusiwahusishe na siasa, sasa huku ni kuwahusisha na siasa, hii michango yenu mnawahusisha na siasa. Kwa hiyo, ningeomba sana tusifanye hivyo, tuwaache wanajeshi wafanye kazi zao, nisingependa kuendelea zaidi. (*Makofi*)

Mhe. Subeit Khamis Faki nakubali pongezi ambazo umetupa umezungumzia suala la ujenzi wa jengo la Micheweni.

Kwanza na mimi kwa niaba ya Madiwani na wananchi wa Micheweni, kwa sababu jengo lile limechangiwa na wana Micheweni wenyewe, kwa maana ya Wilaya na watu wakikusanya wakitoa kodi, ile kodi inatakiwa irudi kwa wananchi wenyewe, ndio maana ya lile jengo kujengwa pale. Sasa umenitaka nikupe hesabu kwa haraka haraka hiyo sina hapa, na kwa sababu umesema sasa hivi tungepaswa kufuata vitabu vyetu, lakini naahidi nitakuletea kwa maandishi sio zaidi ya Jumamosi hii.

Mhe. Spika, lakini jengine ambalo umelizungumza kuhusu kituo au kambi ile inayojengwa ya *KVZ*, na kusema pengine watu hawajapewa fidia. Sisi kama wapiganaji wa SMZ na vikosi vyetu ndio maana kwenye hotuba yangu umeona kikosi kimoja cha KMKM kimelipa fidia kwenye eneo kuongeza eneo lao, hatuingii kwa mabavu, pamoja na kwamba kazi zetu zinaweza *sometimes* zikaturuhusu kufanya hivyo, lakini hatumdhulumu mtu.

Kwa hiyo, na kikosi cha KVZ kilivyokwenda Micheweni kimelipa fidia ya watu waliokuwa na mazao pale na orodha yao ninayo, ukitaka nitakukabidhi baadae ili ikusaidie katika *reference*, na siku ile ya mwanzo nilikupongeza kwa hii itakuwa ni sehemu moja ya kwenda kupiga debe huko ili uweze kuchaguliwa na wananchi.

Kwa hiyo, nitakupa orodha hii sisi tumelipa fidia na hesabu yetu tunayo, tumelipa fidia ya milioni moja, elfu kumi na sita mia tano na hamsini kwa yale mazao ambayo yalikuwepo katika eneo lile. Kwa hiyo, hakuna mwananchi ambaye tumemdhulumu.

Suala jengine ambalo umelisema nakuomba radhi sana rafiki yangu Mhe. Subeit kuhusu soko la Qatar. Sijui kama umepita kipindi hiki lakini haliko hivyo ulivyosema, kwamba ni chafu sana, hapana, haliko hivyo. Ni kwamba tumejitahidi tumetengeneza *parking* pale, tumetia kifusi na katika bajeti hii tunao mpango Mhe. Gavu asubuhi alipokuwa akijibu maswali yanayohusu barabara za ndani. Tunao mpango kupitia fedha za mfuko wa barabara kuijenga barabara ile, fedha hizo zitapita kwenye Baraza la Mji la Chake-Chake. Na kama nilivyotoa taarifa katika kipindi kilichopita Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma imeshatupa kibali cha kuajiri ma-*engineer* watatu kwa ajili ya kusimamia kazi hizo Unguja na Pemba.

Kwa hiyo, hata kile kilio cha kulalamikiwa kwamba hatujengi barabara za ndani ni kwa sababu tulikuwa hatuna utaalamu, sasa tunaajiri na kibali tumeshapewa na watu wameshafanya *interview* na karibu wanamaliza taratibu zao, tukiwapata hawa barabara ile itajengwa.

Na kuhusu soko lile la *Qatar* ni kwamba kupitia Mradi wa *MIVARF*. Mhe. Subeit na wale wote walioulizia kuhusu soko lile, kupitia Mradi wa *MIVARF* wanamaliza kazi za barabara awamu ya kwanza ni ujenzi wa kazi za barabara za vijijini. Wakimaliza kazi hizo sasa wanakuja katika awamu ya pili ya ujenzi wa masoko. Kwa hiyo, pale *Qatar* tutajenga soko la kisasa litakaloondosha tatizo na litakalokidhi haja hiyo ambayo umeisema Mheshimiwa.

Kuhusu hoja nyengine nitajibu kwa jumla ile ya upunguzaji wa wadi na mambo mengine nitaijibu baadae kwa ujumla.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na yeye ametupongeza kwa kazi ambazo tumezifanya. Nataka nikubali kupokea pongezi zake na watendaji wangu bahati nzuri wapo, tena wapo kwa wingi, hakuna mtendaji ambaye hayupo pale. Kwa hiyo, pongezi hizo nazipokea pamoja na wenzangu wale walioko pale.

Eneo la Magereza linalowekwa wanawake ni dogo. Hili nataka niliunganishe na wale Waheshimiwa waliopendekeza suala la mahabusu ya watoto, hili jambo nimeshakuwa nalitolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, Magereza yetu ni ya zamani na makongwe. Kwa maumbile ya Magereza yetu lazima sehemu ya wanawake na sehemu ya mahabusu ya watoto yatakuwa yanakaribiana, lakini hivi sasa tatizo la kuwachanganya pamoja watu wazima na watoto halipo. Isipokuwa ni kweli wanakaribiana na tunapofanya ziara katika Magereza tukiwaita mahabusu na watoto lazima tutawakusanya pahala pamoja, lakini pale tunapowakusanya kwa muda ule pale wanakuwa salama, kwa sababu hakuna jambo jengine lolote ovu linaloweza kutokea. Lakini tunakubali kwamba maeneo yetu ni finyu, na hili tutalitatua tu pale tutakapobadilisha muundo au maumbile ya majengo yetu ya vyuo vya mafunzo kuyajenga kisasa badala ya hivi yalivyo.

Kwa hiyo, changamoto hii tutaendelea kuwa nayo, lakini tutajitahidi kadri tutakavyokuwa tunajenga majengo mapya basi tutakuwa tunabadilisha mfumo na muundo wa haya Magereza, na hasa kutenganisha Magereza ya kinamama na watoto wadogo pamoja na yale yanayotuhusu sisi kinababa. Kwa hiyo, Mhe. Mwanaidi pongezi tunazipokea na watendaji wamezisikia.

Mhe. Panya Ali Abdalla mchango wako ninaupokea na tunapokea pongezi, lakini Mhe. Panya aligusia suala la maslahi ya wafanyakazi, lakini pia maslahi ya wapiganaji na hili limezungumzwa na watu wengi hata Mhe. Saleh *uncle* wangu amelizungumza sana hili.

Na mimi nikwambie askari wanakupenda sana wala hawakuchukii, wanakupenda na wenyewe wale pale. Jana uliposema kwamba wanakuchukia walipatwa kidogo na butwaa namna vile wanavyokupenda.

Kwa hiyo, hawakuchukui wanakupenda, na wanakupenda kwa sababu wanakusikia unatetea maslahi yao. Kwa hiyo, usijenge dhana kwamba askari wanakuchukia.

Najua katika jimbo lako unazo kambi za wapiganaji wetu wa SMZ, unazo kambi za wapiganaji wetu wa SMT, na unaona mambo mazuri ya maslahi ya wananchi wa Jimbo la Wawi yanayofanywa na vikosi hivi vya SMT na SMZ. Kwa hiyo, Mhe. Saleh usiwe na wasi wasi, askari hawa wanakupenda sana wala

hawakuchukii, na wanatupenda sote Waheshimiwa Wawakilishi tumekuwa tukitetea maslahi yao, tumekuwa tukipigania vitendea kazi vyao na hili limezungumzwa na wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi, lakini ukweli usiofichika serikali kadri ya hali na uwezo uliporuhusu tumejaribu kuboresha maslahi ya askari wetu na tutaendelea kuyaimarisha, samahani neno "kuboresha" sio neno zuri lakini kuimarisha maslahi ya askari wetu.

Na katika kuwajengea uwezo wa maslahi yao nataka kupitia Baraza hili Tukufu kuwaarifu kwamba ile faida wanayoipata askari wa SMT kimaisha kupata vyakula na vifaa vya ujenzi na mambo mengine kwa bei nafuu, utaratibu huo si muda mrefu utaanza kwa askari wetu wa SMZ ili kuwapunguzia makali ya maisha.

Nataka niwaarifu taarifa njema kwamba tayari serikali imeamua kwamba nao wafaidike na utaratibu huu wa maduka nafuu askari wetu kama wanavyofaidika askari wa SMT. Kwa hiyo, si muda mrefu pengine ndani ya mwezi huu shughuli hizo za maduka nafuu zitaanza, zote hizo ni juhudi za serikali katika kuwapunguzia ukali wa maisha askari wetu wa SMZ.

Mhe. Panya mengi yalikuwa ni ushauri na pongezi tunazipokea, Mhe. Abdi Mossi Kombo naye halikadhalika.

Mhe. Farida Amour Mohammed ufafanuzi mwengine nimeshautoa lakini ulizungumza suala muhimu sana la *scheme of service* ya wafanyakazi wetu 30 au 31.

Nataka nikuhakikishie kwamba tatizo hilo tayari limeshatatuliwa na utakaporudi Pemba wewe nenda kahakikishe hilo jambo limemaliza tayari na wanafaidika na maslahi hayo kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

Mhe. Hija Hassan Hija alizungumzia suala la Ofisi ya Manispaa iliyoko sokoni. Yeye alisema Mwanakwerekwe lakini ni Darajani na yeye amekiri kwamba kweli ni Darajani. Nataka nimthibitishie kwamba Manispaa hatuwezi kufanya hivyo chini ya usimamizi wangu, hatuwezi kufanya jambo ambalo amelisema, lakini inaonekana taarifa alizozipokea ndio zilimueleza hivyo, na mimi simlaumu kwa sababu taarifa yoyote ukiipokea inabidi uifanyie kazi na kuifanyia kazi kwake yeye amekuja kuileta hapa.

Kilichopo ni kwamba kwanza nashukuru kwa kunipa taarifa, namshukuru sana kwa kunipa taarifa kwa sababu na mimi niliduwaa niliposikia lile. Lakini ukweli ni kwamba kweli Baraza la Manispaa limefanya kumbadilishia mfanyabiashara sehemu ya kufanyia biashara.

Ofisi ile kwetu sisi kwa wafanyakazi walioko pale ilikuwa ni kubwa mno, kwa hiyo tulichofanya ni kwamba tumeihamisha ofisi yetu kwa sababu ya mahitaji yetu tumekwenda pale alipokuwa akifanya biashara, pale tulipokuwepo sisi tumempa yeye afanye biashara ili atuongezee mapato zaidi. Hilo tumelifanya lakini si kwamba pameuzwa, hapakuuzwa isipokuwa ni katika kutafuta namna ya kuongeza mapato ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Hija pia amezungumzia suala la masafa ya soko la Mwanakwerekwe na nyumba za watu. Kwanza nataka nimthibitishie Mhe. Hija ndugu yangu, Mtumbatu mwenzangu na mimi nimuombe asiwe *disappointed*, maana ili uwe *disappointed* wale Watumbatu walioko Kisiwani wawe *disappointed* na wao hawajawa *disappointed* na mimi, bado wana imani na mimi na wataendelea kuwa na imani na mimi. Kwa hiyo, nikuombe Mtumbatu mwenzangu usiwe *disappointed*, na katika hayo mimi nadhani ukitaka kufanya tathmini mimi wala sitaki tufuatane uende mwenyewe, maana Tumbatu kwenu ukafanye tathmini ya kabla ya utawala wa mimi kuwa Mwakilishi na sasa hivi baada ya kuwa Mwakilishi. Sasa sijipigii debe maana muda wa kupiga debe utafika Mhe. Spika, lakini nina imani nikiamua kuchukua fomu watanichagua.

Kwa hiyo, suala la masafa ya *parking* na nyumba za watu. Kwanza kupitia Idara ya Ardhi na Usajili wananchi waliopo katika karibu na eneo la soko wote wale wamepimiwa viwanja, na kila mwananchi katika eneo lake ana *beacon* zinazoonesha mwisho wa *plot* aliyopewa kwa matumizi yaliyokusudiwa. Maana wananchi wale walipewa matumizi ya kujenga nyumba za kuishi, halafu serikali ikaacha eneo kwa ajili ya matumizi ya *public area*. Sasa tatizo ni kwamba baadhi ya wananchi wameingia kwenye eneo lile la *public* wamejenga maduka ya biashara, kwa hiyo na wananchi wengine wanafanya biashara katika eneo lile lisiloruhusiwa hatimaye msongomano wa magari unatokea. Lakini hakuna mwananchi ambaye amedhulumiwa pale ama na Manispaa ama na Halmashauri, isipokuwa wapo wananchi ambao wanafanya biashara kinyume na taratibu, hao wanasababisha msongamano wa magari katika eneo lile. Lakini nataka nimthibitishie kwamba kila mwananchi ana eneo ambalo amepimiwa na serikali, na hilo eneo ndilo anatakiwa alitumie kwa ajili ya shughuli za makaazi na sio nyenginezo.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na yeye ametupongeza na amewapongeza sana KMKM, amepongeza mradi wa *CCTV Camera*. Hapa nataka nichukue nafasi hii kuwaarifu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mradi kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya bajeti mpaka ikifika mwezi wa Disemba mradi huu utakuwa umekamilika.

Mradi utaweka *CCTV Camera* katika eneo lote la Mji Mkongwe na barabara nyengine za mjini, lakini pia kuna wenzetu ambao wamejitokeza kuja kutuongezea nguvu katika kutupatia *camera* za ziada, ili tuhakikishe katika mji wote wa Manispaa ya Unguja unakuwa salama. Mradi huu kwa wale ambao walizungumzia sana suala la zana za Idara Maalum.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie kwamba ndani ya mradi huu kuna *component* ya baadhi ya zana za Idara Maalum, zana ambazo zitahusika na masuala ya uokozi kama magari ya *fire*, zana ambazo zitahusika na masuala ya doria pamoja na uokozi *interceptor boats* ambazo zitakuwa zinakwenda kwa kasi, zana ambazo zitahusisha pia inapotokea ajali kutuma chombo kwenda kupiga picha na ikatueleza na ikatupa mawasiliano ya kuona tukio lile liko wapi, lakini na zana nyengine ambazo zitahusu Idara Maalum. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba kwa hili nilitolee ufafanuzi huo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri jitahidi ili ikifika kwenye saa sita na robo uwe umemaliza.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, ahsante sana. Sasa naomba nijibu yale matatu kwa ufupi sana. La kwanza limezungumziwa suala la upachuaji wa bendera. Hili nataka niliseme tu, juzi katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria lilijitokeza na kwa mujibu wa taarifa nilizonazo kwamba jambo hili liko Mahkamani. Kwa hiyo, tuiachie Mahkama ifanye kazi yake, mimi nisingependa kulizungumzia hili.

Pili, suala la mipaka ya kiutawala. Kwanza nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe hakuna ghila wala ghala, wala ghilba yoyote ile iliyofanyika katika jambo hili. Katiba yetu inamruhusu Rais wa Zanzibar kufanya kazi hiyo, sheria ambazo tumezipitisha za Serikali za Mitaa inaniruhusu mimi kugawa Wadi baada ya kumshauri Mhe. Rais, sheria pia inamruhusu Mhe. Rais kugawa mipaka ya kiutawala.

Kwa hiyo, katika hili nisemeje, niseme kwamba ugawaji huo wa mipaka ya kiutawala, mikoa, wilaya, shehia tumefuata taratibu za Katiba kifungu cha 2(a) cha Katiba ya Zanzibar. Ugawaji huo umewekewa utaratibu katika sheria ya Tawala za Mikoa Sheria Namba 7 ya mwaka 2014, tumeipitisha hapa kifungu cha 4 na kufuata misingi hiyo. Mhe. Rais amefanya kazi hiyo tarehe 8 Mei, 2015.

Kwa hivyo, Mhe. Rais amefanya hivyo na kuna vigezo. Zile sheria mkizisoma zimeweka vigezo vya kufanya hayo. Kigezo cha msingi kabisa ni idadi ya watu na Mhe. Rais katika kufanya kazi hiyo amezingatia hilo, wapo ambao wanasema kwamba kwa nini tubaki na wadi nane? Hata mimi nimebaki na wadi nane na

nilikuwanazo kuliko hizo nane, mimi mgawaji nimebaki na nane kwa sababu ndio utaratibu. Kwa sababu vigezo ndani ya sheria vinasema ili utimie kuwa wadi unatakiwa angalau uwe na shehia zisizopungua mbili, ugawaji wa zamani uliofanyika kulikuwa na shehia moja wadi moja, haiwezekani kwa mujibu wa sheria ya sasa, ili utimize kuwa na kigezo cha kuwa wadi uwe na watu wanaotimia kuanzia elfu tisa na kuendelea.

Sasa nyinyi fanyeni hesabu wenyewe sina haja ya kufanya hesabu mimi hapa, idadi ya watu milioni moja laki tatu mkigawa mtapata idadi ya wadi ziliopo. Kigezo cha zamani kwa sheria ya zamani hatukuzingatia utaratibu huu, sasa tumegawa wadi kufuatia utaratibu huu. *(Makofi)*

Sio haki kabisa Wilaya ya Magharibi A na B yenye watu laki tatu karibu na sabini elfu ukiacha na wadi zilizokuwepo ambapo hakuna Mkoa wowote wa Unguja na Pemba. Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkoa wa Kusini Pemba, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Unguja wenye idadi kubwa ya watu kama walivyo Wilaya ya Magharibi A na B. Hicho ndicho kigezo tulichokitumia, hakuna kigezo chengine tulichokitumia.

Sheria imeweka vigezo, sasa kama sheria ile haifai Mwenyezi Mungu akitujaalia watakaobahatika tuandae utaratibu wa kufanya marekebisho ya sheria, lakini kwa sheria ya sasa hivyo ndivyo ilivyo na hatuwezi kurudi nyuma. *(Makofi)*

Rais ameshatangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali na mimi Waziri nimeshatangaza. Kwa hiyo, kama sheria ina mapungufu utaratibu wa sheria si upo tutaona tutakaporudi serikalini, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atajaalia tulio wengi tutarudi serikalini.

Mwengine hapa alisema samahani ndugu yangu alisema kwamba wengine hawajajijua pengine hawatarudi. Ni kweli CCM wengi hatujajijua lakini *at least* Chama kiliomo humu ndani cha *CUF* wengine wameshajijua.

Ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija angalau kwa ule mchakato wa mwanzo wa kupata kura za mwanzo, lakini wapo hapa ambao wamepata kura nyengine zinaonesha kwamba pengine wanaweza wasirudi itategemea na maamuzi ya chama chao. Mimi nawaombea wote warudi, wale ambao watabahatika kurudi tutakuja kuangalia mchakato huo wakati huo. Lakini kwa sasa hii ndio sheria iliopo, na tumefuata vigezo hivyo sasa tusingeweza kufanya jambo jengine.

Maeneo hayo ya ugawaji wa wadi umefanywa kwa uwezo niliopewa mimi waziri niliyepo sasa, anaweza akaja mwengine baadae, mimi ndiye nasimamia sheria ya Serikali za Mitaa Namba 7 ya Mwaka 2014 kifungu cha 4(1) nimefanya kazi hiyo

kwa mujibu wa sheria hiyo. Hatukuifanya kwa sababu ya kutaka kitu gani, kwa sababu kokote kule wadi inakopelekwa kama unakubalika na wananchi si utachaguliwa, hofu ya nini? Kwa hiyo, tumefanya hivyo kwa sababu hiyo.

Ugawaji wa nchi katika Mikoa, Wilaya nishaisema nadhani niishie hapo. *Legal notice* hii niliyoisaini mimi Haji Omar Kheri kama waziri na nimefanya hivi kisheria wala sikukurupuka kama Waheshimiwa wengine walivyosema. Mimi sina kawaida ya kukurupuka, mimi mambo yangu yanakwenda kwa murua kabisa sikurupuki, *legal notice* ya Mhe. Rais hii ameshaisaini.

Taarifa ya kuniridhia kwamba nifanye hivyo nimeshafanya alichokifanya Mhe. Rais, kwa hivyo haturudi nyuma. Mhe. Spika, kwa hiyo katika eneo hilo ningependa niseme hivyo na haya mengine ambayo yanasemwa sidhani kama ndivyo yalivyo. Kwa hiyo, hapo ningeishia hapo.

Kuhusu suala la kadi za utambulisho. Hoja binafsi ililetwa hapa na hapa tuna utaratibu kwa mujibu wa Kanuni, jambo likishazungumzwa ndani ya Baraza kwa muda gani linatakiwa hilo jambo lisirejewe rejewe. Hoja ililetwa Baraza likaamua, sasa kuna maamuzi gani mimi siwezi kupinga maamuzi ya Baraza, majibu ni yale sina majibu mengine. *(Makofi)*

Jengine kuhusu hoja hii nakumbuka Mhe. Hassan Hamad Omar amesema hapa kwamba alileta vyeti na mimi siku ile nilisema wazi wazi kwamba kwa wale ambao wana risiti zao wapeleke ofisini kwangu ili ikajulikane tatizo ni nini.

Nashukuru kwa Mhe. Hija Hassan Hija katika watu mia moja na arobaini na kitu aliyotoa karibu watu 104 wiki mbili zilizopita walikuwa wameshapata vitambulisho vyao. Hiyo nasema kwa uhakika Mhe. Hija Hassan labda afuatilie watu 104 walishapata vitambulisho vyao kwa zile risiti ambazo ameziwasilisha, waliobakia wakawa wanafanyiwa kazi. Wengine kati ya wale walikuwa bahati mbaya wao walikwenda Jimbo la Kiwani moja kwa moja wakawa hawakutoka jimboni kwako wakawa wanafuatilia taarifa zao katika maeneo mengine.

Waheshimiwa wengine nao wangefanya hivyo kwa sababu mimi nilitoa wito na ninavyosema hivi sasa vile vitambulisho ambavyo vinapigiwa kelele vyote viko wilayani, na taarifa nilizonazo kwamba wiki hii iliyokwisha watu wengi wameanza kwenda kuchukua vitambulisho vyao, na mimi nitaendelea kufuatilia ili hivyo vitambulisho vilivyoko huko katika wilaya basi viendelee kupewa watu wenyewe na wanapewa wenyewe.

Mmoja hapa alithibitisha Mhe. Farida Amour kwamba kwa Wilaya ya Wete waliweka utaratibu kimajimbo wakawa wanakwenda kuchukua, na wilaya

nyengine nadhani nitoe wito waige mfano huo na watu waende wakachukue vitambulisho vyao.

Dhana iliyojitokeza ya watu kushushwa Mkokotoni. Mimi Mkokotoni jimboni kwangu, wanaoshushwa Mkokotoni ni abiria halali wanaokuja na biashara zao wakimaliza wanarudi katika maeneo yao wala hawaji kwa madhumuni ya kuandikishwa.

Mhe. Spika, kwa hiyo baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo hayo ya ufafanuzi, na sasa naomba nichukue nafasi hii kuwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU D01 - OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

KIFUNGU P01 PROGRAMU YA URATIBU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Programu Ndogo S01 Uratibu Tawala za Mikoa Sh.2,063,884,000/=

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake na nilihoji utendaji wa Baraza la Manispaa ambapo nadhani Programu ndogo S01 na P04 zinazohusika kwenye usimamizi wa uratibu wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba nilimtaka Mhe. Waziri atusaidie kwenye eneo la Mlandege kuna *transformer* imeingizwa kwenye ukuta wakati *ZECO* wenyewe waliweka wazi kwa madhumuni kwamba ikitokezea *emergency* ya moto Zimamoto waweze kuja kuzima moto ule na *transformer* kubwa inayosambaza moto katika mji imezingirwa. Jambo ambalo hata leo ikitokezea *short* ya umeme hakuna Zimamoto atakayeweza kwenda. Sasa niombe tu kwamba ule ukuta ni ruhusa ya Manispaa au ni ya nani au ni ruhusa ya Katibu wa Mkoa, tunataka tuweze kujua hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua hilo jambo lakini kwa sababu ya muda sikuweza kumjibu.

Nadhani nimuombe tu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba taarifa nimeipokea na kwa sababu nilipofuatilia kwenye Baraza wao hawahusiki na hilo jambo. Kwa hivyo, nitalichukua nishirikiane na watu wa *ZECO* ili nione kama aliyejenga ukuta hana kibali basi tutachukua hatua ya kumvunjia ili eneo hilo liwe salama.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, *ZECO* waliweka *transformer* lakini ufatiliaji wangu wa kina kibali cha kujenga ukuta wametoa Manispaa wakijua kwamba pale kuna *transformer* ya *high tension*. Sasa *ZECO* kazi yao ni kuweka umeme wamefanya kazi hiyo. Kibali cha ujenzi wa ukuta wametoa Manispaa ndio hoja yangu, kwa nini wakatoa Manispaa wakati kuna ukuta.

Sasa mamlaka ya ukuta ndani ya *transformer* kubwa katoa Manispaa wakati kibali mimi nimefatilia binafsi wametoa Manispaa, nataka kwamba je, Waziri atwambie kwamba ukuta utabakia ili kulinda kibali cha Manispaa au ukuta utaondoka ili kulinda masuala ya usalama wa wananchi na mali zao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Hija Hassan Hija angenifahamu nilivyosema kwamba tutalifuatilia, na ikiwa kwa sababu taarifa ya mwanzo ilikuwa watuletee *ZECO* kama wana matatizo na hili basi tungeshajua ukweli wa mambo na tungefatilia. Lakini na yeye ametupa taarifa hapa kwamba kuna tukio hilo, ndio maana nimemwambia Mhe. Hija Hassan Hija nitafatilia na nikibaini kama kuna jambo limetendeka kinyume na utaratibu tutavunja ukuta. Sasa nisingekuwa na kauli nyengine zaidi ya hiyo.

Kwa hiyo, iwe Manispaa wametoa kibali iwe mtu kajenga bila ya kupata kibali kama lipo kinyume na utaratibu tutachukua hatua ya kuvunja huo ukuta ili eneo libaki salama.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Waziri nimeyakubali na hoja yangu ni kwamba sasa ikifika Hotuba ya Wizara ya Maji ambapo ndiko kwenye *ZECO* huko itabidi tuwaulize ile idhini ya ukuta ni *ZECO* ili turidhike kama si ya *ZECO* maana yake imeenda utaratibu mbovu. Nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba afatilie na mimi naendelea kufanya kazi *ZECO* ili kujua kama ruhusa yao au si yao ili tuweze kwenda sambamba na tutajua usalama wa wananchi. Tuendelee.

Programu Ndogo S01	Uratibu Tawala za Mikoa	Sh. 2,063,884,000/=
Programu Ndogo S02	Uratibu wa Serikali za Mitaa	Sh. 276,819,000/=
Jumla ya Programu P01		**Sh.2,340,703,000/=**

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Programu Ndogo S01	Uratibu wa Idara Maalum	Sh. 53,883,000/=
Jumla ya Programu P02		**Sh. 53,883,000/=**

KIFUNGU P03 - USIMAMIZI WA UTUMISHI WA IDARA MAALUM

Programu Ndogo S01	Usimamizi wa Utumishi katika Idara Maalum	Sh.138,000,000/=
Jumla ya Programu P03		**Sh.138,000,000/=**

KIFUNGU P04 - PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Programu Ndogo S01	Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Tafiti katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum	Sh. 10,295,511,000/=
Programu Ndogo S02	Usimamizi wa Shughuli za Utumishi na Utawala katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum	Sh. 1 ,219,546,000/=
Programu Ndogo S03	Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikao na Idara Maalum Pemba	Sh. 542,557,000/=
Jumla ya Programu P04		**Sh. 12,057,614,000/=**
Jumla Kuu		**Sh. 14,590,200,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 01 Utawala Unguja	Sh.36,337,000/=
Jumla Kuu	**Sh.36,337,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA MAFUNZO NA AMALI UZALISHAJI UZALENDO NA MICHEZO KWA VIJANA

Programu Ndogo S01	Uzalendo, Uzalishaji na Michezo	Sh.1,885,600,000/=
Programu Ndogo S02	Ufundi na Kazi za Amali	Sh. 736,700,000/=
Jumla ya Programu P01		**Sh.2,622,300,000/=**

KIFUNGU P02 PROGRAMU YA ULINZI, MIPANGO NA UENDESHAJI WA JKU

Programu Ndogo S01 Ulinzi Mipango na Uendeshaji wa JKU	Sh. 8,182,200,000/=
Jumla ya Programu P02	**Sh. 8,182,200,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.10,804,500,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D03 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 01- Idara ya Vyuo vya Mafunzo	Sh. **50,586,000/=**
Jumla Kuu	**Sh. 50,586,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D03 - CHUO CHA MAFUNZO

KIFUNGU P01 - HUDUMA ZA UREKEBISHAJI WANAFUNZI WA CHUO CHA MAFUNZO

Programu Ndogo S01 Huduma za Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo	Sh.921,252,000/=
Jumla ya Programu P01	**Sh.921,252,000/=**

KIFUNGU P02 - UONGOZI NA UTAWALA WA CHUO CHA MAFUNZO

Programu Ndogo S01 Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo	Sh.7,054,048,000/=
Jumla ya Programu P02	**Sh.7,054,048,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.7,975,300,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 01 Utawala Unguja	Sh.**25,891,000/=**
Jumla Kuu	Sh.**25,891,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA ULINZI NA UZUIAJI WA MAGENDO

Programu Ndogo S01 Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo	Sh.1,013,500,000/=
Jumla ya Programu P01	**Sh.1,013,500,000/=**

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA KMKM

Programu Ndogo S01 Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM	Sh.12,639,500,000/=
Jumla ya Programu P02	**Sh.12,639,500,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.13,653,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu P01 Utawala Unguja	Sh.**17,606,000/=**
Jumla Kuu	Sh.**17,606,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA UTOAJI WA HUDUMA ZA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Programu Ndogo S01 Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	Sh.274,239,000/=
Jumla ya Programu P01	**Sh.274,239,000/=**

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA KUKUZA HUDUMA KIUTAWALA NA KIUONGOZI KWA WAFANYAKAZI WA KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Programu Ndogo S01 Kukuza huduma kiutawala na Kiuongozi kwa Wafanyakazi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	Sh.4,039,061,000/=
Jumla ya Programu P02	**Sh.4,039,061,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.4,313,300,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D06 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 01 Utawala Unguja	Sh.**17,606,000/=**
Jumla Kuu	Sh.**17,606,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D06 - KIKOSI CHA VALANTIA

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA AMANI NA UTULIVU KWA RAIA, TAIFA NA MALI ZAO

Programu Ndogo S01 Amani na Utulivu kwa Raia,
Taifa na Mali zao Sh. 417,792,000/=

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nilipochangia nilimwaambia Mhe. Waziri kuhusu ulipaji wa watu na mali zao katika Afisi inayojengwa Micheweni ya Kikosi cha Valantia.

Mhe. Waziri amenijibu kama wamelipa mali zile kwa wananchi shilingi milioni moja, na akanambia orodha anayo. Sasa Mhe. Waziri wamelipa mazao yaliyokuwemo lakini zile ardhi za watu na wajibu serikali inapotaka kutumia eneo ardhi ni mali ya serikali sawa, lakini inastahiki wale wananchi kulipwa fidia katika yale maeneo yao.

Kwa hiyo, wamelipa fidia ya mazao tu, lakini ile ardhi kwa sababu wananchi wanaitumia, sasa nilitaka na wananchi walipwe fidia ya ardhi yao, hajanijibu suala akanijibu kama wamelipa yale mazao yaliyokuwemo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, tulichofanya kwa mujibu wa taratibu na sheria ya ardhi inavyosema.

Kwanza ardhi ni mali ya Serikali, na ardhi ile katika wananchi waliokuwepo pale hakuna aliyekuwa anaimiliki. Ni ardhi ambayo walikuwa wanaitumia kwa kilimo lakini ni ardhi ya Serikali.

Kwa hivyo, kama ardhi ya Serikali tulichotakiwa sisi kulipa fidia ni yale mazao ambayo yalikuwepo pale, lakini kama wananchi wale angekuwepo mmoja ambaye anaonesha kwamba ana umiliki wa lile shamba, basi hayo tena yangefanywa na taasisi zinazohusika zingefanya thamani ili hayo anayosema Mhe. Subeit Khamis Faki.

Lakini kwa mujibu wa watu tuliowakuta pale, hakuna mwenye kumiliki ardhi isipokuwa kama utaratibu wetu ikiwa unaishi kwa mfano Bweni, unaishi Tumbatu unatafuta pahala unatafuta rizki, lakini ardhi ile haiwi yako, lakini ni kweli pale pahala ni pahala ambapo panakupa kipato. Kwa hivyo, Serikali inapotaka kutumia ardhi ile unachotakiwa wewe kufanyiwa ni kuweza kulipwa yale mazao ambayo yapo juu ya ardhi ile.

Lakini kama yupo mtu ambaye alikuwa ana umiliki, basi taarifa hizo ni vizuri atuletee. Mhe. Subeit ili tufuatilie tuone ukweli wa mambo ukoje, lakini tulichokifanya sisi, tumekifanya kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwanza kama ni kweli kwa mujibu wa sheria yetu ya nchi kama ardhi ni mali ya Serikali. Lakini utamaduni wetu tulionao ni lile eneo Serikali ikiwa inataka kuchukua kutumia wale wanaokaa pale wanaofanya kilimo kwa muda mkubwa wanalipwa fidia juu ya maeneo yao.

Sasa yeye Mhe. Mwenyekiti, alilipa kweli mazao kwa mujibu anavyoeleza, na yeye mwenyewe kaeleza kama wamelipa shilingi milioni moja. Sasa yale maeneo mulikuwa na baadhi ya minazi imekatwa. Sasa wenyewe wamekuja wananchi kunilalamikia mimi kama Mwakilishi wao kwa ajili ya kuwasaidia kwa jambo hili.

Sasa ndiyo ninamwambia Mhe. Waziri ni kweli, na kwetu utamaduni wetu maeneo mengi hakuna utakayemwambia atoe hati miliki akatoa kwa sababu utamaduni huo hatuna. Maeneo yote labda maeneo yale yanayoitwa maeneo huru. Kule ni maeneo huru na Serikali imeshatangaza, lakini huku bado haimo katika maeneo huru na wenyewe wanalimalima wakisaidiana na watoto wao.

Sasa kama Serikali inawaondoa ingewalipa fidia ijapokuwa kidogo. Sasa kwa sababu wananchi ni wanyonge tukisema tu tusiwalipe hata fidia itakuwa hatukuwatendea haki. Kwa hivyo, mimi kama Mwakilishi wao ninamuomba Mhe. Waziri aone kama wale watu wapewe japo fidia ndogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Siwezi nikawaonea huruma nikapinda sheria, lazima nifuate sheria kwanza, hiyo sheria iniruhusu mimi kuwaonea huruma, ninawaonea huruma sana mimi. Lakini sheria hainiruhusu kuwaonea huruma kwa sababu hapa hakuna *options*. Jambo la hapa ni kufuata sheria na taratibu na ndivyo tulivyofanya.

Sasa Mhe. Mwakilishi ninajua yeye anawawakilisha wananchi, aende akawaambie hivyo ili aendelee kuwa Mwakilishi mzuri. Lakini akienda akiwaambia vyenginevyo ninadhani hiyo haitasaidia sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwakilishi mzuri nikienda hivyo au nisiwaambie wanajua kama ni Mwakilishi mzuri, na ndiyo maana wakanichagua kwa kura nyingi, kwa sababu ni Mwakilishi mzuri. (*Makofi*)

Lakini ninawatetea haki zao. Lile eneo wamekaa wamelima kwa muda mkubwa, kwa sababu mtu anapokaa miaka zaidi ya ishirini eneo lile Serikali inapotaka kuchukua, linakuwa lile eneo lina mwenyewe na ndiyo maana tukawa hata sisi raia katika kuishi kwetu, tukiambiwa tukiishi sehemu baada ya miaka mitatu unaambiwa ni mkaazi. Ni sheria yenu muliyoipitisha nyinyi wenyewe humu, baada ya miaka mitatu tu ukikaa pahala unaambiwa sasa ni mkaazi.

Sasa na hawa wao wamekaa zaidi ya miaka ishirini katika maeneo yale, kweli Serikali ina sheria inayosema hivyo. Lakini sasa je, kwa sababu unataka kumtoa sehemu ile aliyekuwa ameshazoea kufanya kazi kwenda sehemu nyengine, basi hata fidia ndogo asipewe.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! mimi ninadhani. Eeh! kuna maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii hata siku moja haitomdhulumu mwananchi haki yake, na haki ndiyo tukawalipa mazao, hii ndiyo haki yao. Ardhi siyo haki yao.(*Makofi*)

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba Mwenyekiti una busara sana. Hapa tunazungumzia *peace and security,* hatuzungumzii *development*. Sasa hata tukiwa tunaendelea kuyatetea mambo kama haya, ninadhani hatutofika pahala. Lakini kimsingi haki ya wananchi tumeilipa, ardhi siyo haki yao kwa sababu ni mali ya Serikali. (*Makofi*)

Lakini hapa tunazungumzia *peace and security*, amani na utulivu, hatuzungumzii masuala ya *development*, ndiyo programu hii inavyosema. Kwa hivyo nimefanya ihsani kama ulivyofanya wewe kutoa ufafanuzi kwa Mhe. Subeit. Atuachie tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Acha mimi nitoe ushauri kwamba Mhe. Mwakilishi arudi kwa wananchi aende kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati awaombee Waheshimiwa hawa wapate eneo jengine ili watumie.

Sasa hiyo ninadhani itasaidia ili kuona kwamba kama hawana pahala pengine basi muache aende kwenye Wizara inayohusika ya Ardhi ili awaombee eneo la kuweza kutumia au wao wenyewe wafanye hivyo kwa ajili ya kupata matumizi ya kilimo hicho.

Ninadhani baada ya hayo nashauri tungeendelea.

Kifungu P01	Programu ndogo Amani na Utulivu kwa Raia, Taifa na Mali zao	Sh. 417,792,000/=

Kifungu P02	Programu ya Usimamizi na Utawala wa Kikosi cha Valantia	Sh. 5,585,808,000/=

Jumla ya Kifungu	**Sh.5,585,808,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.6,300,600,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D07 - MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Kifungu 01	Mipango na Sera	Sh.29,954,000/=

Jumla Kuu	**Sh.29,954,000/=**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D07 - MKOA WA MJINI/MAGHRIBI

Kifungu P01	Programu ya Uratibu wa Shughuli (Miradi ya Maendeleo)	Sh.264,066,000/=
Kifungu P02	Programu ya Usimamizi na Utawala wa Mkoa	Sh. 1,257,734,000/=

Jumla ya Kifungu	**Sh.1,257,734,000/=**
Jumla Kuu	**Sh.1,521,800,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D08 - MKOA WA KUSINI - UNGUJA

Kifungu P01	Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa wa Kusini Unguja	Sh. 203,353,000/=
Kifungu P02	Programu ya Uendeshaji na Utawala Mkoa wa Kusini Unguja	Sh.1,133,247,000/=

Jumla ya Kifungu **Sh.1,133,247,000/=**
Jumla Kuu **Sh.1,336,600,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D09 MKOA WA KASKAZINI - UNGUJA

Kifungu P01 Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo Ndani ya Mkoa Sh. 240,018,000/=

Kifungu P02 Programu ya Utawala na Uendeshaji Sh.1,133,832,000/=

Jumla ya Kifungu **Sh.1,133,832,000/=**
Jumla Kuu **Sh.1,373,900,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D10 MKOA WA KUSINI - PEMBA

Kifungu P01 Programu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa Shs.19,980,000/=

Jumla ya Kifungu **Sh.19,980,000/=**

Kifungu P02 Programu ya Kuratibu Shughuli za Ulinzi na Usalama Ndani ya Mkoa Sh. 5,665,000/=

Kifungu P03 Programu ya Mipango na Utawala katika Mkoa Sh.1,746,355,000/=

Jumla ya Kifungu **Sh.1,746,355,000/=**
Jumla Kuu **Sh.1,772,000,000/=**

FUNGU D11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu P01 Programu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa Shs.79,992,000/=

Kifungu P02 Programu ya Kuratibu Shughuli za Ulinzi na Usalama Shs.6,581,000/=

Kifungu P03 Programu ya Mipango na Utawala katika Mkoa Shs.1,573,027,000/=

Jumla ya Kifungu **Shs.1,573,027,000/=**
Jumla Kuu **Shs.1,659,600,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D12 - OFISI YA USAJILI WA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu P01 Programu ya Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho Sh.17,606,000/=

Jumla ya Kifungu **Sh.17,606,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D12 - OFISI YA USAJILI WA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu P01 Programu ya Kusajili na Kutoa Vitambulisho kwa Wazanzibari wote na wasio Wazanzibari wanaoishi Kisheria.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimwambia Mhe. Waziri kama kuna watu ambao wamepiga vitambulisho kuanzia tangu mwaka jana, lakini kuna watu ambao wamepewa vitambulisho kuanzia mwezi wa sita mwaka jana mpaka kufika mwezi wa kumi na mbili. Lakini kuanzia Januari mpaka hivi sasa kuna watu wana risiti za kuchukulia vitambulisho lakini vitambulisho vyao hawapewi, wakifika wanaambiwa vitambulisho vyenu havijaletwa havipo.

Sasa mimi nilikuwa atwambie hasa Mhe. Waziri kwa sababu tulipitisha sheria ndani ya Baraza la Wawakilishi, na sheria inamtaka mtu ili awe amesajiliwa kwenye vitambulisho akamilishe yale masharti. Sasa wale watu ambao wameshakamilisha yale masharti na wameshakwenda kupiga picha kwa ajili ya kupewa vitambulisho, wanakuwa na muda gani kupata vitambulisho vyao. Maana atwambie hapa tujue na kila mwananchi asikie.

Kwa sababu unafika mwezi wa sita huu watu hawajapewa vitambulisho vyao na wakati tulipokaa na Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Vitambulisho, kipindi tulichokuwa tukavutanavutana mpaka tukaenda tukakaa pamoja, walitwambia hivi ili mtu apate kitambulisho chake hafiki wiki mbili.

Sasa ni miezi sita. Sasa atwambie Mhe. Waziri ili mtu apate kitambulisho baada ya kukamilisha hayo masharti ni muda gani atapata kitambulisho chake.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa ufafanuzi juu ya jambo hili nimesema kwamba vitambulisho vyote mpaka vya mwezi wa Aprili vipo Wilayani, sasa waende huyo atakayekosa kitambulisho Mhe. Subeit aniletee risiti yake.

Lakini vitambulisho vipo Wilayani waende wakachukue.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninasema hivyo sisemi kwa kubahatisha. Tumekwenda karibuni tumekaa kitako na Ofisa Mipango baada ya Mkuu wa Wilaya wa Micheweni anaumwa alipata matatizo kidogo akaumia mguu anaumwa.

Lakini na Ofisa Tawala aliyekuwepo pale ana uhamisho. Sasa aliyekuwepo pale anayekaimu ni Ofisa Mipango. Tumekwenda tumekaa naye kama timu na wakatupa ufafanuzi, wakaitwa wale wanaotoa hivyo vitambulisho vyenyewe wakaitwa na wakatueleza wazi wazi tukiwa Kamati nzima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwemo, Mhe. Rufai Said alikuwemo na baadhi ya Wabunge na Wawakilishi tulikwenda, tukakaa pale tukazungumza. Walitueleza wazi wazi kama vitambulisho vilivyopo ni vya kuanzia mwezi wa 12, yaani mwezi wa 6 mpaka vya mwezi wa 12. Kuanzia Januari mpaka sasa havijaletwa, na kama Mhe. Waziri anasema vitambulisho vipo, basi ndio pale tunaposema kwamba vitambulisho vipo lakini hamtaki kuwapa watu.

Maana akithibitisha kama vipo basi ndio ushahidi tosha kama vitambulisho vipo, lakini kuwapa ndo hamtaki na ilikuwa mnafanya hivyo ikiwa leo mnatwambia vipo, kwa sababu leo mwisho wa daftari Micheweni, ni kwamba yale matakwa yenu yameshakamilika, kama lipite daftari ndio watu wapewe vitambulisho. Sasa tukisema hapa mnatwambia kama tunapiga kelele tu ovyo ovyo. Hatupigi kelele ovyo mnatufanyia mabaya.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo zaidi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, sijawahi kumfanyia mtu vibaya, na mimi nasema kwa uhakika. Wananchi wa Wilaya ya Micheweni waliopata risiti zao waende wakachukue vitambulisho vyao wilayani. Hayo maneno anayosema Mhe. Subeit Khamis Faki, nadhani ndio nayasikia sasa. Kwa hivyo, aende halafu na mimi niyasikie kwa hao maafisa wanaowarudisha watu.

Lakini mimi ninachosema ni kwamba nasema kwa uhakika, kwamba vitambulisho vipo, wananchi waende wakachukue.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit Khamis, uende ukachukue vitambulisho vya wananchi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi sisemi kwa kubahatisha wala sisemi kwa sababu nina nia ya kusema tu, hapana.

Nilipochangia hapa nilisema Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna mtu anaitwa Said Mbwana Hassan, alikwenda kujitambulisha akapigwa picha, kisha akapewa kitambulisho chake cha kuchukua. Baada ya kufika siku ya kwenda kuchukua kitambulisho, anaambiwa kawekewa pingamizi. Kwa nini, akaambiwa tangu mwaka 2000 hujaja kujiandikisha mpaka unakuja kujiandikisha leo, wakati huyu mtu alikuwa nyuma hana cheti cha kuzaliwa, hajakamilisha masharti, akakamilisha masharti. Alipokwenda mwenyewe keshakamilisha masharti, kitambulisho chake anapigwa danadana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sisemi hivyo kwa kubahatisha, na sio mmoja, wapo wengi ambao wameanza tangu mwezi wa Januari, mpaka sasa hivi hawajapewa vitambulisho.

Leo kama Mhe. Waziri anasema waende leo kwa sababu mmeshakamilisha ndoto yenu. Kwa sababu daftari leo ni mwisho Micheweni, saa hizi wakienda watapewa kweli kwa sababu yale matakwa yenu yameshakamilika. Sisi tukisema mnasema tunapiga kelele tu, sio wendawazimu sisi, tuna akili zetu timamu kama nyinyi mlivyokuwa na akili. Lakini tunapiga kelele kutokana na ile dhulma inayofanywa, na tukisema humu tunaonekana kuwa tunasema tu, hatusemi tu, tupunguzieni mambo mengine jamani, mambo mengine mnayofanya yapunguzeni.

Kwa sababu leo daftari ni mwisho Micheweni, watu waende kweli watapewa, maana matakwa yameshapita, hawaingii tena kwenye daftari, na ndio maana walikuwa wakipingwa ili wasiingie. Kwa hivyo, kama Mhe. Waziri anasema vitambulisho vipo watu waende ndio alama tosha hiyo ya kuwa walikuwa wakiwazuia watu makusudi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tulikubaliana kwamba kunapokuwa na hoja za aina hii na zote zinaelekeana kuwa ni za aina moja, basi ilikuwa tuchukue huyu na Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Hija Hassan Hija, ili hatimaye sasa maelezo atoe kwa ujumla. Lakini nimalizie pale halafu tena tutoe nafasi ndogo tusikie kinachozungumzwa hapa.

Mhe. Subeit Khamis Faki, shirikiana na Mhe. Waziri ufuatilie huyo mmoja pamoja na wengine, na kama kuna matatizo basi kama alivyosema rudi kwake ili muweze kushirikiana, wapate vitambulisho wote wale ambao walikwishakupata risiti zao. Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilisema kuna usumbufu wa kutosha katika utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari. Lakini katika hoja binafsi ya Mhe. Hamad Masoud, nilitoa ushahidi wa vyeti 103 vivuli yaani kopi.

Jana nilizungumza hapa kama aliyekuwa akiendesha kikao ni Mhe. Naibu Spika. Sasa katika kujibu hoja Mhe. Waziri alisema kwamba kuna vyeti bandia. Nataka kujua vyeti vile 103 vya Jimbo la Kojani, ni vingapi bandia na *original* ni vingapi, atupe majibu. Kwa sababu mwanzo wa kutafuta hizo kadi za vitambulisho vya Mzanzibari uwe na cheti katika masharti yake. Naomba kujua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, hoja yako ni kama hii ya Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni hoja ya eneo hili lakini langu mimi dogo sana.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu iseme kabisa ili Mhe. Waziri ajibu kwa pamoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Waziri amekiri kwamba nilimpa risiti 153, nakiri kwamba nilimpa kweli. Leo amekiri kwamba risiti hizo 153 zaidi ya 140 kadi ziko wilayani.

Mimi ni mtu wa Kiwani yeye mwenzangu ni Mtumbatu na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani ni mtu wa Kiwani. Leo tukutane hapa nje amuulize, ni mara ngapi watu wa Kiwani wamekwenda anawaambia hakuna.

Ninavyoamini mimi na nataka niwaambie wenzangu kama Wawakilishi, ninavyoamini mimi. Makao Makuu ya vitambulisho wamesambaza, na sisi kama Wawakilishi, kamati yetu ya Wawakilishi ilikwenda kumuona Mkurugenzi wa Vitambulisho bahati mbaya akawa hayupo tukamuona Naibu. Tatizo lipo mawilayani.

Sasa atwambie Mhe. Waziri je, yeye amekiri kwamba 153 nilizompa zaidi ya 140 ziko wilayani. Wakati Mkuu wa Wilaya hadi jana watu wanasumbuka kutoka Kiwani, yeye ni mtu wa Kiwani. Atwambie je, kamuagiza azuie au ni utashi wake,

ili watu wa Kiwani wajue kwamba Mtumbatu wa Jongowe sio tatizo, tatizo ni Mtumbatu wa Kiwani Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Hassan Hamad kasema. Lakini hivyo vyeti vya kuzaliwa kwanza hakunikabidhi mimi, kwa hivyo suala hilo silijui isipokuwa alilichangia.

La pili suala la hoja binafsi tulilimaliza, hatuwezi tena hapa tukaja na suala la hoja binafsi na Baraza limeshafanya maamuzi. Hilo ni la Mhe. Hassan Hamad.

Mhe. Hija Hassan Hija, nilichosema katika risiti alizoleta. Risiti za vitambulisho 104 zilitambuliwa na wananchi wenyewe walishaanza kuvichukua. Sasa kama hivyo sivyo, hizo ndio taarifa nilizonazo mimi Waziri. Sasa kama anazo taarifa nyengine na anasema hapa chini chini kanidanganya. Lakini watendaji wale hakuna anayethubutu kunidanganya mimi, kunidanganya kwao basi ni hatari kwao, wanajua wao.

Kwa hivyo Mhe. Hija Hassan nataka nikwambie hakuna anayeweza kunidanganya wale hata mmoja. Kwa hivyo, kama kuna tatizo katika vile vyeti ambavyo vilitambuliwa kwamba ni watu wa Jimbo la Kiwani 104, kuna ambaye hajapata ndugu yangu nakuomba uniambie, katika wale huyu hajapata ili aende wilaya akachukue, wala sina maelekezo yoyote ninayoweza kumpa mimi Mkuu wa Wilaya kuhusu haki ya mtu hapana, ni wajibu wake yeye wa msingi kutekeleza kutoa hiyo haki.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Hija Hassan katika wale watu 104, nilisema katika wale watu zaidi ya 100 ambao walipeleka risiti, na nilisema watawatambua wale kwa sababu taasisi yetu ina uwezo, ukiiona tu ile risiti basi utajua kitambulisho hiki kiko wapi.

Kwa hivyo, kwa muda mfupi tulitambua vitambulisho 104 vilikuwa ni halali vya watu wa Kiwani. Watu wanne walikuwa sio watu wa Jimbo la Kiwani, na wengine walikuwa wanafanyiwa kazi. Sasa mimi nadhani hakuna haja ya kubishana hapa, katika wale kama yupo ambaye hajapata. Kama alivyosema mjumbe, Mtumbatu aliyehamia Kiwani katoka Tumbatu, wala hakutoka Makunduchi, katoka Tumbatu. Kwa hivyo Watumbatu Kisiwani na wa Mwambe ndio wale wale.

Kwa hivyo, Mheshimiwa aamini hilo, na kama ataleta hiyo, kuwa katika wale hakuna aliyepata, basi tutafanya utaratibu kutatua hilo. Lakini mimi ninalosema nina uhakika na wala hakuna anayeweza kunidanganya. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani nitoe maelekezo, kuhusu Mhe. Hija Hassan nadhani maelekezo yawe kama ya Mhe. Subeit Khamis Faki. Hebu fuatilia kukiwa na tatizo shirikiana na Mhe. Waziri ili umrejeshee kwa wale ambao bado hawajapata na risiti zao zilikuwa ziko tayari, fanya hivyo. Mhe. Hassan Hamad.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anifahamu. Katika kopi za vyeti nilivyotoa 103, nilitolea mfano. Lakini jana nilizungumza katika kadhia hii ya vitambulisho. Sasa nataka anifahamu kama vyeti vile 103 nilivyotolea mfano, ni vingapi *fake* na vingapi *original*, ili wananchi wale vile vilivyokuwa halali wapate. Hii ndio *concern* yangu niliyoeleza hakuna jengine. Lakini akiniambia kama hoja imepita, sio kama imepita nilichangia jana, najua siku ile imepita ndio tumemaliza. Lakini jana nilichangia katika kadhia hii, au wale wananchi ndio wameshapuuzwa moja kwa moja, vile vilivyoletwa hapa vyote ndio *fake*, tueleze kama ni *fake* tujue kama ni *fake*, halafu hivyo *original* watu wapatiwe. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kuna maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ili uthibitishe kwamba cheti kilichotolewa ni *fake* au sio *fake*, ni lazima uwe nacho, utafute namna ya kukithibitisha.

Ninachosema mimi vyeti hivyo sikupewa, sasa kama sikupewa nitavithibitisha vipi. Kama anataka nifanye kazi hiyo nitashirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria kuthibitisha, anipe tu hivyo vyeti. Sasa mimi hivyo vyeti sijapewa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Hamad nadhani hili suala la kutaka kuthibitisha hapa itakuwa kwa sasa gumu. Hebu shirikianeni kati ya wizara hii na wizara hii, ili kuona vyeti hivyo uthibitisho wake ukoje, juu ya u-*fake* au la, na baada ya hapo basi tungeendelea. Shirikiana nao Mhe. Waziri hao.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Spika, na yeye ashiriki katika kuvitoa vile, kwa sababu siku ya pili aliniambia nikachukue makaratasi yako, hakuyaona aliyapeleka wapi, avitafute aje navyo tushirikiane sote. Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Naibu Spika, sote tushirikiane tutambue ukweli uko wapi. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Hamad mimi nadhani maelekezo yangu yamebaki pale pale, shirikiana na wahusika. Naibu Spika, alikuwa mezani kama mimi, hawezi akafanya *identification* kama hiki sawa au sio sawa. Shirikiana na wahusika, wahusika kwa hapa ikitoka hapa inakwenda hapa. Hebu shirikiana nao

hawa mfanye hiyo kazi, na hapa uturuhusu tumalize hii na muda wetu utatosha kumaliza kazi, tuendelee.

Programu Ndogo S01	Kusajili na kutoa vitambulisho kwa Wazanzibari wote na wasio Wazanzibari wanaoishi kisheria	Sh.75,000,000/=
Jumla ya Programu P01		**Sh.75,000,000/=**

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA UTUMISHI NA UENDESHAJI OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Programu Ndogo S01	Utumishi Na Uendeshaji Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	Sh.1,693,009,000
Jumla ya Programu P02		**Sh.1,693,009,000/=**
Jumla ya Fungu		**Sh..1,768,009,000/=**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa mashirikiano, katika wizara ambayo mipango yake imekwenda juu ya utaratibu moja ni hii. *(Makofi)*

Tulikubaliana michango imalizike saa 5:00 imemalizika saa 5:00. Nilimuomba Mhe. Waziri amalize saa 6:15, kamaliza saa 6:00. Mafungu kuyakamilisha bado kama dakika mbili tu. Kwa hivyo, mambo yote yamekwenda kwa utaratibu.

Nawashukuru sana kwa mashirikiano hayo, kufanikisha kuendesha shughuli hii kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru wote pamoja na watendaji ambao kwa wizara hii ni ya pekee, watendaji wamejitokeza kwa wingi sana na tunawashuhudia wote pale. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Huu ndio uzuri ukiwa na wizara ambayo inahusiana na watu wa vikosi namna hii, Idara Maalum namna hii, nidhamu yake inakuwa ya juu sana, na wengine hata kama hamna vikosi nidhamu iwe kama hii ya watumishi wenu.

Baada ya machache hayo basi sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo. *(Makofi)*

(Saa 7:00 za mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Afya

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuwa na afya nzuri na kukutana tena mwaka huu katika baraza lako hili na kuniwezesha kutoa hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Baraza hili likae kama Kamati ya matumizi ili liweze kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/15. Aidha, naliomba Baraza lako likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na kazi za maendeleo ya wizara kwa mwaka 2015/16.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima namshukuru kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo ambayo yametuwezesha kutoa huduma bora za afya kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa uongozi wake

na maelekezo yake ambayo yamenisaidia sana kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi. Aidha, naomba nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za kiserikali katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Pia nachukua fursa hii kumpongeza kutokana na maelezo aliyoyatoa kwenye hotuba yake ambayo imeonesha jinsi serikali itakavyotekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika kwa njia moja au nyengine kutokana na mvua zilizonyesha hivi karibuni katika visiwa vya Unguja na Pemba hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Namuomba Mwenyezi Mungu awape subira kwa wale waliopoteza jamaa zao pamoja na walioharibikiwa na mali zao.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na juhudi kubwa za serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo pamoja na sekta binafsi na wadau wengine, sekta ya afya imepata mafanikio mengi kwa mwaka wa fedha unaomalizika. Pamoja na mafanikio hayo bado zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii katika kuwahudumia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuliarifu baraza lako adhimu kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 malengo ya Wizara ya Afya yatatekelezwa kwa njia ya programu ambapo sekta ya afya itakuwa na programu kuu tatu nazo ni; Programu ya Usimamizi wa Sera na Utawala, Programu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya na Programu ya Huduma za Tiba. Kwa upande wa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja nayo imepangiwa kutekeleza programu kuu mbili nazo ni; Programu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu na Programu ya Uongozi na Utawala.

Mhe Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba uniruhusu nitoe maelezo ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015.

MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, wizara ina jukumu la kuchangia mfuko mkuu wa serikali kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato vilivyomo ndani ya taasisi hii. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, wizara ilipangiwa kuchangia jumla Tsh. 124,000,000, hadi kufikia Machi, 2015, jumla ya Tsh. 108,194,500 (87%) zimekusanywa. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Afya imepangiwa kuchangia jumla Tsh. 168,738,000 katika mfuko mkuu wa serikali. Kwa upande wa mapato ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara ilipangiwa kukusanya

jumla ya Tsh. 550,000,000 hadi kufikia machi, 2015 jumla ya Tsh. 582,641,363 (106%) zimekusanywa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015 wizara ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh. 50,954,097,000 kati ya hizo Tsh. 26,597,200,000 kutoka Serikalini na Tsh. 24,356,897,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kati ya fedha kutoka Serikalini Tsh. 7,253,200,000 zimepangwa kwa kazi za kawaida, Tsh. 14,274,800,000 kwa ajili ya mishahara na maposho, Tsh.1,219,200,000 ni ruzuku na Tsh. 3,850,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2015, jumla ya Tsh. 4,049,763,501.95 ziliingizwa sawa asilimia 56 ya bajeti ya fedha za matumizi ya kawaida na Tsh. 11,370,792,819 sawa na asilimia 80 ziliingizwa kwa ajili ya mishahara na maposho. Kwa upande wa ruzuku Tsh. 471,089,581 ziliingizwa sawa na asilimia 39. Aidha, Tsh.2,367,822,000 sawa na asilimia 62, ziliingizwa kutoka Serikalini na Tsh.1,252,884,320 sawa na asilimia 5.1 kutoka kwa washirika mbali mbali kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja iliidhinishiwa jumla ya Tsh.1,478,000,000 kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia Machi, 2015 Tsh. 900,000,000 ziliingizwa sawa na asilimia 61. Aidha, jumla ya Tsh.6,804,000,000 ziliidhinishwa kwa mishahara hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Tsh. 4,936,876,650 sawa na asilimia 73 zimetumika.

MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KWA MWAKA 2014/15

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama haya yafuatayo:-

1. Kuendelea kudhibiti kiwango cha malaria na VVU/UKIMWI chini ya asilimia moja.
2. Kuongezeka kwa asilimia ya mama wajawazito wanaojifungua katika vituo vya afya kutoka asilimia 56.1 mwaka 2013 kufikia asilimia 68.3 mwaka 2014 .
3. Kukamilisha kampeni ya chanjo ya kitaifa ya Surua Rubella kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 15 ambapo kiwango cha chanjo kimefikia asilimia 96.8 ya walengwa.

4. Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kazi kwa jengo jipya la utoaji wa huduma za upasuaji wa maradhi ya mgongo na ubongo *(neurosurgical services).*

5. Kukamilika kwa ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi *(ICU)* katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

6. Kukamilika ujenzi wa majengo mapya ya maabara katika hospitali za Wete, Chake Chake na Micheweni.

7. Kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee

8. Kutiwa saini mkataba wa ujenzi wa hospitali ya Binguni

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Naibu Spika, idara hii ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma za kinga na elimu ya afya kwa jamii ili kuepukana na maradhi mbali mbali yakiwemo ya miripuko, maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Idara hii hutekeleza majukumu yake kupitia miradi mbali mbali, vitengo, timu za afya za wilaya na timu za afya za kanda.

KITENGO CHA UTOAJI WA HUDUMA ZA MACHO

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la kitengo hiki ni kupunguza upofu unaoweza kuzuilika kwa kufuata muongozo wa Dira ya 2020 (Vision 2020) kutoka 0.4% hadi kufikia 0.3%.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Kitengo cha "*Negleted Tropical Desease*" kitengo kilitoa mafunzo ya msingi ya utambuzi wa maradhi ya Trachoma kwa wafanyakazi 55 wa vituo vya Afya katika Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Mjini pamoja na hospitali za Vijiji.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya uhamasishaji pia yalitolewa kwa masheha 76 (45 Wilaya ya Mjini na 31 Wilaya ya Magharibi). Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa utambuzi wa maradhi ya macho ili waweze kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi katika shehia zao ikiwa ni pamoja na kuvitumia ipasavyo vituo vya afya.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15 kitengo pia kilifanya uchunguzi wa macho maskulini ambapo jumla ya wanafunzi 5,964 (wanaume 2,901 na wanawake 3,063). Kati ya hao 52 walionekana na matatizo mbali mbali ya macho na kupatiwa matibabu waliostahiki.

Mhe. Naibu Spika, uchunguzi wa huduma ya macho uliendelea kama kawaida katika vijiji mbali, ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 1.

KITENGO CHA LISHE

Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki kina majukumu ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini shughuli za lishe nchini. Katika kutekeleza hayo shughuli mbali mbali zinaendelea kufanywa ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya ulaji bora, kupambana na ukosefu wa vitamini na madini, pamoja na utekelezaji wa matibabu ya utapiamlo mkali hususan watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/15, Wizara kupitia kitengo hiki ilitoa matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano ambao hufanyika mara mbili kwa mwaka. Mzunguko wa pili uliofanyika mwezi wa Oktoba ulifanyika sambamba na kampeni ya kitaifa ya Surua Rubela. Asilimia ya watoto waliopewa matone ya Vitamini A katika kampeni hiyo ilifikia 98%. Aidha, asilimia ya watoto waliopewa dawa za minyoo ilifikia 104%.

Mhe. Naibu Spika, wizara ilifanya utafiti wa hali ya lishe ya watoto chini ya umri wa miaka mitano. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa hali ya udumavu wa watoto ni asilimia 24.4, uzito pungufu asilimia 13.9 na ukondefu asilimia 7.2. Mikakati inayoendelea katika kuhakisha hali ya lishe ya watoto inaimarika ni pamoja na kutoa elimu juu ya unyonyeshaji bora, kutoa matone ya *vitamin A* pamoja na kushajihisha matumizi ya chumvi yenye madini joto kwenye kaya.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo juu ya umuhimu wa kuuza chumvi iliyowekewa madini joto yalitolewa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo 200 kutoka wilaya zote za Pemba. Sambamba na hilo ugawaji wa madini joto kwa wakulima wa chumvi ulifanyika ambapo jumla ya kilo 200 zilikabidhiwa kwa wakulima hao.

KITENGO CHA AFYA YA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Maabara ya Afya ya Jamii *(PHL), Water Aid, Soap Box Collaborativ*e na SHARE kitengo kilifanya utafiti wa Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi katika vituo vinavyotoa huduma za kuzalisha. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuangalia upatikanaji wa maji, usafi na mazingira kwa ujumla na kuangalia mtazamo wa wadau juu ya masuala ya uzuiaji wa maambukizi.

Mhe. Naibu Spika, uhamasishaji wa ujenzi wa karo na vyoo vya gharama nafuu umefanyika katika Shehia 43 za Unguja na Pemba. Aidha, ujenzi wa karo za maji machafu kwa familia 16 ulifanyika. Lengo kubwa ni kuwahamasisha wananchi kudhibiti maji machafu ili kujikinga na maradhi mbali mbali ya kuharisha hasa kwa watoto, kuweka mazingira safi sambamba na kutunza vyanzo vya maji safi.

KITENGO CHA AFYA BANDARINI

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la kitengo hiki ni kuzuia uingizwaji na usafirishwaji wa maradhi pamoja na wadudu wasababishao maradhi kuingia au kutoka nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kitengo kiliendelea na kazi ya utoaji wa chanjo kwa wasafiri wa kimataifa**.** Jumla ya wasafiri 1,052 wamepatiwa chanjo hiyo ikilinganishwa na wasafiri 814 waliochanjwa mwaka 2013/14. Sambamba na hilo kitengo kilichapisha kadi za chanjo za kisasa 1,460. Katika hatua nyengine kitengo kilikagua jumla ya wasafiri 1,043,523 kupitia bandarini na uwanja wa ndege ambapo wasafiri 190 walitokea nchi zilizoathirika na ugonjwa wa Ebola na kufanyiwa ufuatiliaji wa ziada wakati wote walipokuwapo nchini. Aidha, jumla ya vyombo 1,269 vikiwemo meli kubwa 99, boti 1,085, jahazi 125 vilikaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 kitengo kiliendelea na kazi ya ukaguzi wa wageni wanaoingia nchini. Jumla wageni waliokaguliwa walikuwa 70,601. Kati yao 38,674 hawakuwa na kadi za chanjo ya homa ya manjano, ambapo wasafiri 31,718 walitokea maeneo yasiyo hatarishi na 168 walikuwa na sababu za kiafya. Wageni 41 walichanjwa hapa hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha huduma za afya bandarini na uwanja wa ndege kitengo kilitoa mafunzo kwa wafanyakazi 34 wa afya bandarini na uwanja wa ndege kuhusiana na kazi zao.

KITENGO CHA KUPAMBANA NA MARADHI YASIYOAMBUKIZA

Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki kilifanya utafiti uliolenga kupima uelewa na mitazamo ya wafanyakazi pamoja na jamii juu ya magonjwa yasiyoambukiza. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha kuwa asilimia 26.5 ya wafanyakazi waliohojiwa hawakuwahi kupata mafunzo yoyote yanayohusiana na magonjwa yasiyoambukiza. Kati ya waliowahi kupata mafunzo asilimia 30.8 waliwahi kufundishwa kuhusu saratani ya shingo ya kizazi na asilimia 34.6 walifundishwa juu ya saratani ya matiti. Aidha, ilibainika kwamba asilimia 50 ya wafanyakazi wanao uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wa kisukari na shindikizo la damu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa jamii, asilimia 73.4 ya watu waliohojiwa wanajua kama magonjwa yasiyoambukiza hayawezi kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine, wakati asilimia 15 walisema magonjwa hayo yanaweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine na asilimia 11.6 hawajui kama yanaweza kuambukizwa au la.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma za maradhi yasioambukiza zinaimarika katika ngazi za msingi, wizara imenunua na kusambaza vifaa vya kufanyia uchunguzi wa magonjwa ya kisukari, shindikizo la damu na pumu katika vituo vya afya. Kazi hii ilifuatiwa na mafunzo kwa wafanyakazi 144 kutoka katika hospitali ya Mnazi Mmoja, hospitali tatu za wilaya, hospitali nne za vijiji pamoja na vituo 37 vya ngazi ya msingi. Kufuatia kukamilika kwa mafunzo haya, wizara imeweza kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma hizo kutoka vituo vitatu hadi 26 kwa Unguja na kutoka vituo vitano hadi kufikia 19 kwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua nyengine ya kuimarisha huduma hizo, wizara ilinunua vifaa kwa ajili ya uchunguzi wa macho kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi wagonjwa wa maradhi ya kisukari na shindikizo la damu ambao mara nyingi hupata taathira hii. Ununuzi huo ulifuatiwa na mafunzo kwa wafanyakazi na baadae vifaa hivyo kusambazwa
katika vituo vya afya vikiwemo Chumbuni, Mpendae, Bumbwini Misufini, Mwera, Uzini, Donge, Fuoni na Chwaka kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni hospitali ya Wete, Micheweni na vituo vya afya vya Makangale, Konde, Pujini, Bogoa na Kojani.

KITENGO CHA UFUATILIAJI WA MWENENDO WA MARADHI

Mhe. Naibu Spika, jukumu la kitengo hiki ni kuratibu, kufuatilia miendendo ya maradhi, kutafuta yanzo na vichocheo vya maradhi pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana na maradhi pamoja na majanga mengine yanayotokea katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, katika kujitayarisha na kujikinga na ugonjwa wa Ebola wizara imekuwa ikichukuwa hatua mbali mbali katika kukabiliana na ugonjwa huu pindi ukitokea. Hatua hizo zilijumuisha kuunda kamati maalumu ya kitaifa pamoja na kamati maalumu ya ufuatiliaji ya wizara, mafunzo kwa wafanyakazi wa afya, na utoaji wa elimu ya afya kwa jamii kupitia njia tofauti zikiwemo vyombo vya habari, vipeperushi, midahalo, filamu na nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia Shirika la Afya Ulimwenguni imenunua vifaa vya kujikinga na maradhi hayo. Aidha, ufuatiliaji maalumu kwa wageni wote wanaoingia nchini kupitia viwanja vya ndege na bandarini pamoja na upulizaji wa dawa unafanyika (*disinfection*) katika maeneo ya kusubiri abiria na sehemu za mizigo.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, wizara imefanya mawasiliano na taasisi za uchunguzi wa tafiti za afya za *National Medical Research (NMR)* ya Tanzania Bara na Kenya *Medical Research (KEMR)* kuhusiana na uchunguzi wa kimaabara. Imekubalika kwamba sampuli za damu za washukiwa zitasafirishwa huko kwa

uchunguzi kwa utaratibu maalumu kama ilivyopendekezwa na Shirika la Afya Ulimwenguni. Aidha, wizara inaendelea na jitihada za kuzipandisha daraja maabara zetu za Mnazi Mmoja na Maabara ya Afya ya Jamii Pemba ili ziweze kutumika kwa uchunguzi wa awali wa maradhi haya. Aidha , maeneo ya Vitongoji kwa Pemba na Fuoni Kibondeni kwa Unguja yametengwa na kuwekwa vifaa mbali mbali kwa ajili ya matibabu ya washukiwa wa ugonjwa wa Ebola pindipo wakitokea.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wizara imeweza kupokea taarifa za kuwepo kichaa cha mbwa katika sehemu mbali mbali za Unguja. Jumla ya watu 23 waliripotiwa kutafunwa na mbwa hao kati ya hao wagonjwa wanne walitokea Wilaya ya Magharibi, 11 wilaya ya Mjini, mmoja wilaya ya Kaskazini A na saba kutoka Wilaya ya Kati. Maeneo yalioathirika zaidi ni Fuoni, Maungani, Kianga, Bomani, Mkunazini, Mwembeladu, Kwahajitumbo, Kijangwani, Hurumzi, Shangani, Nungwi, Mwera na Chuini. Kufuatia kuripotiwa kwa kesi hizo elimu ya afya ilitolewa na kupatiwa chanjo kwa wale walioathirika na kusisitizwa kumaliza sindano zote za matibabu hayo.

KITENGO CHA AFYA YA WAFANYAKAZI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya watu 6,499 waliifanyiwa uchunguzi wa afya zao. Wafanyakazi hawa walijumuisha wafanyakazi wa Hoteli, Mikahawa na Nyumba za kulala wageni (4,185), wafanyakazi wa Viwanda (117), wauza vyakula (126) na wafanyakazi wa maduka ya nyama (143). Halikadhalika, jumla ya wafanyakazi wapya wa serikali, waajiriwa na wanafunzi wanaokwenda masomoni (889) na wafanyakazi wa kampuni binafsi na mashirika ya umma (1,039) pia walifanyiwa uchunguzi huo.

Mhe. Naibu Spika, kitengo pia kiliendelea kutoa elimu ya afya kwa jamii kwa kupitia redio, hasa wafanyakazi wa vituo vya Petroli kuhusu athari na madhara yanayoweza kusabishwa na mafuta. Aidha, elimu ya afya hutolewa kwa wote wanaogunduliwa na matatizo ya uchunguzi wa afya zao.

KITENGO CHA KUPAMBANA NA MARADHI YA KICHOCHO, MINYOO NA MATENDE

Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki kinaendelea kutoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wote wanaosumbuliwa na Maradhi ya Kichocho na Minyoo. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2014, jumla ya watu 3,952 walichunguzwa, kati yao 1,646 (41%) waligunduliwa na maradhi (Unguja 1,292 na Pemba 354).

Mhe. Naibu Spika, kitengo kilifanikiwa kufanya ukaguzi katika mito na maziwa 40 katika wilaya tano za Unguja kwa lengo la kuangalia makonokono wenye uwezo wa kusambaza maradhi ya Kichocho. Baada ya ukaguzi huo maeneo yaliyobainika kuwa na makonokono yalinyunyiziwa dawa kwa ajili ya kuwaangamiza.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba maradhi ya Kichocho yanatoweka ifikapo mwaka 2016 na kupunguza maambukizo ya maradhi ya minyoo, ulishaji wa dawa kwa lengo la kutibu na kupunguza maambukizo mapya ya maradhi haya ulifanyika. Jumla ya walengwa 1,093,004 walitarajiwa kula dawa, kati yao watu 915,954 (84%) walipatiwa dawa hizo.

Mhe. Naibu Spika, katika kuelimisha jamii juu ya mabadiliko ya tabia kitengo kimetoa mafunzo ya kurekebisha tabia katika shehia 30 (15 za Unguja na 15 za Pemba) pamoja na madrasa zote zilizomo katika shehia hizo. Aidha, jumla ya mafulio 60 (30 kwa Unguja na 30 kwa Pemba) yamejengwa kwenye maeneo yenye maambukizi ya maradhi ya Kichocho.

Huduma za Afya Wilayani

Mhe. Naibu Spika, huduma za afya wilayani zinatolewa kupitia timu za afya za wilaya zilizopo Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 timu za afya za wilaya zilipata mafanikio makubwa, mafanikio hayo ni pamoja na kuchimba kisima kwa ajili ya kituo cha afya cha Mpendae, kuipatia umeme nyumba ya madaktari Tumbatu Gomani na kituo cha afya cha Jendele, Machui na Ukunjwi sambamba na ulipaji wa madeni ya umeme kwa vituo vya afya vya Kiboje, Uroa, Mwera, Uzi, Tunguu na Pongwe pwani.

Mhe. Naibu Spika, shughuli nyengine zilizofanyika ni uwekaji wa matanki ya maji katika nyumba za madaktari Tumbatu, kituo cha afya cha Miwani na Kojani. Wakati huo huo matengenezo madogo madogo yalifanyika kwa nyumba za madaktari Kojani, kituo cha afya cha Dunga, Jendele, Cheju, Pandani, Mokongeni, Junguni, Tundauwa, Shungi, Mgelema, Ziwani, Mvumoni na Kinyasini kwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikiwa wananchi, timu za afya za wilaya zinaendelea kutoa huduma za mkoba *'outreach services'* katika vijiji vilivyo mbali na vituo vya afya. Lengo la utoaji wa huduma hizi ni kugundua na kutoa matibabu ya maradhi yanayowakabili wananchi wa maeneo hayo. Aidha, rufaa ilitolewa kwa wale waliookenekana na dalili za saratani ya matiti na ile ya shingo ya kizazi.

Mhe. Naibu Spika, elimu ya afya kwa jamii imeendelea kutolewa dhidi ya kinga ya maradhi mbali mbali kuhusiana na utumiaji wa huduma za afya ya macho, kinywa na meno, umuhimu wa chanjo ya pepopunda kwa wanawake wenye umri wa kuzaa, kampeni ya Surua Rubella, pamoja na uhamasishaji jamii katika kuweka usafi wa mwili na mazingira. Elimu ya afya ilitolewa katika skuli za Mahonda, Kinduni na Kitope na jumla ya wanafunzi 183 walihudumiwa.

Mhe. Naibu Spika, uchunguzi wa maradhi mbali mbali ulifanyika katika siku za maadhimisho ya siku za afya za kijiji, katika maadhimisho hayo, jumla ya watu 1,232 walichunguzwa maradhi ya sukari na sindikizo la damu na waliobainika walipatiwa matibabu.

Mhe. Naibu Spika,**,** uchunguzi wa masikio, pua na koo katika skuli tano na uchunguzi wa kinywa katika skuli 10 za maandalizi na msingi ulifanyika. Jumla ya wanafunzi 1,341 walichunguzwa masikio, pua na koo, kati yao 352 walitibiwa kwa mujibu wa matatizo yao. Pia wanafunzi 2,106 wamefanyiwa uchunguzi wa kinywa kati yao 487 waligunduliwa na matatizo mbali mbali na kupatiwa matibabu.

Mhe. Naibu Spika, wanafunzi 346 wamepatiwa elimu ya afya juu ya maradhi ya kuharisha na UKIMWI. Aidha wanafunzi 150 walifanyiwa uchunguzi wa meno na macho, kati yao 12 waligundulika kuwa na matatizo hayo, walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya matibabu.

IDARA YA TIBA

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Tiba inasimamia huduma zinazotolewa katika hospitali ya Chake Chake, Abdalla Mzee, Wete, Micheweni, Vitongoji, Makunduchi na Kivunge. Idara hii pia inasimamia Mpango wa Damu Salama, huduma za uchunguzi pamoja na usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi. Taarifa za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na wazazi waliojifungua zinaonekana katika Kiambatisho namba 2 na 3.

Mhe. Naibu Spika, huduma za matibabu katika kliniki maalum zimeendelea kutolewa katika klinki za kisukari, shindikizo la damu, macho, pua, masikio na koo, kifua kikuu pamoja na magonjwa ya wanawake. Ufafanuzi wa taarifa za wagonjwa unapatikana katika Kiambatisho namba 4.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, jumla ya wagonjwa 206 walifanyiwa uhakiki na Bodi ya Madaktari kati ya hao wagonjwa 156 walithibitishwa kusafirishwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi. Jumla ya Tshs. 3,231,526,142.40 zilitumika kwa ajili ya usafirishaji na matibabu ya wagonjwa

hao, idadi hii ya fedha ni kubwa ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 ambazo zilikuwa ni Tsh. 800,000,000.

Mhe. Naibu Spika, damu salama ni muhimu katika kuhuisha afya za wananchi. Mpango wa Damu Salama una lengo la kuhakikisha upatikanaji wa damu salama na ya kutosha kutoka kwa wachangiaji wa hiari. Damu salama inayokusanywa katika hurahisisha upatikanaji wa damu katika hospitali zote zinazotoa tiba ya damu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha July 2014 hadi Machi 2015**,** mpango huu umefanikiwa kukusanya jumla ya uniti za damu 5,931 (59.3%), lengo la mwaka lilikuwa ni kukusanya uniti za damu **10,000** kutoka kwa wachangiaji wa hiari. Kiwango hicho cha makusanyo hayo yamechangiwa na uhamasishaji uliofanywa katika vikundi mbali mbali vya jamii vikiwemo vilabu vya mipira na sanaa, skuli mbalimbali, vyuo, mikusanyiko ya kidini na vikosi vya ulinzi. Hadi sasa kuna vilabu vya uchangiaji damu "Donor clubs" vya kijamii vipatavyo 70 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kumbukumbu za wataalamu wa huduma za uchunguzi zimeanza kukusanywa na kurikodiwa katika ngazi ya wilaya. Aidha, mafunzo kwa wataalamu wa maabara juu ya ubora wa vipimo wa kufikia viwango *"Quality Management System"* yametolewa kwa wataalamu **25** na mafunzo ya ufuatiliaji wa maradhi yanayopaswa kuchukuliwa hatua za haraka *"integrated disease surveillance and response"* yametolewa kwa wataalamu wa maabara **27** Unguja na Pemba.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Naibu Spika, jukumu muhimu la Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kutoa huduma za uchunguzi, rufaa na matibabu kwa wagonjwa na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa kada mbali mbali za afya wanaotoka katika vyuo vya ndani na nje ya nchi, idara hii inajumuisha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Hospitali ya wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu.

Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Naibu Spika, ili kukidhi mahitaji ya wataalamu mbali mbali katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa, wizara imewapeleka masomoni madaktari wawili kwa shahada ya tatu na madaktari saba kwa ajili ya masomo ya shahada ya pili (*specialization*), ili wawe madaktari bingwa katika mionzi (*radiology*), matibabu ya macho, mifupa, meno, pua, masikio na koo, maradhi ya akili na upasuaji wa matatizo ya watoto. Ni mategemeo yetu kuwa kurudi kwa wataalamu hawa

kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha huduma katika hospitali hii na pia kupunguzia mzigo serikali kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma zinakuwa za kisasa zaidi vifaa vya mtambo na mfumo wa kusambazia oxygen, hewa na 'vacuum' katika wodi ya wagonjwa mahututi, chumba cha upasuaji, chumba cha huduma ya dharura na wodi ya wazazi tayari vimeshafungwa na kuanza kutumika.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza azma ya hospitali hii kuwa na hadhi ya kujitegemea, hospitali ya Mnazi Mmoja imepatiwa vifaa vipya kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi ya mfumo wa chakula *(gastro-intestinal system)* kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, vifaa hivi vinatuwezesha kugundua na kutibu maradhi ya vidonda vya tumbo, uvimbe, saratani za mfumo wa chakula, uchunguzi wa kifua kikuu, upasuaji na matibabu ya meno. Vile vile ukarabati wa wodi ya mifupa, wodi ya ICU yenye vitanda 8 pamoja na kuwekewa vifaa vya kisasa umekamilika na wodi hiyo tayari imeshaanza kazi.

Mhe. Naibu Spika, Takwimu za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa, kliniki maalumu na waliojifungua katika Hospitali ya Mwembeladu na Mnazi Mmoja zinaonekana katika Kiambatisho namba 5, 6 na 7.

Hospitali ya Wagonjwa wa Akili - Kidongo Chekundu

Mhe. Naibu Spika, Hospitali hii ni hospitali pekee ya rufaa kwa wagonjwa wa akili hapa Zanzibar. Kuanzia Julai, 2014 hadi Machi, 2015, mahudhurio ya wagonjwa wa nje yalikuwa ni 7,678 (wanaume 3,684 na wanawake 3,994). Aidha, wagonjwa waliolazwa walikuwa ni 631 kati yao wanaume 350 wanawake 281, wagonjwa watatu wamefariki.

Mhe. Naibu Spika, huduma za afya ya akili zimeanza kutoa matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya husan kwa wale wanaojidunga *heroin* kwa kutumia dawa ya *methedone*, tokea tarehe 2/2/2015. Hadi kufikia tarehe 11/5/2015 jumla ya vijana 78 (wavulana 68 na wasichana 10) wanaendelea na huduma hiyo ikiwa ni mwendelezo wa Serikali kuwanusuru vijana kurejesha nguvukazi ya taifa.

OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba, vitendanishi (*reagents*) pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya dawa. Katika kulifikia lengo hili, Ofisi hii imepewa dhamana ya kufanya tathmini ya dawa (*quantification*) pamoja na kuratibu ununuzi wa dawa na vifaa, kufanya ukaguzi kwenye hospitali na vituo vyote vya afya vya serikali kuhakikisha utunzaji bora na utumiaji sahihi wa dawa. Pia inajukumu la kusimamia sera ya dawa nchini *(National Medicine Policy).*

Mhe. Naibu Spika, wizara inaendelea kutumia mfuko maalum wa dawa *(Essential Medicine Account),* ambapo ununuzi wa dawa unatumia utaratibu wa Mkataba maalum yaani '*Framework Contract'*.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliendelea kununua dawa na vifaa tiba kwa kutumia fedha za Serikali, pamoja na Washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa Serikali jumla ya Tsh. 2,800,000,000 zilitengwa, hadi kufikia Machi 2015, TSh.1,368,325,561 (49%) zimepatikana. Pia Wizara imepokea dawa na vifaa tiba kutoka kwa Washirika wa Maendeleo vyenye thamani ya Tsh.2,603,135,438. Kiambatisho namba 8. kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha dawa zinasimamiwa na kufanyiwa ukaguzi unaofaa wizara imeweza kupokea pikipiki kumi kwa ufadhili wa JSI, ambazo zimegharimu jumla ya TSh. 44,940,000/= kwa ajili ya ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya. Pikipiki hizo tayari wamekabidhiwa maafisa wasimamizi wa wilaya wa dawa *(District Material Managers)* wote Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mfamasia Mkuu inaendelea na mchakato wa kuanzisha kitengo cha uratibu wa usimamizi wa dawa *(Logistic Management Unit).* Kitengo hiki kitaangalia na kusimamia mwenendo mzima wa dawa ikiwemo ukusanyaji wa taarifa za dawa *(End Use Verification)* pamoja na kuanzishwa mfumo wa kielektroniki wa kuweka kumbukumbu pamoja na uagizaji wa dawa kwa Hospitali na Vituo vya Afya *(Electronic Logistic Management Information System - eLMIS).* Mfumo huu utasaidia upatikanaji wa dawa taarifa za matumizi pamoja na kupunguza utumiaji mbaya wa dawa.

IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Bohari Kuu ya Dawa ina jukumu la kupokea, kutunza na kusambaza dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vyote vya afya vya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha huduma za usambazaji dawa na vifaa tiba idara inaendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji wa dawa kwa njia ya kielektroniki hatua kwa hatua. Jumla ya watendaji 141 wamepatiwa mafunzo hayo na yanaendelea kutolewa kwa mujibu wa mahitaji, upatikanaji wa dawa muhimu uliimarika kutoka asilimia 50 mwaka 2012/2013 hadi asilimia 63 katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, Bohari Kuu ya Dawa inaendelea na mchakato wa kuandaa rasimu ya sheria itakayoifanya idara hii kuwa ni yenye kujitegemea *(Semi-Autonomous).*

MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa huduma za kitaalamu na kisayansi kwa kuangalia ubora na usalama wa vyakula na dawa, udhibiti wa kemikali na usalama wa mazingira, kufanya uchunguzi wa vinasaba na vielelezo vinavyowasilishwa kutoka taasisi za serikali na watu binafsi vikiwemo vile vinavyohusiana na makosa ya jinai. Aidha, Maabara inajukumu la kufanya tafiti zinazohusiana na kazi za maabara.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Maabara imefanya uchunguzi wa vielelezo 590, kama inavyoonekana kwenye kiambatisho namba 9.

Mhe. Naibu Spika, uandaaji wa michoro na gharama za ukarabati na utanuzi wa majengo mawili ya maabara umekamilika. Aidha, matayarisho ya kupata eneo la ujenzi wa maabara kwa upande wa Pemba yanaendelea. Katika hatua nyengine Kanuni ya udhibiti wa kemikali imeshakamilika na inatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara ina majukumu ya kutayarisha Sera, miongozo na mipango mikuu ya wizara pamoja na kusimamia na kutathimini utekelezaji wake ikiwemo kufuatilia ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa za afya.

Mhe. Naibu Spika, matayarisho ya uanzishwaji wa mfuko wa bima ya afya ikiwa ni miongoni mwa vyanzo mbadala umefikia hatua nzuri baada ya mshauri muelekezi kuanza kazi ya kufanya tathmini ya mfuko huo. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kufanya utafiti utakaotumia takwimu ya idadi ya watu pamoja na hali ya wananchi kimapato *(Actuarial Study)*, utafiti huo utasaidia wizara pamoja na serikali kufanya maamuzi sahihi ya uendeshaji mzima wa mfuko wa Bima ya Afya. Ripoti ya awali inategemewa kuwasilishwa serikalini hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa wizara umetayarishwa na kukamilika, kabla ya kuanza kazi hii, tathmini ya kina ya kuangalia hali halisi ya ufuatiliaji na tathmini ilivyo ndani ya wizara ilifanywa, Ripoti ya tathmini hiyo imekamilika na ndiyo iliyotumika katika kutayarisha mpango huu. Mpango huu utaisaidia wizara kusimamia utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitano.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2015 Idara kupitia kamati ya kusimamia maadili ya tafiti za afya imefanikiwa kuzipitia tafiti 10 na zote zilipewa maelekezo ya kuziimarisha zaidi ili ziendane na maadili hayo.

Mhe. Naibu Spika, azma kuu ya lengo la wizara ni kuzidi kufikisha taarifa za afya kwa jamii ili waweze kuelewa mwenendo halisi wa hali ya afya na kinga dhidi ya maradhi mbali mbali. Katika kulisimamia hili wizara imeunda timu ya wataalamu ya kusimamia utoaji wa taarifa za afya kwa jamii kupitia kijarida maalumu ambacho kitatayarishwa kwa kila robo mwaka. Tayari usajili wa kuchapisha kijarida hicho umefanyika kupitia Idara ya Habari Maelezo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina dhima ya kusimamia uwajibikaji kazini, haki, maslahi, nidhamu, stahiki za wafanyakazi pamoja na kujenga uwezo wa nguvu kazi ya afya ili kuongeza ufanisi. Aidha, idara hii inasimamia masuala ya usafiri, utunzaji kumbukumbu za wafanyakazi na miundombinu yote iliyomo ndani ya wizara.

Nguvu kazi ya Sekta ya Afya

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla wafanyakazi wote wanaoendelea na masomo hadi sasa ni 343 ambapo jumla ya wafanyakazi 62 wamerudi kutoka masomoni na kupangiwa kazi katika sehemu tofauti. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Mei, 2015, jumla ya wafanyakazi 92 wa kada mbali mbali wamepelekwa masomoni ndani na nje ya nchi.

Kiambatisho namba 10 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kimeanzisha masomo ya kujiendeleza kwa wafanyakazi wenye cheti kwa muda mrefu na hawakupata nafasi ya kujiendeleza kielimu katika fani zao. Hivi sasa jumla ya wanafunzi 192 wanaendelea na masomo yao mwaka wa kwanza na wa pili, kati yao wanafunzi 11 wamedhaminiwa na *AMREF*.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hicho, Wizara pia imeajiri wafanyakazi 56 wa kada tofauti. Jumla ya wafanyakazi 153 (130 Unguja na 23 Pemba) wamestaafu kwa mujibu wa Sheria. Vilevile wafanyakazi 9 wamefariki dunia (5 Unguja na 4 Pemba).

Mhe. Naibu Spika, ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya na nyumba za wafanyakazi umefanyika katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Maeneo hayo ni Fundo, Makangale, Wesha, Ukutini na Mtangani kwa upande wa Pemba na Sebleni, Uzini, Kombeni, Magogoni, Selem, Chumbuni, Unguja Ukuu na Muyuni kwa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuliarifu Baraza hili kwamba wizara kwa kushirikiana na asasi isiyo ya kiserikali ya *"MILELE ZANZIBAR FOUNDATION"* wizara

imeanza ujenzi kwenye vituo vya afya vinne ambavyo ni Kinuni, Kiongwe, Bumbwi Sudi na Ukongoroni.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2012, kanuni mbali mbali zimetengenezwa zikiwa ni pamoja na viwango vya usafi na afya ya mazingira, Umalizaji wa Maradhi ya Malaria, udhibiti wa matumizi ya Tumbaku na kanuni nyenginezo zinazofanana na hizo.

TAASISI MAALUMU

Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya
Mhe. Naibu Spika, Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya Taaluma za Sayansi za Afya katika fani mbali mbali. Hivi sasa chuo kina idadi ya wanafunzi 872 wanaoendelea na masomo yao wakiwemo uuguzi (198), Afya ya Mazingira (127), Ufundi sanifu wa Maabara (128), Famasia (123), Afya ya Kinywa na Meno (44), Afisa Tabibu (213), Ufundi wa Vifaa Tiba (18) na *Fiziotherapia* (21).

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015 mwezi wa Septemba Chuo kimechukua wanafunzi wapya 327. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi 2015, Chuo kimetoa wahitimu 281 katika fani mbalimbali za Uuguzi (68), Waganga Wasaidizi (51), Afya ya Mazingira (49), Famasia (48), Afya ya Kinywa na Meno (13), Maabara (38) na Ufundi wa Vifaa Tiba (13).

Mhe. Naibu Spika, katika kukijengea uwezo wa kitaaluma walimu wanne wamemaliza masomo ya muda mrefu, kati yao watatu wamehitimu Shahada ya Uzamili na mmoja amehitimu Shahada ya kwanza ya uuguzi. Aidha, walimu na wafanyakazi 21 wanaendelea na masomo yao (Shahada ya Uzamivu mmoja, Shahada ya Uzamili saba na shahada ya kwanza 13).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, chuo kimeweza kutayarisha mpango wa kujiendesha *(Business Plan)* ambapo utasaidia chuo kuongeza mapato yake ili kiweze kujiendesha wenyewe.

Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi
Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza Sheria Nambari 2 ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Bodi ilikagua jumla ya maeneo 1,304 ya biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Katika ukaguzi huo hatua mbali mbali zilichukuliwa kwa waliobainika na kasoro zikiwemo kupewa elimu ya usajili wa biashara zao, kupewa muda wa kuweka bidhaa katika mpangilio mzuri na kusafisha maeneo yao ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, mbali na kufanya ukaguzi Bodi pia ilisajili jumla ya maeneo 1,151 ya biashara za chakula, dawa na vipodozi. Vile vile bidhaa moja ya dawa na

bidhaa 63 za chakula zimesajiliwa. Pia jumla ya bidhaa 100 za wajasiriamali na vifaa tiba 25 zilitambuliwa. Aidha, Bodi iliweza kuwasajili waingizaji chakula *(Food Importers)* 68, wasafirishaji chakula *(Food Exporter)* 11, wafamasia watano na wafamasia wasaidizi *(Pharmaceutical Technicians)* 49.

Mhe. Naibu Spika, katika uchunguzi wa kimaabara sampuli 888 zikiwemo 792 za chakula, 4 za dawa, 43 za vipodozi na 49 za dawa za mitishamba zilichunguzwa. Katika uchunguzi huo ni sampuli 1 ya chakula ndio ilionekana haifai kwa matumizi ya binadamu na sampuli zote za dawa, vipodozi na dawa za mitishamba zilionekana zinafaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya tani 88.9 zikiwemo tani 84.9 za bidhaa za chakula, tani nne za bidhaa za Dawa na Vipodozi zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu ambazo zilikamatwa wakati wa ukaguzi ziliteketezwa, na tani 25 za bidhaa za chakula ambazo hazifai kwa matumizi ya binaadamu zilirejeshwa zilikotoka. Halikadhalika jumla ya tani 103 za chakula na tani 1.5 za vipodozi zilizoingia maji ya chumvi, tani moja ya dawa zilizoisha muda wa matumizi zimekamatwa na kusubiri hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2014/2015, kuwa bodi itamalizia ujenzi wa ofisi yake, napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza hili kwamba ujenzi huu umeshakamilika na tayari wafanyakazi wameshahamia katika jengo hilo jipya.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala *(Traditional and Alternative Medicine Council)* ni chombo kilichoundwa chini ya sheria No.8 ya mwaka 2008, na linajukumu la kisheria kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa tiba asili na tiba mbadala.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya waganga 205 ambao wameweza kutimiza masharti yaliowekwa ikiwa ni pamoja na kumiliki sehemu maalumu ya kutoa huduma kwa wagonjwa wamesajiliwa. Sambamba na hilo, maduka 40 ya dawa za asili, kliniki 11 (Unguja 9 na Pemba 2) na wasaidizi waganga 58 wamesajiliwa.

Mhe. Naibu Spika, imebainika kuwepo kwa ongezeko kubwa la matangazo yanayohusu tiba asili ambayo yanakiuka taratibu zilizomo katika sheria ya baraza la tiba asili na tiba mbadala. Kwa mintarafu hii, wizara inaendelea kuzuia na kupiga marufuku matangazo yote ambayo hayafuati sheria na taratibu zilizowekwa na baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukuwa fursa hii, kuwaomba wananchi kutoendelea kuuza dawa hizo katika maeneo yasiyoruhusiwa kama vile misikitini,

barabarani pamoja na sehemu zote ambazo hazikubaliki kuuza dawa hizo. Hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote wanaoenda kinyume na agizo hili.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi
Mhe. Naibu Spika, Bodi hii ina jukumu la kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa hospital na vituo vya afya vya binafsi, kukagua na kuzipa maelekezo ya utendaji yanayostahiki. Aidha, kusimamisha utoaji wa huduma kwa kituo husika pale vigezo na miongozo inapokiukwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa kazi za Bodi takribani hospitali 40 zimekaguliwa kwa kipindi hiki na jumla ya hospitali nane zilipewa onyo kwa utoaji huduma kinyume na sheria na miongozo ya uendeshaji wa hospitali za binafsi na kwa hivi sasa kuna jumla ya hospitali na vituo vya afya binafsi 68 Unguja na Pemba vinavyotambuliwa.

MIRADI YA MAENDELEO

Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar
Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Kumaliza Malaria Zanzibar inaendelea kutekeleza mikakati ya kumaliza malaria kama inayoshauriwa na Shirika la Afya Ulimwenguni. Mikakati hiyo ni pamoja na usambazaji na ushajihishaji wa matumizi sahihi ya vyandarua, ufukizaji wa dawa za kuulia mbu majumbani, uchunguzi na tiba ya wagonjwa wa malaria, ufuatiliaji wa wagonjwa katika ngazi ya shehia na ufuatiliaji wa tabia na wingi wa mbu wanaoeneza Malaria katika maeneo yote ya hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ugonjwa wa malaria bado unaendelea kupungua kwenye visiwa hivi kutokana na kutekeleza mikakati hiyo. Takwimu zinaonesha kuwa bado yapo maeneo ambayo taarifa za ugonjwa huu zimekuwa zinajirudiarudia kila ifikapo wakati wa mvua za masika na vuli. Wilaya zote zimeendelea kuonyesha kuwepo kwa ugonjwa huu isipokuwa Wilaya ya Mjini. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba, katika Wilaya za Micheweni na Wete taarifa za wagonjwa wa malaria zimekuwa zikijirudia mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, programu ya kumaliza maradhi ya malaria imeanzisha mradi wa kuangamiza viluilui katika visiwa vya Uzi kwa Unguja na Kisiwa Panza kwa Pemba katika hatua za majaribio. Mnamo mwezi wa Julai, 2014 kabla ya kuanzishwa kazi hii kituo cha afya Uzi kiliripoti wagonjwa 51 na Kisiwa Panza wagonjwa saba. Baada ya kazi hii kuanza mwezi wa Agosti 2014, hadi kufikia mwezi Machi 2015 hakuna mgonjwa yeyote aliyeripotiwa kutoka vituo hivi vya afya.

Mhe. Naibu Spika, upatikanaji na matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa si wa kuridhisha. Programu imeanzisha utaratibu mpya wa kugawa vyandarua kwa mpango endelevu. Ndani ya utaratibu huu vyandarua vitaendelea kugawiwa kwa familia zenye mahitaji kwa kila leo badala ya kusubiri hadi baada ya miaka mitatu kama utaratibu wa zamani ulivyokuwa ukitekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi 2015, jumla ya vyandarua 114,394 sawa na asilimia 51 ya makisio ya mwaka unaomaliza vimegawiwa kwa wananchi ambao wamekidhi sifa na vigezo vilivyowekwa.

Mhe. Naibu Spika, mwezi Februari mwaka 2015, kazi ya upigaji dawa majumbani iliingia kwenye mzunguko wake wa 12 tokea kazi hii ilipoanza mwaka 2006 hapa Zanzibar. Upigaji huu wa dawa ya majumbani ni kwa maeneo maalumu ya wilaya za Magharibi, Kati, Kusini, Wete, Kaskazini A, Kaskazini B na Micheweni. Katika zoezi hili la upigaji dawa mwaka 2014, jumla ya nyumba 70,368 zililengwa kupigwa dawa katika wilaya 9 za Unguja na Pemba. Jumla ya nyumba zilizopigwa dawa ni 66,497 sawa na asilimia 94.5 ya nyumba zote zilizolengwa.

Mhe. Naibu Spika, katika zoezi hilo nyumba 3,868 hazikuweza kupigwa dawa kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo; kuwepo na mgonjwa mahututi katika nyumba, nyumba kufungwa, kukataa bila ya sababu za msingi na kuwepo kwa mzazi aliyejifungua chini ya wiki moja.

Mhe. Naibu Spika, programu inaendelea na uchunguzi wa vimelea vya malaria katika kazi zake za kila siku. Jumla ya watu 172,972 walichunguzwa vimelea vya malaria ambapo watu 1,648 (0.9%) waligundulika kuwa na vimelea hivyo. Kati ya watu wote waliochunguzwa, 5,086 walikuwa ni watoto chini ya umri wa miaka tano na waliokutwa na vimelea vya malaria ni 177 (0.1%). Wagonjwa hawa walichunguzwa kwa njia ya darubini na njia ya uchunguzi wa haraka - (*mRDT*) ambazo ndizo zinazopendekezwa kwa kuchunguza malaria.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wana uwezo wa kuhamasisha jamii kwenye mpango wa kumaliza malaria, hivyo suala la uhamasishaji jamii linafaa kupewa kipaumbele cha hali ya juu ili kuhakikisha lengo la asilimia 100 linafikiwa

Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha afya ya mama na watoto kwa kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi, na vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine kubwa ambalo husaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi ni matumizi ya njia bora ya uzazi wa mpango na salama.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014 kiwango cha kinamama waliojifungulia hospitali kimefikia asilimia 68.3 ukilinganisha na asilimia 56.6 mwaka 2013. Natoa wito kwa mama wajawazito wote kuendelea na mwamko huo ili kuepusha matatizo yanayoweza kutokea kabla, wakati, au baada ya kujifungua na hatimae kusababisha vifo vya uzazi. Aidha, nachukua fursa hii kuwaomba wananchi kuendelea kujifungua katika vituo vya afya kwa wakati. Mbali na mambo hayo niliyoyataja hapo juu suala la kufika kliniki mapema wakati wa ujauzito husaidia sana kupunguza vifo vya mama wajawazito.

Mhe. Naibu Spika, ili kuwakinga na maradhi ya UKIMWI watoto waliozaliwa na mama wenye Virusi vya UKIMWI huduma maalumu hutolewa kwa kinamama hao ili kuwanusuru watoto watakaozaliwa wasipate maambukizi. Kwa mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya mama wajawazito 33,202 walichunguzwa VVU katika kliniki. Kati yao kinamama 73 waligunduliwa na VVU.

Mhe. Naibu Spika, chanjo za watoto ni muhimu sana katika maendeleo ya ukuaji wa mtoto. Huduma ziliendelea kama kawaida, ambapo chanjo zilendelea kutolewa katika vituo vyote vya afya ya uzazi na mtoto. Kwa mwaka 2014 kiwango cha chanjo kitaifa kimeendelea kuwa zaidi ya asilimia 90.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2014/15, wizara ilianzisha chanjo ya pili ya surua hapa nchini. Lengo la kuanzisha chanjo hii ni kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa huu wa surua na kutokomeza ugonjwa wa surua ifikapo mwaka 2020. Aidha, mtakumbuka kwamba mnamo mwezi wa Oktoba, 2014, kulikuwa na kampeni ya kitaifa ya chanjo ya Surua Rubella. Kampeni hii ilihusisha watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 ambao walichanjwa kwa zaidi ya asilimia 96 chanjo ya Surua Rubella na zaidi ya asilimia 100 kwa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo. Takwimu za chanjo zimeainishwa kwenye kiambatisho namba 11.

Mhe. Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba watoto wachanga wanapatiwa huduma wanazostahiki mafunzo ya siku sita juu ya utoaji wa huduma za dharura kwa watoto wachanga yamefanyika kwa watoa huduma 120 wa afya kutoka vituo vya afya mbali mbali (60 Unguja na 60 Pemba). Aidha, tathmini ya ufuatiliaji wa upatikanaji na utoaji wa huduma kwa watoto wachanga imefanyika kwa kushirikiana na mshauri muelekezi kutoka Shirika la Kuhudumia Watoto Ulimwenguni.

Mradi Shirikishi wa Maradhi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma

Mhe. Naibu Spika, mradi huu una lengo la kupambana na maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma ambapo unahusisha huduma ya ushauri nasaha, uchunguzi

na kutoa tiba kwa wagonjwa wanaohudhuria kliniki na kutoa huduma za wagonjwa wa UKIMWI majumbani.

Mhe. Naibu Spika, huduma za ushauri, nasaha na upimaji wa VVU inatolewa katika vituo 91 (Unguja 58 na Pemba 33). Kwa kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, jumla ya watu 60,638 walichunguzwa (wanawake 29,896 na wanaume 30,742), Kati yao watu 740 (1.2 %) waligundulika kuwa na VVU, wanaume ni 330 (44.6%) na wanawake 410 (55.4%).

Mhe. Naibu Spika, tathmini kwa mama wajawazito wanaohudhuria kliniki ili kujua kiwango cha maambukizo ya VVU, kaswende, homa ya ini "B" na homa ya ini "C" imefanyika. Jumla ya wajawazito 6,367 kati yao asilimia 39 Pemba na asilimia 61 kwa Unguja wameshiriki katika tathmini hiyo. Matokeo ya tathmini hii ilionesha kwamba wajawazito 39 (0.6%) wameambukizwa Virusi vya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, katika kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wanaoishi na VVU na UKIMWI, jumla ya kliniki 11 zinatoa huduma hii (7 Unguja, 4 Pemba). Kuanzia Julai, 2014 hadi kufikia Machi, 2015, jumla ya wagonjwa 7,820 walikuwa tayari wameshasajiliwa kwenye kliniki hizo. Miongoni mwao wagonjwa 5,375 (68.7%) walianzishiwa dawa za *ARVs*. Waliobaki kwenye dawa kufikia Machi, 2015 ni wagonjwa 3,587 na wagonjwa 1,788 (33.3%) wamekimbia kuchukuwa dawa.

Mhe. Naibu Spika, uchunguzi wa maradhi ya ugonjwa wa ukoma majumbani ulifanyika katika Shehia 15 za Wilaya ya Kusini ambapo ugonjwa huu umeenea. Jumla ya nyumba 425 zilipitiwa na watu 2,275 walichunguzwa. Kati yao watu 215 waligunduliwa na maradhi ya ngozi na watu 40 waligundulika na maradhi ya ukoma. Katika hatua nyengine watu 390 (202 Unguja na 188 Pemba) waligundulika na Kifua Kikuu, kati yao 162 kwa njia ya makohozi (*smear positive*), 91 njia ya *x-ray* (*smear negative*), 56 *TB* ya nje ya mapafu na 81 waliorejewa na Kifua Kikuu.

Mradi wa Kustawisha Siha za Wazanzibari

Mhe. Naibu Spika, utoaji wa elimu ya afya ni moja kati ya mikakati inayoendeleza jamii ili kujua, kuelewa na kufahamu yale yote ambayo ni muhimu katika kuimarisha afya bora na kujikinga na maradhi. Lengo la mradi huu ni kutoa taaluma hiyo kwa jamii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali pamoja na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Afya ya Jamii, jumla ya Kamati Kiongozi za Shehia 72 zimeundwa kati ya hizo kamati (63 Unguja na 9 Pemba). Kati ya hizo Kamati 36 za Wilaya ya Magharibi, Kaskazini 'A' na Mkoani

zimeshapata mafunzo ya utekelezaji wake. Aidha, wafanyakazi 34 wa vituo vya afya vya Wilaya ya Magharibi na Mkoani wameshapatiwa mafunzo juu ya uanzishwaji wa kamati Kiongozi za Afya za Shehia na jinsi ya kushirikiana nazo. Mafunzo mengine yametolewa kwa madiwani na wadau 181 wa Wilaya zote.

Mhe. Naibu Spika, elimu ya afya imetolewa katika skuli mbali mbali, kazi hii ilifanywa katika skuli 13 kwa walimu na wanafunzi juu ya umuhimu wa chanjo, ugonjwa wa kisukari na uhifadhi wa chakula kwa wauzaji chakula katika maskuli. Aidha, jumla ya skuli 177 zimepatiwa mafunzo ya elimu kuhusu stadi za maisha pamoja na elimu ya afya juu ya umuhimu wa unyonyeshaji, ugonjwa wa kichocho na matende, umuhimu wa chanjo, na uhifadhi wa taka imetolewa katika maeneo ya Shehia mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya vipindi 46 vya elimu ya afya vya redio vilirushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar *ZBC* (Redio), *Zenj FM* na Redio NURU. Vipindi hivyo vilihusisha kampeni ya chanjo, kichaa cha mbwa, dawa za kulevya, tahadhari ya mvua, maradhi ya kuharisha, ukoma, kifafa, kichocho, umuhimu wa afya ya uzazi, mabadiliko ya tabia na athari za ulawiti, lishe na majanga ya mtoto kwa mtoto na watu wazima. Elimu pia ilitolewa juu ya umuhimu wa kutambua na kujikinga na maradhi ya *Ebola* na wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama.

Mhe. Naibu Spika, vipindi 39 vimerushwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar *ZBC (TV*) vinavyohusu maradhi kama vile macho, meno, kisukari, homa kwa watoto, maradhi ya *Ebola*, ulishaji wa dawa za minyoo na kichocho, kampeni ya chanjo dhidi ya Surua Rubella, afya ya akili, sindikizo la damu na saratani ya kizazi vimetolewa kwa njia ya televisheni.

Mhe. Naibu Spika, chumba cha kurushia matangazo kwa ajili ya Redio ya Afya *FM* kimetengenezwa. Aidha, vifaa vitakavyotumika kurushia matangazo ya redio hiyo ikiwemo *"Professional moving camera 5D, Editional machine, Conses, flash, Binocular, memory card heavy duty, Professional conirocoder, tripod delux camera stand, Delux back pack na Delux hard cases*" vimenunuliwa.

Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja Kuwa ya Rufaa

Mhe. Naibu Spika, azma ya serikali ya kuipandisha hadhi hospitali hii kuwa ya rufaa kwa Zanzibar, ni kutoa huduma zitakazokwenda sambamba na mpango mkakati wa hospitali hii. Huduma hizo ni pamoja na kuongeza miundombinu, wataalamu, kuimarisha huduma za uchunguzi, huduma za kitalaamu za upasuaji wa maradhi ya mgongo na ubongo (*neurosurgical services*), kuanzisha huduma za maradhi ya figo (*Dialysis*) na huduma za matibabu ya kensa.

Mhe. Naibu Spika, jengo la huduma za upasuaji wa maradhi ya mgongo na ubongo *(neurosurgical services*) limeshakamilika na tayari limeshaanza kazi. Jengo hili limejumuisha chumba cha upasuaji (*theatre*), chumba cha kuhudumia wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu – *Intensive Care Unit* (*ICU*), kliniki pamoja na wodi za kulaza wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua nyengine wizara imetiliana mkataba na Kampuni ya *Rans* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la watoto chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway. Jengo hilo litakalokuwa na wodi mbili, maabara ndogo, Kitengo cha Kusafisha Damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo (*dialysis unit*) na chumba cha watoto wanaohitaji uangalizi maalumu (*Accute Paediatric Care Unit*). Jengo hilo linatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka huu na gharama za ujenzi pamoja na vifaa unakisiwa kuwa ni zaidi ya dola milioni moja za Kimarekani.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo la kliniki ya maradhi maalumu, wodi ya wazazi, chumba cha huduma za dharura, chumba cha upasuaji, wodi ya watoto wachanga na wodi ya huduma za kangaroo kwa watoto tayari umeshanza. Vilevile mitambo ya "*sterilization*" kwa ajili ya vifaa vya upasuaji, mtambo wa kutengenezea "*oxygen*" na umeme wa jua vitawekwa. Ujenzi huo utagharimu jumla ya Euro 9.6m ambapo Euro 4.8m zitachangiwa na Serikali ya Uholanzi na sehemu iliyobaki zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikana na Jamuhuri ya Watu wa China, huduma ya *ICU* zimeimarishwa kwa kuikarabati wodi ya mifupa kuwa wodi ya *ICU* yenye vitanda vinane na kuiwekea vifaa vya kisasa. Ukarabati huo umekamilika na wodi hiyo tayari imefunguliwa rasmi tarehe 10 Januari 2015.

Mradi wa Kuzipandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Vijiji

Mhe. Naibu Spika, mradi huu una lengo la kuzipandisha hospitali za vijiji kuwa za Wilaya na hospitali mbili ya Abdalla Mzee na Wete kuwa ya Mkoa kuwa za Mkoa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha miundombinu kwa hospitali za vijiji, wizara imefanikiwa kumaliza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika hospitali ya Kivunge na kuanza ujenzi wa chumba cha upasuaji (*theatre*) katika hospitali ya Micheweni Pemba.

Mhe. Naibu Spika, wodi mpya na ya kisasa ya wazazi imejengwa katika hospitali ya Wete Pemba na tayari imeshaanza kutumika. Vile vile ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee unaendelea vizuri.

Mradi wa Taaluma za Afya (Zanzibar Medical School)
Mhe. Naibu Spika, mtakumbuka kwamba wizara ilianzisha mafunzo ya udaktari hapa nchini kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Matansas Cuba. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza hili kwamba jumla ya madaktari 38 tayari wamehitimu masomo yao mnamo mwezi wa Septemba 2014 na tayari wameanza kazi rasmi. Aidha, wanafunzi 12 wanaendelea na masomo yao ya mwaka wa sita.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mradi una mpango wa kuhakikisha wanafunzi 12 na walimu wao wanapatiwa huduma zote muhimu zinazohitajika ili kuwawezesha wanafunzi hao kuhitimu vizuri mafunzo yao.

CHANGAMOTO
Mhe. Naibu Spika, mbali na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa kazi zake bado wizara inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo:-

1. Ufinyu wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa kazi za wizara;
2. Upungufu wa wafanyakazi wenye taaluma ya juu ya uhandisi wa vifaa tiba (*Medical Equipment Technology*) inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia;
3. Uwepo wa uingizaji wa bidhaa zilizopitwa na muda wa matumizi na kuhatarisha afya za wananchi;
4. Utegemezi wa wahisani katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

MALENGO MAKUU YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KUPITIA MFUMO WA *PROGRAM BUDGET* (*PBB*)

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi malengo ya Wizara ya Afya katika bajeti ya mwaka 2015/2016 yatatekelezwa kwa njia ya programu ambapo sekta ya afya itakuwa na programu kuu tano, mbili kati ya hizo zitatekelezwa na Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Programu 1:	Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala
Programu 2:	Huduma za Kinga na Elimu ya Afya
Programu 3:	Huduma za Tiba.
Programu 4:	Huduma za Uchunguzi na Matibabu
Programu 5:	Uongozi wa Hospitali na Utawala

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakisha utekelezaji wa program, kila program imekusanya programu ndogo ndogo ikiwa na malengo makuu na kulenga matokeo ya muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala inalenga kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma bora kwa mujibu wa sheria na miongozo yenye misingi ya uwazi, uwajibikaji, ushiriki na ushirikishaji jamii katika kutoa maamuzi kwenye mambo yanayohusiana na afya katika ngazi zote. Programu hii ina programu ndogo tatu nazo ni Uongozi na Utawala, Sera, Mipango na Utafiti na Uratibu Shughuli za Afya Pemba. Malengo Makuu ya programu hii ni kama haya yafuatavyo:-

Kusimamia na kutoa miongozo juu ya uendeshaji wa sekta za afya

1. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi katika ngazi zote
2. Kuhakikisha ufanisi katika kazi na kuendeleza wafanyakazi kitaaluma
3. Kutoa msaada wa kiufundi kwa idara zote za ndani ya wizara ya afya.
4. Kutayarisha na kutoa miongozo ya kisera juu ya uendeshaji wa sekta ya afya
5. Kufanya tafiti na kukusanya taarifa za afya kwa ajili ya maamuzi ya kisera
6. Kuimarisha mifumo ya taarifa za afya.
7. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera ya afya na mipango kazi.
8. Kuongeza rasilimali fedha kwa kuanzisha na kutumia aina mbali mbali za kugharamia. Kama inavyoonekana hadi 12. huduma za afya ambazo ni endelevu na zenye kuzingatia uwiano.
9. Kuratibu, kutayarisha na kutekeleza mpango mkakati wa tatu wa sekta, mpango wa matumizi wa muda wa kati, mpango kazi wa mwaka na hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka.
10. Kusimamia na kuratibu misaada ya nje inayotokana na washirika wa maendeleo.
11. Kuratibu shughuli za uendeshaji za utoaji wa huduma za kinga na tiba Pemba.

Mhe. Naibu Spika, *program* hii imepangiwa jumla ya Tsh. 14,155,895,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, programu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya inalenga kutoa huduma bora za afya katika ngazi za Vituo vya Afya ya msingi daraja la kwanza na la pili na kuwa jamii yenye uwelewa jinsi ya kujinga na maradhi yenye kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni programu ya kinga na elimu ya afya. Malengo Makuu ya programu hii ni kama ifuatavyo: Kutoka Nam.1 hadi Nam.5.

1. Kuimarisha huduma za kinga ikiwa ni pamoja na huduma za uchunguzi wa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kwa jamii.
2. Kupunguza maradhi na vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga.
3. Kuongeza uwelewa kwa jamii jinsi ya kujikinga na maradhi na kuishi katika mazingira bora na yenye afya.
4. Kuimarisha mazingira ya afya na usalama kazini ili kupunguza ajali na maradhi katika sehemu za kazi.
5. Kuimarisha afya ya uzazi kwa mama na mtoto pamoja na vijana.

Mhe. Naibu Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Tsh. 32,963,434,000 kwa utekelezaji wa shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Huduma za Tiba inalenga kutoa huduma bora za matibabu katika hospitali za Vijiji, Wilaya na Hospitali ya Rufaa. Lengo kuu la programu hii ni kutoa huduma bora zenye viwango na ufanisi katika ngazi zote za hospitali pamoja na huduma maalumu. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni Programu ya Huduma za Hospitali.

Mhe. Naibu Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Tsh. 37,860,771,000 kwa utekelezaji wa shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina programu kuu mbili ambazo ni:

Programu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu na Programu ya Uongozi na Utawala.

Mhe. Naibu Spika, programu ya huduma za uchunguzi na matibabu inalenga kuimarisha huduma bora za matibabu ikiwa na malengo ya kuimarisha huduma

bora za uchunguzi na kupunguza kuugua vifo kwa wagonjwa. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni huduma za uchunguzi na huduma za matibabu. Aidha, kwa upande wa Programu ya Uongozi na Utawala inalenga kuhamasisha mazingira mazuri kwa wafanyakazi kwa lengo la kuimarisha taasisi na uongozi katika hospitali. Programu hii ina programu ndogo ya uongozi na utawala wa hospitali.

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uchunguzi na Matibabu imepangiwa jumla ya Shilingi 669,743,000 na Programu ya Uongozi na Utawala imepangiwa jumla ya Shilingi 7,334,757,000 kwa utekelezaji wa shughuli zake.

MGAWANYO WA FEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza programu hizo jumla ya Shilingi 84,980,100,000 zimepangwakwa mwaka wa fedha 2015/2016. Zikiwemo Shilingi 35,535,000,000 kutoka serikalini na Shilingi 49,445,100,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mchanganuo wa fedha kwa programu unapatikana kwenye **kiambatisho namba 12.**

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ina jukumu la kuchangia katika mfuko mkuu wa serikali kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato vilivyomo ndani ya taasisi hii. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Afya imepangiwa kuchangia jumla Shilingi 168,738,000. Kwa upande wa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja jumla ya Shilingi 902,973,000 zinatarajiwa kukusanywa kwa kipindi hicho.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Wizara ya Afya yalitegemea kwa kiasi kikubwa juhudi na maarifa ya watendaji, michango, maelekezo, ufuatiliaji na utekelezaji wa majukumu kutoka kwa Viongozi Wakuu wa Serikali, Wajumbe wa Baraza lako na wadau wengine wa afya.

Mhe. Naibu Spika, shukrani za kipekee ziende kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Wanawake na Watoto chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa ziara za kamati ambazo huzifanya kila robo mwaka na kutoa ushauri na maelekezo ya kuiendeleza sekta ya afya. Vile vile nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako ambao wamekuwa mstari wa mbele kuchangia na kufuatilia mmoja mmoja au kupitia kamati maalumu katika kuangalia utendaji na utekelezaji wa sekta ya afya. Nawashukuru wote ambao walichangia kwa nia na nguvu zote, nawaomba waendelee na utaratibu huo katika kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza tena kamati hii kwa maelekezo na ushauri walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti hii ambayo yamelenga zaidi maeneo muhimu na vipaumbele vya sekta. Aidha, nawashukuru

Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango na misaada mbali mbali waliyoitoa kwa wizara ikiwemo ushauri na maelekezo ambayo yamesaidia katika kutekeleza majukumu ya sekta ya afya.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukuwe fursa hii pia kuwashukuru viongozi wote na wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwa mashirikiano yao wakati wote kwa kuniwezesha kusimamia majukumu yangu kwa wepesi, nawaomba wazidi kuendelea na mashirikiano hayo kila siku katika kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa si kufanya haki kama sikuwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kuwa nasi wakati wote na kutupa mashirikiano mazuri katika kupokea huduma zinazotolewa katika sekta ya afya. Pia shukrani za pekee ziende kwa wananchi wa Jimbo la Ziwani kwa kuwa nami kwa kipindi chote cha uongozi wangu kwa kunipa mashirikiano mazuri katika utekelezaji wa kazi zangu za kila siku ni kiwa muwakilishi wa jimbo hili. Sina budi kuzishukuru taasisi nyengine za serikali na zisizo za serikali kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika suala zima la utoaji wa huduma za afya.

Mhe. Naibu Spika, msukumo mkubwa umeendelea kutolewa na mashirika ya kitaifa na kimataifa, pamoja na nchi marafiki. Msukumo huo wa hali na mali umesaidia kutoa huduma kwa wananchi. Nachukuwa fursa hii adhimu kuwashukuru hasa mashirika ya kimataifa yakiwemo *WHO, UNICEF, UNDP* na *UNFPA.* Pia shukrani ziende kwa *DANIDA, JICA, JSI, JHPIEGO, HIPZ, CLININTON FOUNDATION, GLOBAL FUND,PMI, KOICA, SAVE THE CHILDREN, SIGHT SAVERS INTERNATIONAL, PATH FINDER, IVODE CARNERI, USAID* na *MILELE FOUNDATION*. Pia shukrani ziende kwa serikali za nchi marafiki zikiwemo India, Israel, Cuba, Marekani, Italy, Netherland, Norway, Belgium, China, Misri, Oman, Turkey na wale wote ambao sikuwataja katika orodha hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hitimisho sasa naliomba Baraza lako lijadili, likubali na kuipitisha bajeti ya Wizara ya Afya. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wizara imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 84,980,100,000; kati ya hizo Shilingi 12,893,400,000 kwa kazi za kawaida, Shilingi 16,120,900,000 mishahara na maposho, Shilingi 870,700,000 ni ruzuku kutoka serikalini. Aidha, jumla ya Shilingi 5,650,000,000 kwa kazi za maendeleo kutoka serikalini, na Shilingi 49,445,100,000 ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Pia, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi 8,004,500,000 kwa ajili ya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho. Ufafanuzi wa taarifa za fedha unapatikana katika **Kiambatisho namba 13, 14, 15, 16** na **17.**

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba Wajumbe wa Baraza lako wameipokea hotuba hii, wataijadili kwa kina na kutoa michango yao kwa madhumuni ya kuiwezesha wizara katika kutekeleza majukumu yake. Wizara itaipokea michango yote itakayotolewa na kuifanyia kazi kama inavyostahiki kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

VIAMBATISHO

Kiambatisho namba 1: Uchunguzi wa Macho Vijijini, Julai 2014 – Machi, 2015

	Watu Wazima		**Watoto**		**Jumla**
Maradhi	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**	
Reffractive errer	150	160	32	27	**369**
Pterygium	12	18	0	0	**30**
Cataract	4	2	0	0	**6**
Conjuctivitis	27	37	9	15	**88**
Cornea abnormality	5	4	2	0	**11**
Retinal disorders	26	17	0	0	**43**
Pseudoplakia	15	6	2	0	**23**
Jumla	**239**	**244**	**45**	**42**	**570**

Kiambatisho Namba 2: Mahudhurio Wagonjwa wa Nje, Waliolazwa na Wagonjwa waliofariki katika Hospitali za Idara ya Tiba, Julai 2014-Machi 2015

Hospitali	Wagonjwa wa nje		Wagonjwa waliolazwa		Wagonjwa waliofariki	
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Mkoani	10,797	15,094	712	2,387	49	32
Chake Chake	21,050	28,530	2,210	5,503	81	73
Wete	18,804	26,403	1,350	3,787	35	37
Micheweni	7,015	9,312	593	1,841	21	13
Vitongoji	6,247	6,121	262	643	4	5
Kivunge	30,002	29,078	542	2,351	32	28
Makunduchi	10,325	12,211	457	1,593	8	7
Jumla	**104,240**	**126,749**	**6,126**	**18,105**	**230**	**195**

Kiambatisho Namba 3: Taarifa ya Hali ya Uzazi katika Hospitali za Idara ya Tiba, Julai 2014-Machi 2015

Hospitali	Jumla ya Wajawazito waliolazwa	Jumla ya Waliojifungua Kwa njia ya		Watoto waliozaliwa Hai		Jumla ya Wazazi waliofariki
		Kawaida	Upasuaji	Me	Ke	
Mkoani	1,691	1,316	96	720	663	3
Chake Chake	3,235	2,675	239	1,509	1,357	9
Wete	2,190	1,686	201	1,071	884	6
Micheweni	849	650	0	337	317	1
Vitongoji	209	175	0	103	74	0
Kivunge	1,865	1,651	10	880	794	3
Makunduchi	916	798	16	419	376	2
Jumla	**10,955**	**8,951**	**562**	**5,039**	**4,465**	**24**

Kiambatisho Namba 4: Mahudhurio ya Wagonjwa katika Kliniki za Maradhi Maalumu kwa Hospitali za Idara ya Tiba, Julai 2014-Machi 2015

Kliniki	Mkoani		Chake Chake		Wete		Micheweni		Vitongoji		Kivunge		Makunduchi	
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Cardiac	119	109	401	759	177	458	149	219	139	212	184	758	-	-
HIV CTC	100	130	277	477	271	430	145	386	-	-	-	-	8	11
Dental	650	910	664	1,024	903	1,100	156	246	65	77	788	1,306	765	1,031
Diabetic	226	286	308	653	168	286	58	85	29	43	384	600	236	448
ENT	556	1,015	1,333	2,064	546	624	109	134	-	-	-	-	-	-
Eye	889	1,256	1,262	1,856	2,996	3,181	373	418	199	218	169	179	156	176
Eye theater	-	-	-	-	71	69	-	-	-	-	-	-	-	-
Eye refraction	-	-	471	769	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Gynaecology	-	814		1,900		917	-	-	-	-	-	-	-	-
Major Theatre	106	151	356	498	158	251	-	-	-	-	53	14	72	35
Minor Theatre	220	115	708	625	371	186	-	-	355	107	3,070	1,143	-	-
Orthopedic	1,657	1,812	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Physiotherapy	64	123	302	263	113	108	-	-	-	-	-		236	355
Psychiatric	23	30	694	729	826	862	-	-	16	26	-	-	256	388
STI	11	22	5	68	3	7			44	58	14	106	13	31
Surgical OPD	598	701	959	924	834	297	1	7	-	-	-	-	-	-
Jumla	**5,219**	**7,474**	**7,740**	**12,609**	**7,437**	**8,776**	**991**	**1,495**	**847**	**741**	**4,662**	**4,106**	**1,742**	**2,475**

Kiambatisho Namba 5: Mahudhurio ya Wagonjwa wa Nje na Waliolazwa katika Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Julai 2014-Machi 2015

Hospitali	Wagonjwa wa nje		Wagonjwa waliolazwa		Wagonjwa waliofariki	
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Mnazi Mmoja	42,359	37,799	6,352	20,612	480	418
Mwembe Ladu	164	264	-	5,547	0	0
Kidongo Chekundu	3,684	3,994	350	281	2	1
Jumla	**46,207**	**42,057**	**6,702**	**26,440**	**482**	**419**

Kiambatisho Namba 6: Mahudhurio ya Wagonjwa katika Kliniki za Maradhi Maalumu kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja Julai, 2014 - Machi 2015

Kliniki	Me	Ke	Jumla
Cardiac	805	1,237	2,042
Dental	1,503	1,799	3,302
Diabetic	2,105	2,573	4,678
ENT	10,488	15,072	25,560
Eye	2,031	2,617	4,648
Eye Major Theatre	233	203	436
Major theatre	328	140	468
Minor theatre	2,781	1,942	4,723
Obs. and Gynae	-	2,631	2,631
Orthopedic	2,545	1,817	4,362
Paediatric medical	926	847	1,773
Physiotherapy and rehabilitation	2,104	1,996	4,100
Accupunture	996	1,355	2,351
Surgical OPD	2,881	1,534	4,415
STI/RTI	9	39	48
CTC Clinic	2,158	4,602	6,760
Jumla	**31,893**	**40,404**	**72,297**

Kiambatisho Namba 7: Taarifa ya Hali ya Uzazi katika Wodi ya Wazazi kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu, Julai 2014 –Machi, 2015

Hospitali	Jumla ya Wajawazito waliolazwa	Jumla ya Waliojifungua Kwa njia ya		Watoto waliozaliwa Hai		Jumla ya Wazazi waliofariki
		Kawaida	Upasuaji	Me	Ke	
Mnazi Mmoja	8,624	6,563	1,022	4,288	4,202	22
Mwembe ladu	4,926	4,594	71	2,392	2,285	0
Jumla	**13,550**	**11,157**	**1,093**	**6,680**	**6,487**	**22**

Kiambatisho Namba 8: Thamani ya Dawa na Zana za Tiba zilizopatikana, Julai 2014 –Machi, 2015

CHANZO	THAMANI (TSH)
SMZ	1,368,325,561
DANIDA	58,831,265
GLOBAL FUND	283,201,354
UNICEF	66,158,764
WHO	37,258,704
UNFPA	141,084,015
USAID	42,962,400
PROJECT HOPE	1,973,638,936
JUMLA	**3,971,460,999**

Kiambatisho Namba 9: Idadi ya Sampuli Zilizochunguzwa,

Julai 2014 – Machi, 2015

Taasisi	**Aina ya Kielelezo**	**Idadi ya Sampuli**
Polisi	Bhangi	95
	M/kulevya	80
	Pombe	30
	Mikojo	333
	Damu	20
	Sumu	9
Jumla Ndogo		567
Taasisi ya watu Binafsi	Tomato	2
	Asali	18
	Sabuni	2
	Kibali cha kemikali	1
Jumla Ndogo		23
JUMLA KUU		**590**

Kiambatisho Namba 10: Wanafunzi Waliokwenda Masomoni, Julai 2014 - Mei 2015

KADA/FANI	KIWANGO						
	DIPLOMA	ADV.DIP	DEGREE	POST GRAD	MASTERS	PHd	TOTAL
V.CONTROL		3					3
SOCIAL WORK			2				2
SCIENCE AND BEHAVIOR CHANGE					1		1
PUBLIC HEALTH			3		3		6
PSYCHOLOGY AND CONCELLING			1				1
PROCUREMENT AND CONTRACT MANAGEMENT			3				3
PHARMACY			4				4
PATHOLOGY						1	1
PAEDIATRICS					3		3
NURSING	2		10		3		15
MONITORING &EVALUATION				3			3
MOLECULAR MEDICINE					1		1
MIDWIFERY AND WOMAN HEALTH					2		2
MICROBILOGY AND IMMUNOLOGY					1		1
MEDICAL LABORATORY SCIENCE			1				1
MEDICAL BIOCHEMISTRY					1		1
MBBS			4				4

LIBRARIAN	1						1
INTERNAL MEDICINE					2		2
IMAGE SCIENCE AND NUCLEAR MEDICINE					2		2
HUMAN RESOURCES PLANING AND MANAGEMENT			1				1
HOME ECONOMIC AND NUTRITION			2				2
HEALTH SYSTEM MANAGEMENT					1		1
HEALTH PROMOTION			1	1			2

Jadweli la walio masomoni linaendelea

KADA/FANI	KIWANGO						
	DIPLOMA	ADV.DIP	DEGREE	POST GRADUATE	MASTERS	PHd	TOTAL
HEALTH MONITORING AND EVALUATION					2		2
GLOBAL HEALTH					1		1
GASTROENTROENTERITIS					1		1
FOOD SCIENCES AND TECHNOLOGY					1		1
EYE CARE					1		1
ENVEROMNENTAL HEALTH			5				5
ENT					1		1
ECONOMIC AND FINANCE					1		1
DESASTER MANAGEMENT					1		1
CRITICAL CARE AND TRAUMA					1		1
COMPUTER SCIENCE			1		1		2
CLINICAL STOMATOLOGY					1		1
CHINESE MATERIAL MEDICAL						1	1
BUSINESS INFORMATION TECHNOLOGY	1						1
BIOMEDICAL ENGINEERING					1		1
ANAETHESIA		5					5

AMO		2					2
ACCOUNTING AND INVESTMENT					1		1
JUMLA	**4**	**10**	**38**	**4**	**34**	**2**	**92**

Kiambatisho Namba 11: Taarifa ya Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja, Julai 2014 hadi Machi, 2015

WILAYA	BCG	Polio 3	Penta 3	Surua Rubella
Unguja				
Kaskazini A	6,409	3,375	4,444	4,191
Kaskazini B	3,129	2,116	2,887	2,735
Kati	3,708	3,018	3,608	3,246
Kusini	1,542	1,311	1,666	1,473
Magharibi	16,968	7,239	9,553	10,689
Mjini	22,507	6,862	9,898	9,633
Jumla Ndogo	*54,263*	*23,921*	*32,056*	*31,967*
Pemba				
Chake	7,217	4,999	5,018	5,218
Micheweni	5,893	4,059	4,058	4,130
Mkoani	5,631	3,746	3,686	3,869
Wete	8,066	5,390	5,416	6,298
Jumla Ndogo	*26,807*	*18,194*	*18,178*	*19,515*
JUMLA KUU	**81,070**	**42,115**	**50,234**	**51,482**

Kiambatisho Namba 12: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Programu 2015/16

PROGRAMU	PROGRAMU NDOGO	JUMLA KUU	KAZI ZA KAWAIDA	RUZUKU	KAZI ZA MAENDELEO (MCHANGO WA SERIKALI)	KAZI ZA MAENDELEO (FEDHA ZA WAFADHILI)	MAKUSANYO
P01 Huduma za Kinga na Elimu ya Afya	S01 Kinga na Elimu ya Afya	32,963,434,000	7,589,961,000	-	650,000,000	24,723,473,000	47,338,000
P02 Huduma za Tiba	S01 Huduma za Hospitali	37,860,771,000	9,568,444,000	70,700,000	4,500,000,000	23,721,627,000	25,400,000
P03 Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala	S01 Uongozi wa Utawala	3,106,943,000	2,806,943,000	300,000,000	-	-	-
	S02 Sera Mipango na Utafiti	3,417,952,000	1,542,952,000	375,000,000	500,000,000	1,000,000,000	-
	S03 Kuratibu Shughuli za Afya Pemba	7,631,000,000	7,506,000,000	125,000,000	-	-	96,000,000
JUMLA		**84,980,100,000**	**29,014,300,000**	**870,700,000**	**5,650,000,000**	**49,445,100,000**	**168,738,000**

Kiambatisho Namba 13: Makadirio ya Miradi ya Maendeleo kwa Programu 2015/16

PROGRAMU KUU	HUDUMA/MIRADI	JUMLA KUU	MCHANGO WA SERIKALI	FEDHA ZA WAHISANI
P01 Huduma za Kinga na Elimu ya Afya	S01 Programu ya Kinga na Elimu ya Afya			
	H01 Mradi Shirikishi wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto	1,837,142,000	500,000,000	1,337,142,000
	H02 Mradi Shirikishi wa Huduma za Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma	5,842,895,000	100,000,000	5,742,895,000
	H03 Programu ya Huduma ya Kumaliza Malaria Zanzibar	17,693,436,000	50,000,000	17,643,436,000
	JUMLA	25,373,473,000	650,000,000	24,723,473,000
P02 Huduma za Tiba	S01 Programu ya Huduma za Hospitali			
	H01 Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Vijiji	11,724,000,000	300,000,000	11,424,000,000
	H02 Mradi wa Chuo cha Kusomeshea Madaktari - Zanzibar	200,000,000	200,000,000	-
	H03 Mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa	16,297,627,000	4,000,000,000	12,297,627,000
	JUMLA	28,221,627,000	4,500,000,000	23,721,627,000
P03 Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala	S02 Sera, Mipango na Utafiti			
	H05 Kuchunguza Sampuli mbalimbali kwa Jamii	1,500,000,000	500,000,000	1,000,000,000
JUMLA		1,500,000,000	500,000,000	1,000,000,000
JUMLA YA FEDHA KWA KAZI ZA MAENDELEO		55,095,100,000	5,650,000,000	49,445,100,000

Kiambatisho Namba 14: Muhtasari wa Makisio ya Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

kwa kipindi cha 2015 - 2016

PROGRAMU KUU	**MAELEZO**	**JUMLA KUU**	**FEDHA ZA KAWAIDA**
P01 Huduma za Uchunguzi na Matibabu	**S02 Huduma za matibabu**		
	H01 Kutoa Huduma kwa Wagonjwa	669,743,000	669,743,000
	JUMLA	**669,743,000**	**669,743,000**
P02 Uongozi na Utawala	**S01 Uongozi na Utawala wa Hospitali**		
	H02 Kutoa huduma za Mipango na Utumishi	7,334,757,000	7,334,757,000.00
	JUMLA	**7,334,757,000**	**7,334,757,000**
Jumla kuu kwa Programu		**8,004,500,000**	**8,004,500,000**

Kiambatisho Namba 15: Fedha Zilizotengwa na Kukusanywa kwa Kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 na Makisio ya 2015/2016

KASMA	MAELEZO YA MAPATO	MAKADIRIO 2014/2015	MAKUSANYO JULAI-MACHI 2014/2015	ASILIMIA (%)	MAKISIO YA MAPATO 2015/2016
0601	**IDARA YA KINGA**				
142238	Shahada ya maradhi ya kuambukiza	16,000,000	7,842,000	49.0	29,338,000
142260	Huduma za daktari na orodha wa wafanyakazi na abiria	15,000,000	9,064,000	60.4	18,000,000
	Jumla ndogo	**31,000,000**	**16,906,000**	54.5	**47,338,000**
0701	**IDARA YA TIBA UNGUJA**				
142261	Malipo ya X-Ray na uchunguzi wa damu.	20,000,000	15,961,000	79.8	25,400,000
	Jumla ndogo	**20,000,000**	**15,961,000**	79.8	**25,400,000**
0801	**IDARA YA TIBA PEMBA**				
142261	Malipo ya X-Ray na uchunguzi wa damu.	3,000,000	3,688,000	122.9	6,000,000
	Jumla ndogo	**3,000,000**	**3,688,000**	122.9	**6,000,000**
145000	**MAPATO MENGINEYO**				
145002	**Mapato mengineyo**	70,000,000	71,639,500	102.3	90,000,000
	Jumla ndogo	**70,000,000**	**71,639,500**	102.3	**90,000,000**
	JUMLA KUU	**124,000,000**	**108,194,500**	87.3	**168,738,000**
1501	**HOSPITALI YA M/MMOJA**				
145001	**Mapato mengineyo**	200,000,000	306,385,954	153.2	475,859,807

145003	**Huduma za haraka**	350,000,000	276,255,409	78.9	427,113,193
	Jumla ndogo	**550,000,000**	**582,641,363**	105.9	**902,973,000**
	JUMLA KUU	**674,000,000**	**690,835,863**	102.5	**1,071,711,000**

Kiambatisho Namba 16: Fedha Zilizotengwa na Kuingizwa kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo kutoka Serikali kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 na Makisio 2015/2016

KASMA	MAELEZO	MAKADIRIO 2014/2015	MATUMIZI HALISI JULAI-MACHI. 2015	ASILIMIA %	MAKISIO KAZI ZA KAWAIDA 2015/2016
O301	OFISI KUU PEMBA	100,000,000	21,804,625	21.8	145,000,000
O401	MIPANGO NA SERA UNGUJA	252,896,000	42,060,309	16.6	452,000,000
O601	KINGA - UNGUJA	259,000,000	109,723,900	42.4	2,126,100,000
O701	TIBA - UNGUJA	1,361,376,000	2,538,971,289.95	186.5	3,000,000,000
O801	TIBA - PEMBA	732,424,000	136,741,125	18.7	782,000,000
O901	KINGA - PEMBA	145,000,000	25,793,625.00	17.8	275,000,000
2001	UTUMISHI NA UENDESHAJI – UNGUJA	1,031,360,000	340,743,774	33.0	1,150,000,000
2002	UTUMISHI NA UENDESHAJI – PEMBA	150,000,000	51,160,625	34.1	163,300,000
2003	BOHARI KUU YA DAWA	216,896,000	38,303,625	17.7	300,000,000
2101	MFAMASIA MKUU WA SERIKALI	3,004,248,000	744,460,604	24.8	4,500,000,000
	JUMLA	**7,253,200,000**	**4,049,763,501.95**	**55.8**	**12,893,400,000**
	RUZUKU				
2004	CHUO CHA AFYA MBWENI	463,296,000	168,853,281	36.5	300,000,000
1401	MKEMIA MKUU - UNGUJA	566,420,000	174,508,379	-	375,000,000
1601	MKEMIA MKUU - PEMBA	189,484,000	127,727,921	-	125,000,000

	BODI YA CHAKULA NA VIPODOZI	-	-	-	70,700,000
	JUMLA	**1,219,200,000**	**471,089,581.00**	**38.6**	**870,700,000**
	JUMLA NDOGO	**8,472,/400,000**	**4,520,853,082.95**	**53.4**	**13,764,100,000**
	MISHAHARA NA MAPOSHO				
2001	UTUMISHI NA UENDESHAJI - UNGUJA	7,681,739,000	6,706,169,739	87.3	9,816,900,000
2002	UTUMISHI NA UENDESHAJI - PEMBA	6,593,061,000	4,664,623,080	70.8	6,304,000,000
	JUMLA	**14,274,800,000**	**11,370,792,819**	**79.7**	**16,120,900,000**
	JUMLA YA BAJETI KAZI ZA KAWAIDA	**22,747,200,000**	**15,891,645,901**	**69.9**	**29,885,000,000**
KASMA	**MIRADI YA MAENDELEO**	**MAKADIRIO 2014/2015**	**MATUMIZI HALISI JULAI-MACHI.2015**	**ASILIMIA %**	**MAKISIO KAZI ZA KAWAIDA 2015/2016**
1210018	Program ya Kumaliza Malaria Zanzibar	50,000,000	733,276,441	**1,467.0**	50,000,000
1210004	Taaluma za Afya (ZMS)	150,000,000	179,520,580.98	**119.7**	200,000,000
1210012	Kuipandisha Hadhi M/Mmoja Hospitali	2,500,000,000	1,113,765,258.66	**44.6**	4,000,000,000
1210010	KuvipandishaHadhi Vituo vya Afya	200,000,000	47,359,600	**23.7**	300,000,000
1210022	Mradi Shirikishi wa Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma	50,000,000	2,000,000	**4.00**	100,000,000
1210023	Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na	800,000,000	271,900,119.16	**34.0**	500,000,000

	Mtoto				
1210003	Kustawisha siha za Wazanzibari	100,000,000	20,000,000	**20.0**	-
	Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu	-	-	**-**	500,000,000
	JUMLA KWA MIRADI	**3,850,000,000**	**2,367,822,000**	**61.5**	**5,650,000,000**
	JUMLA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI	**26,597,200,000**	**18,259,467,901.95**	**68.7**	**35,535,000,000**

Kiambatisho Namba 17: Fedha Zilizotengwa na Kuingizwa kwa kazi za Maendeleo kutoka kwa Wahisani kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 na Makisio 2015/2016

KASMA	MIRADI	MAKADIRIO 2014/2015	MATUMIZI HALISI JULAI - MACHI. 2015	ASILI MIA %	MAKISIO 2015/2016
1210018	Programu ya kumaliza Malaria	2,849,803,000	71,693,750	2.5	17,643,436,000
1210004	Taaluma za Afya (ZMS)	-	-	-	-
1210012	Kuipandisha Hadhi M/Mmoja Hosp.	3,760,000,000	-	-	12,297,627,000
1210010	Kuvipandisha Hadhi Vituo vya Afya	10,000,000,000	-	-	11,424,000,000
1210022	Mradi Shirikishi wa Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma	4,268,198,000	32,759,750	0.8	5,742,895,000
1210023	Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na Mtoto	2,268,769,000	1,148,430,820	50.6	1,337,142,000
1210003	Kustawisha siha za Wazanzibari	1,210,127,000	-	-	-
	Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu	-	-	-	1,000,000,000
	JUMLA	**24,356,897,000**	**1,252,884,320**	**5.1**	**49,445,100,000**
	JUMLA KUU	**50,954,097,000**	**,512,352,221.95**	**38.3**	**4,980,100,000**

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, ahsante. Napenda kuchukua fursa hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu ambaye ametujaalia neema ya uhai na uzima na kutupa uwezo wa kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa niaba ya wananchi tunaowawakilisha kupitia nafasi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi chote ambacho tumekuwa tunatekeleza majukumu yetu ya kamati, Wajumbe wa Kamati wamekuwa wakichukua jitihada za dhati katika kufanikisha majukumu hayo na hivyo sina budi kuchukua fursa hii kuwapongeza kwani bila ya jitihada na mashirikiano yao tusingeweza kufanikisha shughuli za kamati kwa muda uliokusudiwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa nguvu na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, chimbuko la taarifa hii linatokana na jukumu uliotukabidhi la kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali kwa Wizara ya Afya juu ya makadirio, mapato na matumizi ya kila mwaka kama kanuni ya 112(e) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (toleo la 2012) inavyoelekeza. Aidha, baada ya kukamilisha kazi hiyo, kwa maelekezo ya kanuni ya 96(1) Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya kamati mzima hutakiwa kumpa taarifa Mhe. Spika juu ya kukamilisha jukumu waliokabidhiwa na mimi nilifanya hivyo kwa niaba ya kamati.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba niwatambuwe Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
5.	Mhe. Mohamed Mbwana hamad	Mjumbe
6.	Mhe. Farida Amour Mohamed	Mjumbe
7.	Mhe Mwanaid Kassim Mussa	Mjumbe

Mhe. Naibu Spika, aidha kamati katika kutekeleza majukumu yake inasaidiwa na makatibu wawili ambao pamoja na mambo mengine hufanya shughuli za kuratibu mikutano yetu katika kamati na hatimae kufanikisha utekelezaji wa shughuli inayokusudiwa. Kwa mchango wao mkubwa wanaotupatia naomba nao niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Ndg Abubakar Mahmoud Idd na
2. Ndg. Asha Said Mohamed.

Mhe. Naibu Spika, kamati imefanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2015/2016 siku ya Ijumaa ya tarehe 08/05/2015 iliyowasilishwa katika mfumo mpya wa bajeti kwa programu yaani *(Programme Based Budget)*. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya imepangiwa kutekeleza Programu Kuu tatu ambazo ni:

1. Programu za Kinga na Elimu ya Afya,

2. Programu ya Huduma za Tiba

3. Programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala.

Mhe. Naibu Spika, katika mfumo huu mpya uliowasilishwa, Kamati ilipitia na kuchambua makadirio ya mapato ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 wizara imekisiwa kukusanya Jumla ya Shilingi (168,738,000) milioni mia moja na sitini na nane, laki saba na thalathini na nane elfu kupitia malipo ya *X –ray* na Uchunguzi wa damu yanayokusanywa na Idara ya Tiba kwa upande wa Unguja na kwa Pemba yanakusanywa na Ofisi kuu Pemba.

Aidha, mapato mengine yaliopangiwa kukusanywa na wizara hii ni pamoja na malipo ya huduma za afya ambayo yatakusanywa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti, mapato yanayotokana na shahada ya maradhi ya kuambukiza na mapato ya orodha ya wafanyakazi na abiria ambayo yatakusanywa na Idara ya Kinga Unguja.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza Wizara hii kwa majukumu wanayoyatekeleza katika shughuli zao za kila siku hasa kwa upande wa ukusanyaji wa mapato. Hii imedhihirika wakati kamati yako ilipokuwa ikipitia na kuchambua mswada wa makadirio ya mapato ya wizara pamoja na Hospitali ya Mnazi mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kamati imegundua kwamba mapato waliyojipangia kukusanya kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 yameongezeka kutoka Shilingi 124,000,000 (milioni mia moja na ishirini na nne) hadi Shilingi 168,738,000

(milioni mia moja na sitini na nane, laki saba na thalathini na nane elfu) na kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja makadirio ya makusanyo yameongezeka kutoka Shilingi 550,000,000 (milioni mia tano hamsini) mwaka wa fedha 2014/2015 hadi Shilingi 902,973,000 (milioni mia tisa na mbili, laki tisa na sabini na tatu elfu) kwa mwaka huu wa fedha. Hii ni hatua kubwa ambayo kamati yetu inajivunia.

Kamati ilipofanya uchambuzi wa makadirio ya wizara kwa kazi za kawaida imebaini ongezeko la makadirio hayo ambapo kwa mwaka wa fedha uliotangulia makadirio yalikuwa ni Shilingi 22,747,200,000 (bilioni ishirini na mbili, milioni mia saba na arubaini na saba na laki mbili) na katika mwaka huu wa fedha wa 2015/2016 makadirio ni Shilingi 29,885,000,000 (bilioni ishirini na tisa na milioni mia nane na thamanini na tano). Kamati imeridhika sana na ongezeko hilo na inaitaka Wizara ya Fedha kuiingizia wizara hii fedha ipasavyo ili iweze kufanikisha shughuli walizojipangia kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali pekee ya rufaa ambayo inategemewa na wananchi wetu wote na ndio kimbilio la wengi. Mwelekeo wa Hospitali hii ni kutoa huduma bora za afya zitakazowafikia wananchi wote, lakini kamati imekuwa na wasiwasi mkubwa juu ya kufikia muelekeo huo kwani hospitali inakabiliwa na changamoto ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, makadirio ya mwaka huu wa fedha yamepungua kwani Hospitali imekadiriwa kupata Shilingi 8,004,500,000 (bilioni nane, milioni nne na laki tano) ukilinganisha na makadirio ya mwaka uliotangulia ambayo yalikuwa ni Shilingi 8,282,000,000 (bilioni nane na milioni mia mbili na thamanini na mbili). Kushuka kwa makadirio ya fedha katika hospitali hii kunaashiria kudorora kwa utekelezaji wa majukumu yao na kudhoofika kwa huduma zinazotelewa. Kwa msingi huo, kamati inaitaka serikali kuipa kipaumbele hospitali hii na kuipatia fedha za kutosha ili itekeleze majukumu yake ipasavyo na ile azma ya kuwapatia huduma bora kwa wananchi wote iweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu kama ilivyo kwa Kamati nyengine za Kudumu za Baraza lako tukufu hii ni fursa yake ya mwisho ya kupitia bajeti ya serikali mpaka muda mwengine kwa watakaobahatika kuchanguliwa katika Baraza lijalo. Hivyo, kamati yetu imeona ni busara kutumia fursa hii kuweza kushauri maeneo ambayo hayakuweza kukamilishwa kwa kwa kipindi cha miaka miwili na nusu ambayo ulitupa jukumu la kusimamia wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa 2014/2015 miongoni mwa malengo makuu ya wizara ni kuimarisha miundombinu ya afya kwa kulifanyia matengenezo jengo la macho la Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuendelea na ukarabati wa majengo na vituo vya afya. Kamati imebaini kuwa hatua za kulifanyia marekebisho

jengo hilo bado hazijakamilika na muda umekuwa mrefu, hivyo inaitaka wizara kufuatilia kwa karibu ili kukamilisha ukarabati huo. Aidha, kamati inaitaka Wizara kupitia programu zake kuvifanyia matengenezo vituo vya afya vikiwemo vya Ukutini na Kojani ili kuimarisha huduma za afya vijijini.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ya kukosekana kwa jengo la ofisi kwa upande wa Pemba ni tatizo kubwa ambalo linazorotesha ufanisi wa kazi kwa wizara hii. Kamati imeshuhudia kadhia hiyo ambayo inasababisha usumbufu mkubwa, kwani imeshuhudia kuwa watendaji wa wizara wanafanya kazi zao katika Hospitali ya Wete kitu ambacho kinazorotesha ufanisi wa wizara hii. Kiukweli kamati haifurahishwi hata kidogo na hali hiyo, kwani watendaji wanakosa utulivu wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao. Hivyo, kamati inaitaka serikali kuliona tatizo hilo na kulitafutia ufumbuzi.

Katika Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2012/2013 iliripoti kukosekana kwa Kifaa cha *DNA* na Kamati imeshauri juu ya umuhimu wake na namna kitakavyosaidia kutatua kesi za udhalilishaji. Hivyo, kamati inachukua fursa hii tena kuitaka serikali kununua kifaa hicho ili kisaidie katika kutatua kesi za udhalilishaji hasa kwa wanawake na watoto.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaitaka wizara katika bajeti hii kuipatia ruzuku Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwani kwa kipindi kirefu bodi hiyo haipatiwi ruzuku. Aidha, kamati inaitaka wizara kufuatilia na kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006 ili iende sambamba na mahitaji ya bodi.

Mhe. Naibu Spika, kiujumla kamati imepitia Bajeti ya Wizara na kufanya uchambuzi wake na napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, kamati ilijitahidi kupitia kwa umakini mkubwa licha ya kuwa mfumo huu mpya bado haujazoeleka vizuri kwa Wajumbe. Kamati inaisisitiza wizara kutekeleza programu zake kwa umakini mkubwa na kwa upande wa serikali kuzingatia maoni ya kamati ili kuboresha sekta ya afya nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nakushuku wewe kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa usikivu wao. Naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, na mimi niseme nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Baraza lako hili tukufu na ni mwenye kutoa fikra na mawazo kuweza kuichangia serikali kwa lile ambalo nililoliona katika wizara husika.

Mhe. Naibu Spika, hii ni Wizara ya Afya, Wizara ya Afya ni moja katika muhimili mkubwa sana hata sisi sote binaadamu tunategemea hapa na haswa ukiangalia hapa na Rais wetu wa Zanzibar anangalia hii mashine ya kufundishia ya kuangalia, nafikiri kitengo cha *cancer* hiki naikumbuka kama hivyo hii mashine, kuona jinsi gani wizara hii ilivyojitahidi katika mambo ambayo yaliyokuwa ni muhimu sana.

Huku nyuma nilipokuwa nikiangalia nimeona jengo jipya ambalo *alhamdulillah* matatizo ya kichwa kuvimba maji, ubongo, juzi moja nilishuhudia operesheni mmoja mkubwa sana ulifanywa Zanzibar sikuweza kuamini Mhe. Naibu Spika. Kuna mtu alipata matatizo kwenye ubongo na kwa bahati nzuri nilipewa taaluma nzuri sana jinsi ulivyokatwa sehemu hiyo na nikaelimishwa jinsi gani kilichokuwa kinatafutwa, kule ndani na jinsi gani baadae kinaweza ku-*recover* pale kwa kweli mimi sikuamini. Yule mtu katolewa kipande kwenye kichwa ambacho kuna kitu ambacho jamaa alipigwa kigongo huko nyuma ili kwenda kutizamwa lile kate la damu lililokuwemo huko ndani kuwa amepewa *treatment,* hapo kwa kweli ni jambo ambalo nimefurahi sana na wakati huko nyuma hatuna historia hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nikasema hii ni kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa! Nilikubali jina hilo Mhe. Naibu Spika, wala sina pingamizi nalo na hasa kuona vitu vyake vile vilivyokuwa huko nyuma hatukuwa na historia na kuwa na vitu kama hivi.

Kwanza niseme serikali ile sasa hivi hospitali ile imeshakuwa kubwa kwanza niseme hivyo kutokana na hali ya *population* ya watu sasa hivi wanavyoumwa. Tukitaka tusitake ile hospitali sasa hivi imeshakuwa mzigo inabeba mzigo mkubwa sana. Huko nyuma nafikiri kulikuwa na *plan* nzuri tu ya kusema kuwa tuimarishe hizi hospitali zetu za wilaya ili kuondoa mzigo kule sasa sijui umefikia wapi. Tunazo hospitali nzuri za wilaya hasa kwa kwetu Kaskazini huko Kivunge kusini huko Makunduchi na halkadhalika na sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na jina hilo hilo niite Hospitali ya Rufaa. Mimi nina historia moja niseme kuwa tangu na asubuhi hospitali mimi naijua wakati huo sijawa Mwakilishi, niliwahi kufanyiwa operesheni zamani sana wa *appendix* tangu wakati huo Marehemu Dr. Jumbe zamani sana ndio nimefanya mimi wa *appendix* wa mshipa sijafanya wakati ule Mhe. Naibu Spika.

Sasa wakati ule na sasa hivi tafauti wakati ule hakuna ile wingi la watu kufanya operesheni wanaweza wakafanya operesheni kwa siku moja au wiki nzima wakafanya mtu mmoja operesheni katika hesabu zangu kidogo nikiangalia. Halafu sikuwa na fahamu hata siku moja hospitali ile wakalazwa watu chini mimi sikufahamu.

Sasa mimi nikawa najiuliza sijafahamu kuona msongomano mkubwa wa watu sasa kufanyiwa operesheni ndani ya hospitali ile, sikufahamu kwenye mawodi watu wanalala mpaka chini sikuwahi kuona hilo. Lakini sasa watu wanalala chini.

Lakini kipindi kile ulikuwa unahamu hata ulale chini na sababu gani zilizofanya kuwa una hamu ya kulala chini. Vile vile Mhe. Naibu Spika, kule kulikuwa na *full dressing* ya kutandika kitanda kizuri tu. Mimi nilipokwenda operesheni kila siku akija daktari nilikuwa najifanya naumwa nilikuwa naona tabu kutoka nilikuwa naona raha nikae mle ndani tu. Leo hakukuchi utataka utoke hospitali hata ile nusu dakika ukija juu tu nitoeni jamani nje.

Mhe. Naibu Spika, iko haja sasa hivi hospitali ya Mnazi Mmoja ututafutie eneo jengine la ziada liendane na jina la Rufaa. Wala tusibishe kwa sababu mtu unakwenda na maradhi moja unapata mara mbili maradhi, tunaambukizana kwa sababu kitanda kimoja wanalala watu wawili, sasa umelala hapo mwezako kafa kijasho kiko hapo na wakati mmlezwa kitanda kimoja watu wawili.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri nimshukuru sana Katibu wake pamoja na Wakurugenzi na Naibu Waziri kwa jitihada zao wanazozifanya hali halisi ilivyo. Mimi sipendi Mhe. Naibu Spika, kuwaoneshea kidole wao. Kwa sababu wao hawana fedha za kuweza kuendesha vizuri wana *plan* na mimi naamini wataalamu wetu wana- *plan* jinsi gani kwa sababu pale kuna *management* ambayo ya Afisi tu wanaratibu mambo ya Afisi. Sasa kutokana na hali halisi bajeti zao mara nyingi sana zinakuwa ni funyu.

Mhe. Waziri hapa alisema mambo mengi changamoto alizitaja humu na baadhi ya mambo mengine ambayo yanakuwa hayaridhishi. Kwanza niwapongeze sana siku hizi hata lile neno Kichocho naona haisemwi si sana hilo suala mimi nakupongezeni sana, hapo nakupeni mia kwa mia mmefanya vizuri. Unajua zamani sana nilipokuwa mdogo ikifungwa Shule nilikuwa nakwenda shamba mara nyingi sana nilikuwa nasikia neno la Kichocho. Lakini sasa hivi asilimia imepungua sana. Kwa hiyo, hapo natoa pongezi muendelee na jitihada zenu hizo hizo za kuweza kuondoa hata matende nao hali kadhalika niseme ukweli mmejitahidi sana sifa lazima nitoe.

Mhe. Naibu Spika, hata mabusha sasa hivi yanaanza kupungua. Nilikuwa na Mwalimu wangu pale tukishirikiana sana sijui kama keshastaafu yule jina lake kidogo limenitoka, lakini tukitoka atanipigia simu atanikumbusha, tulikuwa tukishirikiana kuondoa watu mabusha na ilikuwa tatizo kubwa na halafu ilikuwa- *expensive* kidogo anaona tabu na watu walikuwa hawajafahamu nini tatizo lake lile, busha kuondolewa walifikiria labda kwenda pale kuondolewa ni kifo, tumewaelimisha watu tujitahidi *alhamdulillah rabil alamin* nashukuru sasa hivi wengi hawana mabusha wamekuwa vijana. Nalo hilo niwapongeze sana

niwashukuru sana kwa jitihada hizo na Mwenyezi Mungu awazidishie waendelee katika hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, naingia katika idara yenyewe sasa inaitwa ya Hospitali ya Mnazi Mmoja halafu na Hospitali yenyewe ya Mmazi Mmoja. Kwanza mimi nataka niwaombe wafanyabiashara wenzetu kule Bara Mabenki wanapenda kuleta mashuka wakayatia nembo zao zile za Benki, kwa kweli inakuwa inapendeza sana kuwasaidia. Lakini nimejaribu sana kuwapigia debe Wizara ya Afya ili na hawa wafanyabiashara waweze kuwasaidia mimi sijasikia hata mmoja na tunao wengi sana wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spia, hawa tuwasaidieni Wizara ya Afya tena nataka niseme sana wafanyabiashara tuwasaidieni hawa Wizara ya Afya kwa sababu bajeti zao wanazopewa bajeti zao ni ndogo wana- *expensive* ya vitu, lazima tuwasaidie ukweli ni huo uko wazi haufikichiki. Jamani kwa sababu kifaa kimoja leo *city scan* haina filamu nambieni tena hili waziri usije ukanijibu nimeshapiga mimi *city scan* tena kuna rikodi yangu mle nimepiga juzi tu nimefanya lakini haina filamu tena mashine nzuri *East African* peke yake yake Zanzibar lakini haina filamu unapewa *result* za *record* pale anakwenda mtu anatizama pale tu halafu anatoa ripoti sawa, imekwisha huna kumbukumbu ya picha iki- *flat* ile, mchezo umekwisha.

Sasa haya ni mambo kasoro ndogo ndogo hebu nambie *how much* si kitu cha mchezo hichi, ni nusu ya bajeti hii wakienda kifaa hicho. Kwa kweli jamani naomba sana wafanyabiashara wenye mabenki hebu tuwe na uzoefu jamani nisikilizeni na mie kijana wenu ninayepiga debe, tusiisaidie serikali kupitia kitengo cha Wizara ya Afya. Jamani inafika Wizara ya Afya hata zile *gloves* hawana wala msikatae hili mkikataa tutapambana mimi na nyie kubalini mimi nakupigieni debe na ushahidi ninao wa kusema *gloves* hamna.

Sisemi kama wanafanya kusudi hawa hapana maji yamewafika shingoni si mchezo, kwa sababu nimesema zamani *population* hali halisi ilivyo leo tunazaana maradhi leo yakuwa mengi vyakula viko ovyo kabisa maradhi ya kila aina yanachipuka hapa tusijae tele hospitali, lazima tunajaa hospitali na nilisema zamani watu unapenda kabisa ulale kwenye sakafu.

Leo hufanyi hata siku moja kitu hicho *wallah* watu wanalazwa chini godoro moja nimeona wamelazwa watu watatu shuhuda mwenyewe tena wengine wajawazito, nimekwenda wodi ya juu ghorofa ya tatu kabisa labda mnizuie siku hizi niseende kama ukinizuia nisende kuuguza wagonjwa wangu sawa hakuna tatizo, nimeenda nimepigiwa simu mtoto ana maradhi ya jicho kalazwa kule juu mtoto mdogo kama ana miaka kumi na nne tu hivi.

Nilipokwenda kule yamezidi lakini sikulaumuni *wallahi* mimi sikulaumini naona uchungu nimeona unamkiuka mgonjwa *distance* ndogo, ili upate mgonjwa wako tena kwa sababu yale madogoro kwanza ile *mark* yake ni ndogo sana nimetoka kule nimekuja huku nimekuta kigodoro kile kile kina watu watatu wagonjwa wanangojea kwenda kufanyiwa operesheni siku ya pili yake.

Mhe. Waziri, mimi naomba sana tuwe na mapenzi ya wafanyabishara, twende kule hospitali tukaangilie tukawaambie hawa hawakatai nani mtu anakata msaada, hebu twendeni jamani tukawaone wenzetu hawa tuwasaidieni. Hili jambo kubwa ni pepo kubwa si mchezo pepo unaipata hapa hapa duniani unaweza kuipata pepo mapema tu ukitoa kidogo unapata kingi kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu umeenda kuwasaidia watu ambao waliokuwa wanaumwa. Unajua mimi nimesahau nilitaka kuja na aya hapa ambayo aya hiyo ingewasaidia wafanyabiashara wakaweza kuelewa si kitu cha mchezo si masihara.

Nimeona ni jambo ambalo kubwa lakini nitatoa tafsiri ndogo ambavyo kitu gani wanachotakiwa katika dunia huu ukitoe kwa waja wa Mwenyezi Mungu halafu na wewe uone Mwenyezi Mungu atakupa kitu gani. Kwanza kwenda kumtizama mgonjwa peke yake Mwenyezi Mungu anakutilia fungu kubwa sana ile kwenda na kumuombea dua, basi *alhamdulillah* na wewe ukishuka pale Mwenyezi Mungu kakupa kitu ambacho ni sawa sawa, na hizo pesa unazokwenda kukopa milioni mia moja arubaoni, milioni hamsini dhidi ya hapo. Lakini benki yake iko mbali ngoja mpaka uko ndio unakwenda kukuta akhera yale mambo uliyokuwa unayafanya.

Sasa jamani tunafanya nini tuna mashehe kila leo tunawakuta wale hawaendi kufanya fensi, wanakwenda kutoa dua wanawaombea shufaa wale watu utakuta mtu yuko *sakaratul-mauti* hamjaona nyie mtu, *sakaratul-mauti* si mchezo anakwenda kumuombea dua mngekuwa mnakwenda hospitali mngeingia imani, *wallah* wangeingia imani hawa wafanyabiashara wote hawa.

Si wafanyabiashara hata na sisi Waheshimiwa tatizo gani jamani mnaona tabu kwenda kutoa *sadakatul-jaria* kule, katoeni sadaka na kule mkitoa sadaka mtarudi majimboni, msifanye masihara tatizo letu hatutoi ndio maana majimboni hamrudi. Tunakwenda kutoa sadaka kwenye rusha roho kapelekeni hospitali sadaka kwenye rusha roho haifanyiki. Twendeni kule hospitali tukawasaidie, *wallahi* wengine ukiuliza kama Katibu Mkuu.

Katibu Mkuu nimeuliza umri wake sio mkubwa wa kuchosha lakini anachoka kutokana na akili anafikiri mtoto ni mdogo tu, lakini amechoka kutokana na kufikiri nini niifanyie hospitali hawezi mzigo si mchezo, babu Juma Duni huyu hapa alipumua mara tatu alipoambia Wizara ya Afya sasa hivi ameshakuwa sasa hivi hayupo alipumua mara tatu. Mimi nikamuliza Mheshimiwa vipi aah hamna lolote, mie nilishituka kumbe baada ya kuambiwa kuwa kaondoka kule kenda

sehemu nyengine si mchezo waziri mnamuona anakongeka kila siku unafikiri anakongeka, nini wizara kubwa lile.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana, na nimuombe sana Mhe. Rais kwa kuwa amewahi kupitia Idara ile tusione tabu kushajihisha wafanyabiashara wetu kwa kuweza kuchangia ile hospitali na kuweza kutusaidia. Lakini juzi nilisema mie nataka nimsaidie Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri samahani sana juzi nilisema jambo hapa ukanijibu nimefurahi sana lile, jibu Mheshimiwa sasa nataka nikuchekeshe na wewe Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri mimi nikenda hospitali kufanya *checking* ya *blood food picture* nimekwenda mwenyewe wala sikutaka ushahidi wa kinyumbani nilipofika pale nikamololewa hapa nilipokwisha nikaambiwa kuwa Mheshimiwa hapa hiyo mashine haipo nendo kule *first track,* mimi nikaenda *first track* nikafanya kile kipimo nikalipa nikatoka nikenda zangu.

Mheshimiwa wangu akaja kunambia mashine ipo inafanyakazi na kila kitu. Mheshimiwa risiti ninayo kuwa nimefanya mwenyewe *study*. Mimi nakwambia Mhe. Naibu Waziri hamniwezi kwa sababu mimi nakuwa nishafanya *research* nikisema hapa kitu kiko *up down,* sisemi kitu cha kuripuka. Mashine hiyo iko mpaka leo iko *labour* pale ipo mpaka leo na wamepata mkopo wale, kwa sababu unajua niseme kitengo hiki mwaka jana nilisema habari ya zile mashine za *cancer*, alijitahidi sana Katibu Mkuu kuzifanya lile suala *live* kwa kutafuta vitu vyengine wanakuwa wabunifu kwa kutafuta vile vitu kwa kuomba *alhamdulillah* amefanya mambo yale, tumeona vitu, hiyo ndio desturi yetu.

Hawa wanafanya mbinu za kutafuta *donors,* kuna hawa *East Africa* hawa wameleta bajeti zao wameleta fedha mle zikiingia mle ndio utaratibu ulivyo tena. Sio apewe mtu ende akanunue kitu ambaye mtu sie *specialist* yake, tatizo lenyewe liko hapo mie ndio uchungu wangu.Unajua mimi uchungu wangu kitu kinachoniuma sana kwa sababu tuna jina kubwa sana Rufaa hospitali ya Mnazi Mmoja, halafu mtu anakwenda kukichezea chezea tu kipuuzi puuzi halafu mtu anaachiwa tu hivi tu basi.

Kule kwenye *cancer* katuharibu halafu na huku mnakwenda kumuachia hilo, mimi sikubaliani nalo. Nasema kabisa arejeshe pesa zetu achukuwe mashine yake, mashine arudishe Mhe. Naibu Spika, hakuna sababu kwa nini sasa tumsamehe, lakini mashine arudishe au pesa zetu aturejeshee. Mashine za China na China hivi sasa wameshaondoka na *model* ile kabisa *long time ago* imeshaindoka *system* ile, Muhimbili wamezikataa pale. Nimefika mpaka Muhimbili kwa taarifa yenu nyinyi hamujui kuziulizia mashine zile, kwa sababu nina uchungu na Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu mimi angenijaalia ningelikuwa bilionea basi ningewekeza katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini Mwenyezi Mungu hajanijaalia, lakini hicho hicho kidogo ninakwenda kikipeleka pale hospitali. Ninakuta pale mgonjwa wangu hana bomba ninatoa, usikatae hilo.

Nimekwenda *emergency* juzi juzi, waulizanu wale hawakwambieni, kulikuwa *gloves* hamna basi tumetoa boksi nzima, watu wametoa pale nimechanganyisha watu wakatoa boksi nzima.

Sasa mimi naomba sana hili Mhe. Naibu Spika, aah! hayo mambo ya kawaida lakini hii mashine mimi sikubaliani nayo. Mimi ninajua Katibu hajui kwa sababu angekuwa anajua Katibu hapa ashamfukuza mtu kazi au ashamrukia mbili. Manaibu Waziri hujui wewe, Waziri mwenyewe hajui. Halafu tunakuwa *safe* tunachekelea *wallahi*, tunachekelea watu. Mtu anataka kuja kuangalia mzunguko wa damu katika mwili wake kama ana matatizo anaoneshwe tunakosa kifaa.

Ilikuwa kama si *first track* iliyotuokoa maana yake ndiyo mkombozi iliyobakia *first track* pale, ingebidi tungekwenda *out*. Tumekwenda kwa mwekezaji huyu wa hapa nje Mwenyezi Mungu amjaalie mtoto huyu ajiendeleze hivi hivi tutafika atuletee neema kama hizi. Eeh! hatuna taabu hii, hebu *check* vitu vya kisasa hivi si mchezo *from* India. Tuseme ukweli ulivyo hawa wawekezaji hawa kama hawa tunawataka katika dunia hii ya kwetu Zanzibar.

Wanatuonesha miujuza jinsi gani kinawezekana hichi kitu kufanywa. Ninamshukuru sana huyu Toufiq azidi na Mwenyezi Mungu ajaalie atuokoe lakini *price* kidogo atusaidie sisi wanyonge. Mimi nimuomba sana hapa awasaidie wanyonge kidogo *price* iwe ndogo kidogo ili biashara iende vizuri sana. Lakini vifaa vya kisasa tunavyo anafanya *competition* na *government*, ni vizuri na Serikali imetoa mwanya kuwa ifanyike kitu hicho.

Siyo leo mtu anatuchezea, mashine yetu twenty millions zipotee bure bure tu. Hebu tuchukueni hatua bwana, tuchukue hatua halafu tufurahi. Wallahi mimi mukichukua hatua mimi nitafurahi sana. Niseme ukweli kuwa munajitahidi kiasi kikubwa sana Mhe. Naibu Spika. Halafu leo watu wanakuchezeeni, hapana haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, Katibu hamaki kabisa, sipendi mimi nikusemeni *wallahi* katika Wizara inayonitia huruma ni moja hii, sipendi kuwasema sema mambo mengine si vizuri, wakati nyinyi munajitahidi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na Hospitali ya Kidongo Chekundu. Sasa hapa utashangaa. Hospitali ya Kidongo Chekundu kwanza wafanyakazi kidogo, hili mukitaka musitake mulikubali, nina ushahidi tosha kama wafanyakazi kidogo

kabisa Mheshimiwa lakini madaktari wake ninawashukuru sana wanajitahidi wanafanya kazi muda mrefu sana. Hili ninawasifu sana Mheshimiwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, nilisikitika sana juzi ninakwambia na mimi hapa sifichi, mimi tatizo langu ni bahari siweki uchafu ili kujisafisha vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nina mgonjwa kapigwa kalenda zaidi ya mara mbili na alichorudishwa mara ya tatu kunitafuta mimi nilisikitika sana. Mgonjwa ambaye kutafuta historia na historia inakuwa kuna *special form*. Wamerudishwa watu zaidi ya mara tatu hazipatikani fomu hizo Mhe. Naibu Spika, nimeambiwa hakuna, wanashindwa watu kufanya kazi kwa fomu. Sasa tatizo nini, hawana *photocopy.*

Please, naomba sana *photocopy* ipelekwe *immediately* kabisa, si hivyo Mheshimiwa tutawapa taabu sana wale watu wetu, watakuwa wanakwenda wakirudi hakuna historia. Kwa sababu historia inakuwa wana *special form*, lakini siku niliyokwenda niliambiwa kuwa wamekuja humu kwenye Idara wakaambiwa kuwa *photocopy machine* haikufanya kazi sijui au sijui karatasi ilikuwa hakuna.

Kule hakuna *photocopy*, kule wamejitahidi majengo mazuri kwa Wagonjwa wa Akili lakini hamna. Mhe. Naibu Spika, siku moja nilikwenda kusoma mimi, juzi juzi nilikwenda kusomeshwa. Kuna semina nilikwenda nilialikwa Mheshimiwa nilijiuliza, kumbe sisi sote humu ni wagonjwa wa akili. Hiyo semina niliyosomeshwa Mhe. Naibu Spika, humu ndani sote ni wagonjwa wa akili. Sasa utashangaa eeh! mbona mheshimiwa anasema sisi hatuna wagonjwa wa akili, eeh! ndiyo kwa sababu kuna mambo unaweza ukafanya jambo, mimi ninazungumza *sometime* yangu sauti yangu inapanda, *sometime* sauti inashuka, tayari ugonjwa huo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, automatical haki ya Mungu ninakwambia. Humu tunaweza tukafanya jambo la manyago, mtu akafanya jambo aka-*raise* issue ambayo hata haimo katika agenda, tayari ugonjwa ule. Nilivyosemeshwa ugonjwa wa akili una namna nyingi. Mhe. Naibu Spika, nilipata elimu kweli kweli, nikajua kumbe *may God*, kumbe sisi ni wagonjwa wa akili, loo! (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nilimshukuru sana yule jamaa aliyenipa taaluma, kweli kweli alinisomesha vizuri sana kuhusu ugonjwa wa akili, kujua nini maana ya ugonjwa wa akili kutambua na sababu gani ambazo zinaelimisha ugonjwa wa akili. Juzi ulizungumzia hapa suala kuhusu ulaji wa vyakula hivi Mhe. Naibu Spika. Kumbe hivi ndivyo vinavyotufanya sisi tukose madini fulani hatimaye inaelekea kuwa sisi ni wagonjwa wa akili.

Kumbe hizi mboga mboga, hivi vitu fresh hivi, mahindi bila ya kukoboa, vitu chungu nzima, kumbe Mheshimiwa ndivyo vinavyojengwa. Lakini tatizo lake kubwa kuja kuzaa *over age*, nalo hili ukizaa kwenye *over age* mtoto anayepatikana

tayari inasababisha yule mtoto kutokuwa na akili. Nayo hiyo tujilinde tuwe tusizae kwenye *over age*, nayo kumbe ni tatizo Mhe. Naibu Spika, *it is real* kabis. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ni serious kabisa hiyo, kuna mambo mengi sana yanayosababisha ugonjwa wa akili. Mhe. Naibu Spika, niseme ukweli na mengine ningesomesha hapa lakini ninaendelea.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hapa hatujawatendea haki. Ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, waongezwe watu wafanyakazi kule sehemu hiyo, lakini kusema la ukweli wenzetu bado imekuwa kama tumewatupa. Hiki kitengo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna mambo mengi yanataka kufanywa mule yanakuwa. Humu Mhe. Naibu Spika, ukenda ninataka nikwambie nendeni kaulizeni ni mdau mmoja mkubwa sana kwenye sehemu ile, ni mdau kabisa wala sikuchagua mimi hospitali gani, labda kuna nyengine imejificha ikawa sijenda na hatimaye ninakwenda kule kwa wananchi wangu siyo ninakwenda mimi kutia pozi, kule nani utamtilia pozi.

Siku moja nilikwenda kule kuna mgonjwa mmoja alinicheka sana. Sasa nikamuuliza wewe unacheka nini, anasema na mimi babu yangu ana suti kama hiyo. Sasa Mhe. Naibu Spika, ni suala ambalo kule kwa kweli tuangalie sana.

Karibuni kule Mhe. Naibu Spika, kuliangukiwa, sijui kama lile kuta limeshajengwa. Mhe. Naibu Spika, kuta halijengwi watu wanaparamia wanakwenda kuwabaka wale wagonjwa. Je, kama ikiwa kuwazi itakuwaje. Sasa kama lile kuta halijengwa basi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hivi karibuni nilienda nilipeleka mgonjwa. Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, na kule nako tukuangalie, bajeti zetu tuangalie jinsi gani ya kuweza kuwa-*play* vizuri sana mheshimiwa kwa sababu tumekutupa utaona taabu wafanyakazi kidogo ndiyo kama nilivyosema, kuna kunatakiwa ngaringari si kitu cha mchezo.

Mhe. Naibu Spika, unamkuta mgonjwa kakusimamia na kigongo wewe unafikiri utafanya nini na upo peke yako. Lakini niwapongeze sana akinamama mule ni majasiri Mheshimiwa, haki ya Mungu ninakwambia. Ninawashukuru sana akinamama, wanajua kuwa-*treat* vizuri na wanastahamili lakini ndiyo hali yenyewe bado, sijui posho yao yakoje. Kama Mhe. Naibu Spika, maposho yao wanapata kidogo basi mimi ningeomba waongezewe ili kuweza kufanikisha ili kupata maendeleo yanayostahiki.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika sehemu ya, unajua mheshimiwa kusema hapa kijisentensi kunasema kuwa kwa kushirkiana na Jamhuri ya Watu wa China huduma za *ICU* zimeimarishwa kwa kukarabati wodi ya mifupa kwa wodi *ICU* yenye vitanda vinane na kuiweka. Sasa ninajiuliza hicho kitu kimefanyika kweli. Je, tujiulize inafanya kazi. Suala lipo hapo Mhe. Naibu Spika.

Wallahi kwa huzuni sana huwezi kuamini, mimi ndiyo njia yangu ile, *sometime* siku nyengine ninapandia huku ninakwenda kule. Lakini mpaka leo siamini kama sasa hivi yumo mgonjwa ndani. Sasa naomba sana tuendane na hii dhana ya sentensi kuwa vitu vimekamilika. Tatizo lipo wapi Mhe. Naibu Spika. Njoo unijibu hili, tatizo lipo wapi kuwa mpaka leo chumba hichi cha *ICU* kipya kabisa kimeshafunguliwa, tarehe hizo zinazoonesha tarehe 10 Januari, 2015 kuwa mpaka leo *still* hakijafanya kazi, sababu nini, *gas* hamna, sababu ni kitu gani

Mhe. Naibu Spika, lakini nimesahaui hapa mapokezi, unajua sasa hivi kunako *emergency*, kwa kweli *emergency* sasa hivi Mheshimiwa hadhi yake imekuwa siyo nzuri. Mhe. Naibu Spika, *emergency* sidhani kama zile *oxygen* zinafanya kazi kabisa. Lakini na yale mapazia Mhe. Naibu Spika, yatolewe. Mapazia yamekuwa *unfit* pale, siyo pazia yale.

Mhe. Naibu Spika, mapazia hayalingani na system au na hali halisi ya kihospitali, hayatofai mapazia yale. Duu! aibu. Mimi ninaamini ingekuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ningemwambia mapazia yale atusaidie kwenda kuweka hapo, kwa sababu mapazia yale yaliyokuwepo siyo mazuri kusema la ukweli, hayalingani na kihospitali. Kwa hivyo mapazia kwa watu wengine kwenye majumba ya matajiri yanayofanywa mapazia ya ndani yale, hebu yatizameni kweli mapazia yale ya kuwekwa mule, siyo *design*, kule lazima umekosa *white*, umekosa kijani. Ndiyo unaweza ukafanya kitu kama hicho mheshimiwa, yale siyo mapazia yanayokwenda mle bwana, hebu tuondoeni.

Tuangalie kwani mita kiasi hata haiwezekani Wizara ishindwe hawa wafanya biashara waweze kununua, hebu tutafute. Halafu kuna *quality* ukishapata yale mapazia piga nembo ile ya Hospitali ya Mnazi Mmoja iendane na ile hali halisia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, emergency bado tumeyaiangusha. *Emergency* Mheshimiwa inafanya hivi la kuchekesha, wewe una mgonjwa wako leo umekwenda naye pale, basi utaambiwa uongeze dawa kumbe dawa zile zina-*recover* kwa mgonjwa mwengine na mwengine akija anafanya hivyo hivyo. Je, tuseme mtu ikishindikana ina maana mtu asitibiwe. Dawa zinakuwa pungufu pale, kwa kweli dawa zinapungua pale. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimekwenda nikayabeba machupa kumletea mgonjwa wangu aliyekuwa anaharisha pale, baada ya kwisha nikaombwa mheshimiwa hizi zibakishe hapa hapa kwa sababu hali halisi ndiyo ilivyo inaweza jioni, nikasema sawa ndiyo riski yenyewe hiyo. Kwa kweli Mheshimiwa pale mimi nimechukua pepo kwa siku ile pale.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba sana *emergency* kwa kweli bado ingali sehemu nzuri mapokezi lakini bado haijaridhisha. Halafu la pili vile vitorori vinavyobeba wagonjwa. Jamani Mhe. Naibu Spika, naomba sana vimeshapitwa na wakati. Vile vitoroli haviendi na wakati na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Naomba sana twende na wakati.

Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha hii *lift* ya pili hayaendi. Tatizo ni nini mheshimiwa. *Lift* yetu ni moja tu wengine ni heavy *weight* si mchezo Mungu atuepushie mbali, utanibebaje na kunifikisha juu wewe, huna uwezo wa kunifikisha. Mtu ana kilo mia moja na ishirini utanibeba vipi. Hatari mheshimiwa tusifanye mchezo, tunawasumbua. Kwa nini lift ile wallahi inanisumbua kweli.

Mhe. Naibu Spika, sijui sababu gani mutaniambia nini sijui. Lakini Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais alikuja akaangalia sehemu ya kuweka kumbukumbu za wagonjwa. Juzi nilienda pale nilikuwa ninatafuta kumbukumbu yangu mimi mwenyewe, nilijaribu ku-*trace* hebu naomba mimi nilifanyiwa tiba hapa ya goita, siyo *tire road*, Mhe. Naibu Spika, mbona wananikorofisha hawa. (*Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika, hakuna kumbukumbu zangu zimepotea hazijulikani zipo wapi. Hatujaweka ile *special room*. Nenda *Mental Hospital* utafurahi sana, utakuta zimejipanga ma-*file* wanaangalia alphabetical zile, zimekaa vizuri Mheshimiwa. *Wallahi* nilifurahi sana kabisa *wonderful* niwapigie kofi mheshimiwa wale jamaa. Nilifurahi nilipokwenda pale nikataja mgonjwa fulani bin fulani, hawakupata shida wala sikupata kamasi. Mimi nimetoka mule ndani nimetoka na kamasi, fyaaa! mheshimiwa si mchezo niliumwa na kichwa siku tatu.

Mhe. Naibu Spika, si kitu cha masihara. Naomba sana mheshimiwa bado kile chumba cha kuweka kumbukumbu, mheshimiwa kumbukumbu zangu hazipo, nilifanya historia nimefanya na nini ile *appendix* hakuna kumbukumbu. Mheshimiwa utashangaa makatarasi yanatiwa kwenye maboksi, maboksi yenyewe yana mavumbi mutawatia watu *TB, wallahi* watapata watu wafanyakazi wa mule ndani.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana lakini hii inatokana na bajeti finyu, siyo wao, ninataka niwaambie Katibu wangu ajisikie *fresh* kabisa, siyo yeye atafanya nini wakati hana pesa, niambie atafanya nini, hana uwezo. Atahangaika atakwenda duniani kote atapata vitu vidogo tu hawezi kumaliza vitu vyote.

Juzi nilicheka mimi kama unataka nikwambie Mheshimiwa nimesahaui kukwambieni. Nilikwenda na mimi kusaidia kubeba maji ya chumvi kwa vile vidumu, siku ya maji usiku hakuna kama ninataka nikwambieni, mimi nipo kesi ile pale, nyinyi hamjui ulizeni mutaambiwa. Nenda kawaulize wale *surgeon ward* pale watakwambieni.

Tulichukua vidumu vile tukenda tukabeba kule maji ya chumvi, sikio la kusikia ninasema hapa *alhamdulillahi* maji, mimi nikawa ninacheka wallahi laadhim kumbe mimi nimeshajua zamani. Lakini sema kwa kuwa mambo mengine ni *technical,* nyinyi siyo kazi yenu, unaona hiyo. Imekuwa nyinyi siyo kazi yenu siwezi nikawalaumini kwa sababu nyinyi ni ma-*specialists* wa masuala mengine. Kwa hivyo hayo inakuwa siwezi kutia lawamani, lakini Mheshimiwa kusema la ukweli kuwa hatupo *serious* na Hospitali ya Mnazi Mmoja, tena leo ni ya rufaa. (*Makofi*)

Ninachosema, sasa mimi ninatoa ushauri wa mwisho. Ninaomba sana ninatoa ushauri mimi, siyo mwisho kama ninamaliza, mimi nina uwezo wa kuendelea baada ya hapa. Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, nimtake sana Waziri wangu mpenzi wa Fedha tutafute sehemu ya kuongezea ki-*percent* kidogo fedha basi. (*Makofi*)

(Hapa umeme ulizimika kwa sekunde kama tano hivi)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ninaweza nikaendelea.

Mhe. Naibu Spika: Subiri kidogo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, watu wameona hilo wazo ninalotaka kulitoa ni zuri ndiyo maana wakazima umeme.

Mhe. Naibu Spika: Malizia dakika tano za mwisho, umeshachukua nusu saa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Haya. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana kutoa ushauri wangu, tena huu ushauri ni mzuri sana ambao utakaokoa kabisa Hospitali ya Mnazi Mmoja, itakuwa mambo madogo madogo, *finish*.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu upo hivi. Tulitafuta means ya meli hapa tukafanya na Mwenyezi Mungu akatujaalia *alhamdulillahi* tumeipata, tumetafuta njia ya kupata madeski, *alhamdulillahi* Mwenyezi Mungu katujaalia tumepata.

Sasa tutafute njia ya kuichangia Hospitali kwa *means* hii ambayo tuliyoifanyia njia hizi, nimuombe sana Mhe. Waziri, hebu na hii iyatie tuwaondolee mzigo, mambo mengine madogo madogo waweze kupata fedha ya kusaidia katika lile jengo kuendeleza vizuri Mhe. Naibu Spika. Niombe sana suala Mhe. Naibu Spika.

Kwa sababu jana Mhe. Naibu Spika, jana nilikwenda sehemu pale ya wagonjwa sukari. Mhe. Naibu Spika, tizama wapo watu chini sana, wapo watu wengi chini. Kile chumba chenyewe kwanza ni kidogo, chumba kimekuwa kidogo sana too

much Mheshimiwa. Hewa yote imo ndani haitoki nje, wewe unatarajia nini mtu. Jana nimekwenda bwana, watu kibao wapo chini.

Mhe. Spika, nikaambiwa ndiyo Mungu stahamilini *inshaallah* kheri nimeambiwa musiwe na wasi wasi Dkt. Ali Mohamed Shein anajitayarisha kuweka hospitali nyengine kubwa nje ya mji, nimewapa moyo wameridhika wamekaa pale, nimewaambia hilo suala.

Na hiyo ninaamini kabisa mtu na nikauliza, wakasema *alhamdulillahi gloves* zipo, vitu sijui vinaendelea vizuri, wamepata misaada, wameniambia hawakunificha waliponiona tu aah! mheshimiwa tayari mambo mazuri, tumepata *gloves* hapa, tunakwenda vizuri. Lakini nimsifu sana yule kaka anayetibu. Yule kama mmoja jina lake nimemsahau, yule kama jamani kama hamumsaidii basi itakuwa hamusaidii. Yupo mmoja pale nurse wa kike.

Mhe. Spika, *wallahi* yule jamaa Mhe. Naibu Spika, tutapata dhambi kubwa sana kaka yule kama hatukumsaidia. Kwanza amekufa wadudu hana huruma katika kutibu na ndiyo vizuri, kama hukufanya hivyo huwatibu wale. Leo kama hatumsaidii Mhe. Naibu Spika, yule tutamtia maradhi, hatutomtendea haki.

Nimuombee sana kwa Katibu mpeni posho *special*, mpeni *allowance risk* munaita *risk allowance*, mtengenezeeni mpeni mheshimiwa yule lazima nimpigie debe kwa kazi anayoifanya, kazi ya hatari. *Wallahi* Mhe. Naibu Spika, ninakwambia Katibu Mkuu mpeni raha yake, mpeni yule kaka yangu yule.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana. Kwanza niwapongeze sana. Hivi sasa ninatumia muda huu wa kuwapongeza ili ninamalizia Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri na nimpe pole kutokana na hali halisi ilivyo, kwa sababu kama nilivyosema ile hospitali imeshakuwa kubwa sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nimesahau kitengo kimoja kikubwa sana, muhimu mheshimiwa, Kitengo cha Macho. Mhe. Naibu Spika, niambiwe lile jengo lini litakuja kutengenezwa. Mpaka leo wale watu, ni raha na kule lakini kudogo hawajinafasi vizuri na tuna mashine ambazo ni *expensive*, mashine zile hazitaki kuchezewa, ukipangua tu umekula hasara.

Je, ni lini serikali itaweza kufanya yale mabadiliko ya pale, naomba sana lini mtawaondoa kule. Hebu tuwarudishe nyumbani kwao. Kitengo cha Macho Mhe. Naibu Spika, kina wataalamu wazuri, kinatibu vizuri na hata ukipelekwa Dar es Salaam basi ujuwe unakwenda kwa kazi kubwa, sio mchezo wanajitahidi na dawa zipo sasa hivi za kisasa. Kwa hivyo, naomba sana tuweze kuwarejesha.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Katibu Mtendaji mwenyewe, nimshukuru sana Naibu Katibu wake kama yupo, nimshukuru sana Naibu Waziri, Waziri mwenyewe na Wakurugenzi. Lakini Waziri wangu kama nilivyosema nikupe pole sana, sio mchezo ile wizara Mhe. Waziri unakosa sasa hivi ni kubwa sana, sio kitu cha masihara. Hata Mhe. Naibu Waziri mwanzo alikuwa yuko mnene, lakini sasa hivi mtizame anapuuka, sio mchezo kabisa, Katibu wangu anazeeka ana umri mdogo lakini saas hivi anaingia katika *over age,* kutokana na nini anafikiri nini cha kufanya. Basi usishangae na Mkurugenzi naye Jamala nimecheza naye kabisa, lakini leo anapewa shkamoo yeye wakati mimi mkubwa kuliko yeye. Tatizo ni hili hali halisi sio masihara Mhe. Naibu Spika, tuisaidie serikali.

Mhe. Naibu Spika, niwaambie sana wafanyabiashara mlango uko wazi, nendeni kwa waziri, Naibu Waziri, katibu na hata na mimi mpiga debe njooni nitawapelekeni hakuna tatizo. Waheshimiwa Wajumbe, niwaombeni kwa mara ya mwisho tuipitisheni jamani, tusiipigie buti. Hawa hawana buti hohe hahe maskini ya Mungu, tuipitishe kwa raha mustarehe, nawaombeni sana kweli kwa unyonge sana na kwa sababu hawana kitu, tutawaonea bure. Sisi tukawachangie tusione raha kupiga makofi, tukatowe michango hospitali mkasaidie. Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Makame Mshimba sio machache ni mengi. Tunampa nafasi Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa ushauri wa hapa na pale katika hoja hii muhimu sana kwa jamii yetu, ambayo iko mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 10, kuna kitengo cha ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi. Ukisoma kitabu cha Mhe. Waziri miongoni mwa majukumu ya kitengo hiki ni kuratibu, kufuatilia mienendo ya maradhi, kutafuta vyanzo na vichocheo vya maradhi pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana na maradhi, pamoja na majanga mengine yatokeayo katika jamii. Sasa hili ni jukumu muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna maradhi katika jamii yetu kwa kweli sasa yamekuwa ni tishio na kwa vyovyote vile yangehitaji sasa kufanyiwa utafiti tukaweza kujua, maradhi haya chanzo chake nini, vichocheo vyake ni nini ili tuweze kuifahamisha jamii yetu tuepukane na hili janga, maana yake nguvu kazi inapotea sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna maradhi ya kisukari, maradhi ya moyo, *pressure* wengine wanaita *stroke,* kuna maradhi ya viungo, kuna matatizo ya uti wa mgongo sasa hivi, wataalamu wanaita *disc* imepanguka mgongoni, unamkuta mtu anatembea sio

kawaida na anapoteza nguvu zake zote, na maradhi ya magoti sasa hivi miguu inakuwa haina nguvu.

Sasa wengi wetu huwa tunajiuliza kwa nini haya maradhi yamekuwa mengi, yanasababishwa na kitu gani. Tulitarajia sana Mhe. Waziri atupe taarifa za kiutafiti za kitaalamu kabisa, ili tuweze kujua maradhi haya basi yanasababishwa na kitu gani, kama ni vyakula tunavyokula ni vyakula vya aina gani vinavyosababisha hayo maradhi na kama ni tabi, ni tabia gani inayosababisha hayo maradhi ili tuweze kuinusuru nguvu kazi yetu iliomo katika jamii na tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri kama kuna taarifa zozote za kiutafiti ambazo wizara yake imefanya, basi hebu atuelimishe kama kuna mambo ambayo tunaweza kuyaepuka basi tuweze kuyaepuka, au kama kuna hatua za kuchukua lakini haya matatizo kwa kweli yatatumaliza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapa nataka niende kwenye ukurasa wa 15 ambapo pale kuna Idara ya Tiba. Mhe. Naibu Spika, moja katika kazi ambayo idara hii inashughulika nayo ni kufanya tathmini ya wagonjwa. Ukifanya *paragraph* ya 5.1.3, Mhe. Waziri anasema katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 jumla ya wagonjwa 206 walifanyiwa uhakiki na bodi ya madaktari na kati ya hao wagonjwa 156 walithibitishwa kusafirishwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi. Katika kadhia hiyo Mhe.

Naibu Spika, pesa zilizotumika ni bilioni 3,231,526,142.40/- na zilizotengwa na kuidhinishwa na Baraza hili kwa ajili ya kazi ya kusafirishia wagonjwa nje ya nchi, ilikuwa ni shilingi milioni 800,000,000 pekee. Lakini kilichotumika ni bilioni 3,231,526142.40/-. Sasa hili ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, ukenda mbali zaidi utakuta hata hawa wagonjwa waliofika kufanyiwa uhakiki, sio wote waliohitaji shughuli hii. Mimi ninavyoamini kuna wengine wengi hawakuweza kufika katika *stage* hii wakafanyiwa uhakiki, lakini kama wangefanyiwa, basi wizara siku moja ingejikuta ina wagonjwa wasiopungua 700 au 800, ambao wanahitaji kusafirishwa nje ya nchi matibabu yao hayatibiki hapa nyumbani. Sasa hii kweli ni *challenge* kubwa sana katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba kuna haja kubwa sana ya nchi yetu sasa kuweza kufikiria kutoa kipaumbele kikubwa sana, ya kuweza kusogeza hizi huduma hapa nchini kwetu. Badala ya mtu kufuatilia matibabu India au Afrika ya Kusini au Israel, kwa nini tusiweze kukata jongoo kwa meno, tukaweza ku-*invest* katika masuala haya ya tiba ili tupunguze harama kubwa sana ambazo Mhe. Naibu Spika, nchi yetu inapata kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa nje ya nchi. Najua sana kama matibabu ni ghali, madawa ni ghali. Lakini penye nia pana njia.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni baada ya kupatwa na majanga ya meli hizi tunazosafiria kuanguka mara kwa mara baharini kupoteza watu, serikali ilifunga macho ikaagiza meli hivi karibuni itafika ni pesa nyingi sana. Sasa kwa msingi huo nafikiri tukikusudia tunaweza tukabana huku na huku, lakini hatimaye tukapata basi wataalamu, tukapata vifaa vya kuweza kufanya upasuaji wa mambo ya mgongo, upasuaji wa moyo hapa hapa ndani ya nchi yetu, tunapunguza gharama kubwa sana. Tunaweza kutumia gharama kubwa mwanzo, lakini hatimaye tukawa tumepunguza gharama kubwa siku za baadae.

Kwa hivyo, nilikuwa nashauri sana waziri alipeleke hili wazo serikalini, ili serikali ilitafakari kwa makini sana. Kama mwaka huu tumetulia bilioni 3,000,000,000/- mwakani hizi zitaongezeka na mwaka unaofuata zitaongezeka tena, kwa sababu *population* inaongezeka na maradhi yanaongezeka siku hizi. Kwa hivyo, tutakuja kukuta siku moja watu wetu wanakufa tu, halafu tutashindwa kuwahudumia.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 27 ambapo pale pana Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niipongeze wizara, kwa kulitilia maanani na kulipa umuhimu hili jambo, kwa sababu wananchi wetu kwanza ni masikini, dawa za kuweza kumtibu mtu sasa ni ghali. Mhe. Naibu Spika, dawa tunazotumia hapa Zanzibar hazina ubora wowote. Dawa unazokula kwa maleria hapa ukenda hapo Kenya hutumii hizi, unatumia dawa nyengine ambazo ni ghali na wananchi wetu hawawezi kuzinunua.

Mhe. Naibu Spika, mtu akiumwa na kichwa au maradhi yoyote dawa anayopewa basi akienda nchi nyengine, dawa ile hasa hawaitaji kama ni dawa ya kuweza kumsaidia mtu. Sasa tunakula kwa ukosefu. Lakini ukweli ni kwamba wananchi wetu hawana uwezo kabisa wa kujihudumia katika matibabu na matokeo yake sasa tumelimbikiza masumu tu mwilini, unakula madawa unachoongeza ndani ya mwili ni sumu maradhi hayaondoki. Sumu zile zinazalisha maradhi mengine mengi, mengine ndio haya tunasema yanaendelea kuongezeka sasa hivi. Kwa hivyo, kuwa na *alternative* kwa mazingira yetu ni jambo muhimu sana, ndio maana nikasema naipongeza sana wizara kwa kulizingatia hili.

Mhe. Naibu Spika, tumeambiwa humu kuna karibu waganga 205 wamesajiliwa kwa ajili ya kutoa tiba mbadala. Lakini bado dawa wanazouza mara nyengine zinakuwa ghali, kwa sababu wengine ni kampuni kutoka nje. Kuna Kampuni moja ya Kichina kama huna pesa bora usiende kabisa, wana dawa nzuri lakini dawa zao ni ghali sana.

Mhe. Naibu Spika, sisi mazingira yetu Mwenyezi Mungu katupenda sana, ardhi yetu ni ya kijana, kila mtu unaouona nje ya mazingira yako ni dawa. Tatizo tulilonalo hatujui kama hii ni dawa ya maradhi gani na hii ni dawa ya maradhi gani. Sasa nilikuwa naomba sana kitengo hiki au wizara kwa jumla kwa kweli

itafute wataalamu wa miti shamba, shamba tunazo za kutosha kabisa. Kama tungekuwa tunajua basi tungekuwa tunajitibu kwa gharama nafuu sana. Kwa hivyo, tupate wataalamu wanaojua miti shamba na wako duniani.

Hapo Nigeria kuna wataalamu wa kutosha wa miti shamba na wao kule wamefungua mashule maalum ya kufundisha watu tiba za mitishamba na wako mbali sana sasa. Sasa kwa mazingira hapa kwetu hilo ni rahisi. Kwa hivyo, wizara hii itafute wataalamu halafu waandae mitaala maalum, wafanye utafiti na waandae mitaala, sio vibaya hata mitaala hiyo ikaletwa shule ili jamii yetu ikafundishwa mitishamba hii na faida zake.

Mhe. Naibu Spika, jana nilikuwa naangalia *ZBC TV*, kuna mama mmoja anaitwa Hawa na bwana mmoja anaitwa Yussuf, walikuwa wanatoa faida za miti fulani. Kuna mti mmoja unaitwa mpande sijui kama hivi aliokuwa anauzungumzia, una faida chungu nzima na huo mti hapa kwetu upo. Kuna mmoja nimeusahau jina lake, lakini miti ina faida sana. Ingekuwa watu taaluma hizi wanazo wala wasingekwenda kupiga foleni pale Mnazi Mmoja hata siku moja, tungekuwa tukijitibu wenyewe kabisa.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili alipe kipaumbele na serikali itowe kipaumbele maalum. Sasa jamii yetu ifundishwe tiba hizi za miti shamba tutapunguza gharama kubwa sana serikalini, maana yake serikali inalazimika sasa hivi kuagizia madawa wala hatuna pesa, tunawategemea wafadhili, tunaona changamoto humu. Tunawategemea wahisani, hao wahisani hawatupi pesa za kutosha, kwa hivyo matokeo yake ukienda kwenye Vituo vya Afya hakuna dawa. Lakini ukimfundisha mtu akijua kwamba mimi nikipata maleria niende nikatafute vilele vya mpapai nakunywa, basi muhimu ajuwe kiwango tu kwa sababu na zile dawa pia zina matatizo yake. Lakini ukimsomesha akijua kiwango cha kutumia haji hospitali atajitibu mwenyewe. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana hili jambo nalo lipewe kipaumbele cha kutosha. Tuna malighafi ya kutosha kabisa katika nchi yetu ya miti ambayo yote ni dawa tunaweza tukajitibu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye Hositali ya Mnazi Mmoja. Hospitali hii tuna azma ya kuifanya Hospitali ya Rufaa, muda mrefu tunataja taja hii. Lakini hatujafikia kiwango cha kuifanya ile kuwa Hospitali ya Rufaa. Kwanza hatuna madaktari mabingwa wa kutosha, lakini pili, hatuna vifaa na tatu hata miundo mbinu ya pale hospitali bado haijakuwa tayari kuifanya ile Hospitali iwe ya Rufaa.

Sasa mimi nilikuwa nashauri sana na nimeona humu pahala wizara inasomesha madaktari. Kuna madaktari wanakwenda kufanya udokta watatu, wengine saba wanachukuwa *Master* sasa hii itasaidia sana, lakini bado itakuwa haijatosha. Lakini jambo jengine ambalo linasumbua kwanza usafi nao pale Mnazi Mmoja haujawa katika kiwango.

Jambo jengine muhimu ni kujaribu iwezekanavyo, nayo nimeona kuna mradi huo kuzipandisha daraja hizi hospitali nyengine za Wilaya na Vijiji, ziweze kutoa huduma ambazo zinapatika pale Mnazi Mmoja kwa hivi sasa, ili ule mkusanyiko wa watu pale upunguwe pasiwe na zogo, maana yake Hospitali ya Rufaa inataka iwe shuwari sana kwa sababu wagonjwa wanakuja pale ni wagonjwa wakubwa sana na wenye matatizo makubwa. Kwa hivyo, pakiwa na *chaos* la namna ile hata wagonjwa hawana raha.

Kwa hivyo, tutakapoziwezesha hospitali hizi pembeni pembeni humu, zikaweza kubeba ile mizigo inayokwenda pale Mnazi Mmoja, basi hospitali ile itakuwa haina vurugu la watu na hapo nafikiri itakuwa rahisi zaidi kuifanya iwe Hospitali ya Rufaa. Lakini cha msingi ni kupata vifaa, kwa sababu ili iwe Hospitali ya Rufaa lazima iwe na vifaa ambavyo zitaweza kutibu wagonjwa wakubwa wale wazito. Sasa hili bado hatujawa tayari sana.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nyimbo yetu tunaimba mara kwa mara, kwa kweli ni maadili ya madaktari wetu. Madaktari wetu kuna haja maalum ya wakubwa wa kitengo wajitahidi kuwafundisha vijana wetu. Wale vijana bado ni wadogo hawajajua mambo mengi. Kwa hivyo, ukienda pale mara nyengine lugha zao hata vile ambavyo wanamkabili mgonjwa inakuwa ni usumbufu mkubwa, na hakuna mtu mnyonge kama mgonjwa.

Mgonjwa mnyonge sana, anahitaji lugha za kumpa moyo, anahitaji hata kama maradhi yake daktari keshaona kama maradhi haya kupoa ni tatizo lakini usimpe lugha ya kumkatisha tamaa ile ni saikolojia maalumm, vijana wetu wengi hawana. Kwa hivyo, namuomba sana waziri kwa kushirikiana na *Management* ya Wizara yake wajitahidi sana kusema nao vijana wetu wanaotoa huduma kwa wagonjwa, ili waweze kutumiam lugha za upole.

Mhe. Naibu Spika, kutoka mtu kwenda kumjuilia mgonjwa ni ibada kubwa na ni abada ambayo anapata mathawabu mengi kweli kweli, hadi yule anayemtibu, yaani wewe unakwenda kumuangalia tu, ukamwambia pole Mwenyezi Mungu atakusaidia hivi na hivi, basi Mwenyezi Mungu anakuandikia mathawabu mengi. Kesho akhera waliokuwa hawana ibada hii Mwenyezi Mungu atawalaumu sana. Wewe walikuwa waja wangu wanaumwa hukwenda kuwaangalia, atakulaumu Mwenyezi Mungu. Sasa wewe uliko pale hospitali tayari tena unalipwa siku nyengine, japo unachopewa ni kidogo lakini unalipwa. Kwa nini huitumii hiyo kama ni ibada ukawa huku unatekeleza kazi yako lakini unapata na thawabu. Lakini unatoa lugha, nasikia hapa Wakurugenzi wengine wakilalamika, kuna akina mama wanahiari wakajifungulie majumbani kwao, kwenye wakunga wale wa mitaani kwa sababu ya usumbufu wanaoupata kule.

Kwa hivyo, naomba sana hili Mhe. Waziri alivalie njuga kila kazi ina saikolojia yake bwana. Ukienda dukani kwa Muhindi bwana hata kama hutaki kutumia wewe utatumia tu, kwa sababu wana saikolojia ya biashara, atakubembeleza wewe utatumia tu japo kidogo. Sasa na pale hospitali napo pana lugha yake, ili mgonjwa apate nafuu kuna lugha ya kumwambia. Sasa naomba sana hili suala lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, muda umekwisha ni ukurasa...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba kuunga mkono hoja ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe kwa ushirikiano mlionipa jioni hii, tumepata wachangiaji wanane. Watatu tayari wamekwisha changia, wamebakia Mhe. Saleh Nassor Juma (Muasisi), Mhe. Mohd Haji Khalid (Kingunge), Mhe. Mohd Mbwana Hamad, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Fatma Mbarouk Said, watachangia kesho tukijaaliwa. Naakhirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 03/06/2015 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku kikao kiliakhirishwa mpaka

tarehe 03/06/2015 saa 3:00 asubuhi)